**20 APRILI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 20 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Tatu, Kikao cha Kumi na Mbili, leo tarehe 20 Aprili, 2026.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. KAFITI W. KAFITI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 128

**Ujenzi wa Mfereji Mto Ngerengere**

**MHE. SHEILA E. LUKUBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga mfereji mkubwa kuelekeza maji Mto Ngerengere ili kunusuru Wakazi wa Kata ya Kihonda na Lukobe kwa mafuriko?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Kihonda na Lukobe katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro zimekuwa zikiathiriwa na mafuriko ya mara kwa mara nyakati za mvua. Ili kutatua changamoto hiyo, Serikali imepanga kujenga mifereji ili kuyaelekeza maji katika Mto Ngerengere. Serikali imeunda timu ya wataalam kwa ajili ya kufanya tathmini na kuandaa andiko la mradi ambalo litaonesha mahitaji halisi na njia nzuri ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ya tathmini inatarajia kukamilisha kazi hiyo kabla au ifikapo Septemba, 2026. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba.

**MHE. SHEILA E. LUKUBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majawabu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; Kata za Kihonda na Lukobe hazikuwahi kupata mafuriko huko nyuma, lakini baada ya ujenzi mkubwa wa Reli ya Kisasa ya *SGR* kumeibuka makorongo makubwa yaliyopo Kwa Wagogo, Juhudi na Azimio. Makorongo haya kwa ujumla yamekuwa yakisababisha mafuriko makubwa na kuathiri mali na miundombinu ya wananchi. Je, lini Serikali itajenga miundombinu imara ili kudhibiti mafuriko na ili kunusuru maisha ya wananchi hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Mkoa wa Morogoro ni wanufaika wakubwa wa Mradi wa *SGR* na sisi sote ni mashahidi tumekuwa tukitumia, lakini kuna changamoto ya vivuko katika Kata ya Lukobe, Mtaa wa Tushikamane, karibu na Shule ya Sekondari Mji Mpya na Mtaa wa Kambi Tano ambao ni mpaka wa Mvomero na Morogoro Mjini. Nini kauli ya Serikali juu ya vivuko hivyo? Kwa sababu imekuwa ahadi ya muda mrefu kwamba wananchi hawa watatengenezewa, nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Morogoro. Amekuwa mfuatiliaji wa karibu sana wa shughuli za ustawi wa wananchi wa Mkoa wa Morogoro, lakini na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge Lukuba kwamba, kwanza Serikali inatambua kwamba tuna changamoto ya mafuriko katika mitaa ya wananchi katika Kata ya Lukobe na Kihonda Morogoro Manispaa na tayari tumeshatuma wataalam. Timu ya wataalam inafanya tathmini maeneo gani yanahitaji miundombinu ya aina gani na gharama za fedha zinazohitajika ili baada ya kukamilisha tathmini ya mahitaji na *design* tutapeleka fedha kwa ajili ya kujenga mfereji wa kupeleka maji yale ya mafuriko kwenye Mto Ngerengere ili kuondoa mafuriko hayo. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kihonda na Lukobe kwamba, Serikali inalifanyia kazi na tutakwenda kumaliza changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tunafahamu kwamba viko vivuko ambavyo vinahitaji kujengwa na kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, Kivuko cha eneo la Tushikamane lakini pia Kivuko cha Mtaa wa Kambi Tano. Ninaomba nimhakikishie tu kwamba, wakati wa ujenzi wa mfereji huo tutapeleka *package* ambayo pia itakwenda kujenga madaraja, lakini pia kujenga vivuko hivyo ili kuondoa changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela, Mbunge wa Maswa Mashariki.

Na. 129

**Ukarabati wa Barabara ya Senani – Gula**

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA** aliuliza:-

Je, lini Barabara kutoka Senani hadi Gula itakarabatiwa ili iweze kupitika wakati wa masika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Senani – Gula ni barabara inayounganisha Kata ya Senani, Mpindo na Kata ya Lalago katika Barabara ya Senani – Zebeya – Lalago katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa yenye urefu wa kilometa 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imeanza kufanya ukarabati wa barabara hiyo urefu wa kilometa 12 kwa gharama ya shilingi milioni 125, ambapo kazi hiyo inaendelea na mkandarasi anaendelea na kazi. Kazi nyingine zinazoendelea katika barabara hiyo ni pamoja na kunyanyua tuta meta 320, kujenga makalavati mistari mitatu na kuchimba mitaro kilometa 6.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea na ukarabati wa barabara hii, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga shilingi milioni 200 kwa utekelezaji. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa vile barabara hii ilikuwa na changamoto ya kupitika kabla ya mvua za mwaka huu na mvua za mwaka huu zimenyesha kwa wingi na kuiharibu zaidi. Je, ni ipi tathmini mpya ya Serikali ya kuhakikisha kwamba

ule uharibifu ambao umetokea mwaka huu unafanyiwa kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuambatana nami kwenye jimbo ili kujionea hali halisi ya barabara hii, lakini pia na barabara nyingine katika Wilaya ya Jimbo la Maswa Mashariki?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela, Mbunge wa Maswa Mashariki amefuatilia sana barabara hii Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na sisi tunamhakikishia kwamba tutahakikisha barabara hii inaendelea kujengwa. Tunafahamu kwamba kumekuwa na mvua nyingi na uharibifu umeendelea kutokea, hasa msimu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi ambao umekuwa ukifanyika, tunaendelea kufanya tathmini ya uharibifu mwingine ulioongezeka kwa ajili ya kutenga bajeti kwa ajili ya kwenda kufanya ukarabati huo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Lugomela kwamba, tutafanya tathmini na kazi hiyo inaendelea na taarifa tunaendelea kuzipokea, Ofisi wa Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa barabara hiyo, lakini na barabara nyingine zote kote nchini kwa ajili ya kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya dharura, lakini na matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Dkt. Lugomela kwenda Maswa Mashariki. Tutakaa mimi na wewe Mheshimiwa Mbunge tupange ratiba na tuone lini tutapata fursa twende tukakague barabara hii na barabara nyingine kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunaboresha usafiri na usafirishaji kwa wananchi. ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fagason Nkingwa, swali fupi la nyongeza.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara zimekuwa zikiharibika nchi nzima, lakini ninayo barabara inayotoka Lulembela – Kiseke ambayo imekuwa ni hatari sana kwa wananchi wangu wa Jimbo la Mbogwe. Je, ni lini Serikali itaenda kutengeneza barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Fagason, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe kwamba, tunafahamu sana umuhimu wa barabara hiyo na tayari Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Geita na Wilaya ya Mbogwe tumeshawapa maelekezo wawasilishe gharama zinazohitajika kwa ajili ya kufanya marekebisho na matengenezo ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba, tunaendelea kuandaa utaratibu wa fedha na mara baada ya mvua hizi ambazo zimeendelea kunyesha kwa muda mrefu kupungua, Serikali itaanza kupeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo. Nimhakikishie tu hiyo barabara tutaipa kipaumbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faraji Nandala, swali fupi la nyongeza.

**MHE. FARAJI B. NANDALA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Hali ya barabara kwenye Jimbo la Ndanda ni changamoto kubwa sana, hasa Barabara kutoka Kata ya Mlingula, Kata ya Namajani, Kata ya Namatutwe kuelekea Kata ya Msikisi. Ni lini Serikali itaanza rasmi ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko barabara ambazo zinaendelea kujengwa kwa

kiwango cha changarawe, kiwango cha udongo na kiwango cha Barabara na Serikali hii imeweka mpango wa kuhakikisha tunahama kwenye ujenzi wa barabara za udongo kwenda zaidi kwenye changarawe, lakini pale panapowezekana kujenga barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, wakati wa utekelezaji wa mipango yetu ya ujenzi wa barabara tutaifanyia tathmini barabara hiyo na kuona uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kwa awamu. Kwa changarawe ama kwa lami kwa kadri ambavyo fedha zitakuwa zimepatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Chanyamisa – Bujara – Kihanga katika Kata ya Nyakasimbi imeharibika sana kutokana na mvua zinazoendelea, na Mheshimiwa Naibu Waziri anajua nimemfuata kuhusu hili. Je, ni lini barabara hii itapata fedha ili iweze kutengenezwa pamoja na barabara nyingine ambazo nimewasilisha kwake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kaka yangu Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Jimbo la Karagwe amefuatilia mara kadhaa barabara hizi na amefika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na ametuletea. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anawapambania wananchi wa Jimbo la Karagwe. Ninaomba nimhakikishie tu kwamba, tayari tumeshazipokea barabara zile na tunaendelea kuandaa utaratibu wa fedha ili kuanza ukarabati na ujenzi wa miundombinu muhimu katika barabara zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba niwahakikishie wananchi wa Karagwe na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali

sikivu itakwenda kutekeleza miradi ya barabara hizo. ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 130

**Mikopo ya 10% kwa Wanawake wa Vijijini**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa kurahisisha upatikanaji wa mikopo 10% kwa wanawake wa vijijini wanaokumbana na changamoto za mfumo wa mtandaoni?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto za mfumo wa mtandao katika maombi ya mikopo ya 10% kwa makundi maalum yakiwemo ya wanawake wa vijijini, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuwawezesha waombaji kufanya usajili wa maombi ya ana kwa ana ambapo Maafisa Maendeleo ya Jamii kupitia Kamati za Kata za Huduma za Mikopo huvisaidia vikundi visivyokuwa na uwezo wa kutumia Mfumo wa kieletroniki wa WEZESHA katika kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali imeendelea kuendesha mafunzo, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 shillingi bilioni 26.3 imetengwa kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji, ikiwemo

shillingi bilioni 7.9 ambapo jumla ya vikundi vya wanawake 24,064 vimefikiwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; vikundi vingi vilivyopo vijijini katika Mkoa wa Mtwara vinajikita katika shughuli za kilimo, lakini moja ya kigezo ni kuonesha mashamba na wakati mwingine mazao hakuna. Je, Serikali haioni haja ya kuondoa hicho kigezo na kuzingatia uzalishaji ili wanawake hao waweze kupata mkopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi vingi vimekuwa havikidhi vigezo hasa kwa kuwa hawana *NIDA* na hii ni katika maeneo mengi. Je, Serikali haioni haja, kwa kuwa hawa wananchi wanatambulika katika vijiji vyao, kupata barua kutoka kwa Serikali za Vijiji ili waweze kutambulika na kupata mikopo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza sana dada yangu na Katibu wetu Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum Mtwara. Kwa kweli amekuwa akichapa kazi sana kuwasemea wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafahamu kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya mikopo ya 10% kuna maelekezo ya namna ya kuhudumia mikopo hiyo na hasa muda wa kuanza kurejesha mikopo ya 10%. Muda wa kuanza kurejesha mikopo hiyo unategemea aina ya shughuli. Wapo akina mama ambao ni wakulima na mara nyingine wanakopa kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunawapa muda, kwa sababu tunafahamu kilimo uwekezaji wake unachukua muda mpaka baada ya kuanza kupata mazao ili kuanza kufanya marejesho. Katika jambo hilo tutaendelea kuhakikisha tunalisimamia ili wapate *grace periods* na baada ya hapo waanze kurejesha mara mazao yanapokuwa yamefika msimu wake wa mavuno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni kweli kwamba ili upate mikopo hii kuna *component* ya *NIDA*, lakini Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba alishatoa maelekezo kwamba, kama mwananchi hana *NIDA* lakini anafahamika katika eneo lake la kijiji au la kata, ana haki ya kupata mikopo hiyo. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hili tumelichukua na tunalifanyia kazi ili kurahisisha mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samira Amour, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SAMIRA K. AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kuwafikia wanawake wa vijijini, Mkoani Kagera, kwa kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo hiyo bila kikwazo cha mtandao? Ahsante, *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kagera na ninamhakikishia tu kwamba, Serikali inafahamu kwamba tuna maeneo ya vijijini na maeneo hayo mara nyingine vikundi hivi vinapata shida au ugumu wa kuwafikia Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo limefanyika, moja ni kuhakikisha kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii wanafanya *outreach* Huduma Mkoba, kwa maana ya kwenda kwenye vijiji

na kwenye kata kwa ajili ya kutoa elimu, kuhamasisha na kuviwezesha vikundi maalum kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumeunda Kamati za Mikopo katika ngazi za kata na kamati hizi zinahusika kuwafikia wananchi katika vijiji. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kulisimamia hili, lakini tumelichukua kuongeza nguvu zaidi kwa Mkoa wa Kagera na mikoa mingine ili kuhakikisha kwamba vikundi hivi vinafikiwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii na zile Kamati za Mikopo ili kutoa mikopo kwa ufanisi mkubwa zaidi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 131

**Ujenzi wa Soko la Mazao, Mkalama**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko kubwa la Mazao ya Kilimo Wilaya ya Mkalama kama ilivyoahidi kwenye Ilani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga soko la mazao katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama. Kwa kutambua umuhimu huo, tayari Halmashauri imepima na kupata hati miliki ya eneo la ujenzi wa soko lenye ukubwa wa ekari 7.2 katika Kata ya Nduguti ambapo ni Makao

Makuu ya halmashauri na tathmini ya mazingira katika eneo hilo imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayoendelea ni kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi huu ambao unatarajia kukamilika Juni, 2026. Baada ya upembuzi yakinifu kukamilika Serikali itatenga bajeti na kuanza ujenzi wa soko hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca David Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Zaidi ya nusu mwaka sasa toka nyaraka zote muhimu kukabidhiwa kwenye mamlaka husika, ikiwepo barua, andiko la mradi, pamoja na *environmental and social impact assessment,* lakini mpaka sasa hakuna majibu yoyote. Swali la kwanza; wananchi wa Wilaya ya Mkalama wanataka kujua, barua na nyaraka zao zimekwamia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; toka mwaka 2012 wilaya hii ilipoanzishwa, wakulima wanapoteza mapato yao 40% kwa sababu ya ukosefu wa soko. Ninaomba commitment ya Serikali, ni lini wanakwenda kujenga soko, ili wananchi wapate ajira, tuongeze pato la mtu mmoja mmoja pamoja na pato la halmashauri? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Iramba Mashariki, anawatendea haki sana wananchi wa Jimbo la Iramba Mashariki. Anawasemea kwa dhati kabisa, ameleta hoja hizi mara kadhaa na Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imezipokea kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunafahamu kuna uhitaji wa kujenga soko la mazao na ndiyo maana tayari timu ya wataalam ipo *site* tunavyoongea sasa na Juni au kabla ya Juni

tutakuwa tumepata *design* yote, lakini na usanifu wa kina na baada ya hapo sasa tunatafuta fedha, kwa ajili ya ujenzi. Kwa hiyo, jambo la kwanza namhakikishia hakuna nyaraka ambayo haijafanyiwa kazi, nyaraka zote ambazo zimeletwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kutoka Mkalama zimefanyiwa kazi, ndiyo maana timu ipo pale *site*. Namhakikishia yeye na wananchi wa Mkalama kwamba, jambo hilo linakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tunafahamu kwamba, kuna upotevu wa mazao baada ya mavuno na wananchi wa Mkalama wanahitaji kupata soko, ili kuokoa mazao yanayopotea baada ya mavuno. Ninaomba nimhakikishie tu kwamba, tutakwenda kujenga soko hilo mapema iwezekanavyo baada ya fedha na usanifu huo kupatikana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Mheshimiwa Waziri, Kata ya Kisukuru yenye wakazi zaidi ya 50,000 haina soko, kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya wananchi wa Kata ya Kisukuru na haijawahi kabisa kuwa na soko na inasababisha wananchi hawa kwenda kutafuta mahitaji kwa kutembea umbali wa kilometa nne. Ninaomba kufahamu kauli ya Serikali, ni lini watajenga soko ndani ya Kata ya Kisukuru ili wananchi waweze kupata mahitaji yao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Segerea, lakini ninaomba nitoe Kauli ya Serikali kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwamba, tumetoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini, likiwemo Jiji la Ilala, kwamba, katika maeneo yote ambayo yanahitaji huduma muhimu kwa wananchi, kama masoko, katika mipango yao ya kila mwaka ya mapato ya ndani lazima waweke kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam ni moja ya majiji ambayo yana mapato makubwa zaidi katika nchi yetu. Kwa hiyo, ninatumia nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kwamba, wafanye tathmini eneo la Kata ya Kisukuru waone uwezekano wa kuanza kutenga fedha kwa awamu, kwa ajili ya kujenga soko kwa sababu, ni huduma za jamii, lakini pia, ni chanzo cha mapato kwa Jiji la Dar es Salaam. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Itwangi.

Na. 132

**Ujenzi wa Barabara Kahama – Mji Mdogo wa Didia**

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha Barabara ya lami ya Kahama – Njiapanda ya Lohumbo, Mji Mdogo wa Didia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Jimbo la Itwangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Didia – Solwa yenye urefu wa kilometa 55.3 inayounganisha Majimbo ya Itwangi na Solwa imekuwa ikitengewa fedha na Serikali, kwa ajili ya ukarabati. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetumia shilingi milioni 131.78 kuchonga kilometa 14, kuweka changarawe na ujenzi wa makalavati matatu. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla shilingi milioni 318.94 zilitumika, kwa ajili ya kuchonga na kuweka changarawe kilometa 13, pamoja na ujenzi wa makalavati manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha barabara kinachoombewa kuwekwa lami kina urefu wa kilometa 4.5 kikiwa ni sehemu ya Barabara ya Didia – Solwa inayoanzia katika Barabara ya Tinde – Isaka – Ushirombo. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini umeweka katika mipango yake ya mwaka wa fedha 2026/2027 kufanya usanifu, kwa ajili ya kipande hiki cha barabara kwa lengo la kujua gharama halisi za utekelezaji wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada kujua gharama halisi, Serikali itaweka kwenye mipango ya fedha, kwa ajili ya kutekeleza ujenzi kwa tabaka la lami kipande cha Barabara ya Njiapanda ya Lohumbo, Mji Mdogo wa Didia, kilomEta 4.5. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Azza Hillal Hamad.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwa wananchi wangu wa Jimbo la Itwangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa, Barabara ya kipande hiki kidogo cha Njiapanda ya Lohumbo kwenda *center* kubwa ya Didia ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Itwangi na kwa halmashauri kwa ujumla, ukizingatia Mji Mdogo wa Didia unakuwa kwa kasi kwa biashara ya mchele na biashara nyingine, lakini Serikali imewekeza fedha nyingi kwa ujenzi wa reli ya mwendokasi na kujenga *station* katika Mji huu Mdogo wa Didia. Je, Serikali ipo tayari sasa kufanya usanifu huu haraka iwezekanavyo, ili kuupa hadhi Mji Mdogo wa Didia na kuipa hadhi *Station* ya Reli ya *SGR*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari sasa kuongozana na mimi kwenda kuona hali halisi ya Mji wa Didia jinsi ulivyo, unavyokuwa kwa kasi na unavyoingizia halmashauri mapato na kuona changamoto kubwa iliyopo katika barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Jimbo la Itwangi, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, amekuwa akifuatilia mara kadhaa kuhusiana na ujenzi wa barabara zake, ikiwemo barabara hii muhimu ya kilometa 4.5. Kwa hakika wananchi wa Itwangi wamempata Mbunge anayefanya kazi kubwa sana kwa ajili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Itwangi kwamba, Serikali inatambua sana umuhimu wa barabara hii kwa sababu, pale kuna Kituo cha *SGR*, lakini pia, kuna huduma nyingi za kiuchumi na kijamii ambazo zinaongezeka kila siku. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, timu yetu ya wataalam ipo hatua za mwisho za kukamilisha tathmini. Ninatumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Shinyanga, pamoja na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya, wahakikishe wanasimamia ukamilishaji wa tathmini haraka iwezekanavyo na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa ajili ya kutafuta fedha ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, nipo tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kufanya ziara katika Jimbo la Itwangi tuweze kuona barabara zetu na tuone namna nzuri ya kuboresha miundombinu hiyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Barabara inayotuunganisha kati ya Shirati – Minigo na Kata ya Nyamtinga Rung'enye imeharibika kwa muda mrefu na haipitiki kwa sasa. Ninataka kujua Serikali ina mpango gani juu ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha changarawe, pamoja na makalavati yanayozunguka barabarani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Wambura Chege kwamba, Serikali hivi sasa inafanya tathmini ya barabara zote zilizokatika kufuatia mafuriko na mvua nyingi. Tutatoa kipaumbele kwenye barabara hiyo katika Jimbo la Rorya, kwanza, kupata taarifa za tathmini na mahitaji ya gharama mapema. Pili, kutenga fedha, kwa ajili ya matengenezo, ili barabara iweze kupitika wakati tunaendelea kupanga mipango ya muda wa kati na muda mrefu, kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kadiri itakavyoonekana inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ninamhakikishia kwamba, suala hilo tumelichukua, tunalifanyia kazi. Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Mara na Wilaya ya Rorya wakamilishe tathmini ya barabara hiyo mapema iwezekanavyo na kuiwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa sababu, tupo hatua za mwisho za ku-*comply* yale mahitaji ya kupeleka fedha, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 133

**Ajira ya Vijana Wanaojitolea Serikalini**

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa ajira vijana wanaojitolea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008, Toleo la Pili, ikisomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 na Mwongozo wa Kujitolea katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2025, ajira katika Utumishi wa Umma hupatikana kwa ushindani na uwazi. Kujitolea katika Utumishi wa Umma huwezesha vijana kujipatia ujuzi wa ziada pamoja na kuwapa uzoefu na uwezo wa kushindana pindi ajira zinapotangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vijana wote wanaohitimu vyuo wanapata fursa ya kujitolea katika Taasisi za Serikali hivyo, utaratibu uliopo wa ushindani unatoa fursa sawa kwa vijana wote wanaojitolea na ambao hawajapata fursa ya kujitolea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninamshukuru Naibu Waziri, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, ndugu yangu, Mheshimiwa Regina Ndege, kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira ya Mwaka 2008, Toleo Namba Mbili pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 na Mwongozo wa Kujitolea wa Mwaka 2025. Ninaomba nitoe ushauri, Mwongozo huo wa Mwaka 2025, basi ufike haraka katika Taasisi za Serikali, pamoja na Taasisi za Sekta Binafsi ili watumishi hawa wa kujitolea wanapopata huduma hii iwe katika uwiano katika taasisi tofauti. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ushauri huo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Lucy kwa namna anavyoendelea kuwasemea watumishi na vijana wa nchi hii. Ushauri wake tumeupokea. Hata hivyo, ninapenda kulihakikishia Bunge lako kwamba, utaratibu tuliouweka, kama Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kwamba, mwongozo tayari umetoka. Hatua iliyobaki ni kuhakikisha mwongozo huo unasambazwa na kufika kwenye taasisi zetu za umma na kwenye idara na Wizara mbalimbali, ili uanze kutumika, kwa ajili ya kuwapata vijana ambao wapo tayari kujitolea katika utumishi wa umma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Paulo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwa kuwa, idadi hii ya vijana wanaojitolea nchini ni kubwa sana. Je, Serikali haioni kuwa, kuna umuhimu mkubwa sasa wa kufanya takwimu na tafiti, kwa ajili ya idadi ya waliojitolea kwa miaka mitatu hadi sasa, ili Serikali ione namna pekee ya ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia, zungumza kwa ufanisi akuelewe. Naona Naibu Waziri anapata mashaka na swali lako.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, vijana wengi sasa hivi wanajitolea kwenye shule zetu na tunashindwa kuwaambia wasiendelee kujitolea kutokana na umuhimu wa nafasi walizoshika na masomo wanayofundisha. Serikali haioni kuwa, ni wakati muafaka sasa wa kuchukua takwimu sahihi ya vijana hawa waliyojitolea kwa miaka mitatu, ili iweze kutoa mwongozo sahihi wa namna ya hao vijana watakavyohudumiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

Kama nilivyosema kwamba, utaratibu wa ajira sasa unaenda kwa njia ya ushindani kwa sababu, tumejiwekea sera ambayo inatuongoza namna ya kuwapata watumishi wanaoingia katika ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la nyongeza linaeleza namna ambavyo tunaweza kuwatazama kwa karibu wale vijana ambao wanajitolea kwenye shule zetu; tayari Ofisi ya Utumishi imeanza kuweka mkakati wa kuwafuatilia vijana hawa, ambao wanajitolea, lakini utaratibu upo palepale kwamba, watafuata mwongozo ule wa kujitolea wanapoingia kwenye ajira zile za kujitolea, hasa kwenye shule zetu. Kama nilivyosema, mwongozo huu utaelekezwa kwenye shule, utaelekezwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwenye taasisi, kwenye Idara na Wizara zote, ili utumike, kwa ajili ya kuwapata vijana wa kujitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira zile za kujitolea ni kuwaandaa vijana wetu waendeleze taaluma walizozipata vyuoni au shuleni, ili wanapokwenda kupambana katika ajira waweze kutumia vizuri ujuzi walioupata. Kwa sababu, wanapopata ile nafasi ya kujitolea inawapa uwanja mpana wa kuelewa *field* au kada zao, ili waweze kupambana katika ushindani wa ajira. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuajiri wanasaikolojia katika ofisi na idara zote za Serikali, ili kuongeza ufanisi kwa sababu, huenda kutokufanya kazi vizuri kunasababishwa na matatizo ya saikolojia? Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi niweze kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Taya, kama alivyouliza. Ni ukweli usiopingika katika ofisi zetu, katika taasisi zetu, watumishi wengi wanapata changamoto na wakati mwingine inasababisha hata wasifanye kazi vizuri. Ofisi yetu tayari imeona kuna tatizo hilo, tupo kwenye kuandaa mkakati kuhakikisha

kwamba, tunapata wataalam ambao watakuwa katika hizo ofisi, ili kutoa huduma za ushauri nasaha au huduma zile za saikoloji, ili kuwasaidia watumishi wetu waweze kutoa huduma vizuri pindi wanapokutana na changamoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas Maganga, swali fupi la nyongeza.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, Wabunge wengi wanazo takwimu sahihi za watumishi na walimu wanaojitolea kwenye majimbo na halmashauri zetu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi kushirikiana na Wabunge, ili kupata takwimu sahihi za watumishi na walimu wanaojitolea kwenye majimbo yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu ya watu wanaojitolea kwa sasa ofisi haijapata takwimu kamili kwa sababu, kwanza watu wamekuwa wakiingiza watumishi kwa namna ambayo, kama nilivyosema kwamba, watu wanapojitolea wakati mwingine wanaingizwa kwa upendeleo na wengine wanaingia kwa kujuana. Serikali imeendelea kupanga mkakati kuhakikisha tuna mwongozo na mfumo ambao utakwenda kufuatilia kwa karibu wale vijana ambao wamepata nafasi ya kujitolea baada ya kutumia mwongozo huu ambao tumeutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watumishi watakapoingia kupitia mwongozo huu, Serikali itapata urahisi wa kupata *data* kamili ya vijana wa kujitolea, lakini pia, mwongozo ule unaeleza masharti na vigezo ambavyo vitatumika, ili watu hawa waweze kujitolea. Kwa hiyo, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tunauchukua, ili kuendelea kupata *data* kamili kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edibily Kinyoma.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwa na wimbi la vijana kufanya *interview* nyingi na

kwenye *aptitude test* wanapata asilimia za juu mpaka 90%, lakini wanakuwa hawapo *selected*. Je, Serikali haioni ipo haja ya kuweka *cutting point,* ili kuepuka vijana kufanya *interview* 10 hadi 20 na hawapati kazi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanapokwenda kwenye mitihani ile ya awali, yaani *aptitude test,* kwanza tunapata waombaji wengi sana ambao ajira ikitangazwa wanajitokeza kuomba ajira hizi. Kwa hiyo, wanapokwenda kwenye usaili wanafanya mtihani wa *written,* kwenye ule mtihani wa *written* kunakuwa na alama ambazo zinamfanya yule msailiwa aweze kufikia zile alama na waliofikia zile alama wanachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, wengi wanafaulu na kwa kuwa kiwango ambacho labda Serikali imepanga kwa muda huo ni watu 10,000 na wanaohitajika labda ni watu 5,000 kwa hiyo, *cutting point* ya alama zile zinazotakiwa lazima itapanda kulingana na wingi wa watu kufaulu kwenda kwenye mtihani wa *written*. Hii ni kwa sababu, tunazingatia Sheria ya *ILO* ambayo inatuelekeza kwamba, nafasi moja itashindaniwa na watu watatu.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, aulize swali lake.

Na.134

**Kuanzishwa kwa Eneo Maalum la Viwanda vya Mazao ya Misitu**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, kwa nini, Serikali isianzishe eneo mahsusi la viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao ya misitu litakalohudumia masoko mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa sekta ya mazao ya misitu katika kukuza uchumi wa nchi, kuongeza thamani ya mazao, kuchangia upatikanaji wa ajira, pamoja na kuchangia katika pato la Taifa. Mkoa wa Njombe, Serikali ina mkakati wa kuanzisha eneo maalum la kiuchumi litakalovutia uwekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu pamoja na mazao mengine ya kimkakati ikiwemo parachichi. Hatua mbalimbali tayari zimeanza kuchukuliwa, ikiwemo uchambuzi na utambuzi na upatikanaji wa maeneo ya ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani, Serikali kupitia *TISEZA* inaendelea kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa ya Tanzania Bara, katika kuhamaisha utengaji wa maeneo mahsusi kwa ajili ya kuanzisha kongani za viwanda, ikiwemo viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu siyo tu kwa Mkoa wa Njombe na hata Mikoa mingine kama Iringa, Katavi na Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu yaliyotolewa na Serikali kutambua umuhimu wa jambo hilo, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga maeneo ni jambo moja na kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanapata hivyo viwanda ni jambo la pili. Sasa Serikali haioni umuhimu, kwa sababu maeneo mengi yaliyotengwa wanajenga viwanda Dar es Salaam, Pwani na maeneo ya mijini. Serikali haioni umuhimu wa kutenga vivutio mahususi kwenye maeneo ya vijijini ambako kule ndiko kwenye ajira kubwa, katika muktadha wa *business as usual* ambayo Wizara hii ndiyo imejirasimu nao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kwanza kwa kuwatetea wananchi wa Njombe Mjini. Mheshimiwa Mwanyika, amekuwa akifuatilia sana suala la uwekezaji kwenye mazao ya misitu nasi kama Wizara tunamuahidi kumpa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba huko nyuma viwanda vingi vili-*concentrate* upande wa Pwani, Mikoa ya Pwani Dar es Salaam na Tanga, ndiyo maana katika mpango wa miaka mitano wa Serikali tumekuja na mkakati wa ku-*decentralize* viwanda vyetu kupeleka kila maeneo. Kwa kupitia hilo tumeanzisha mpango wa maeneo maalum ya uwekezaji na ndiyo maana upande wa Njombe tunaenda kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji wa misitu, upande wa Bunda tunaenda kuanzisha Bunda *SEZ* ambapo tunaenda kuanzisha maeneo maalum kwa ajili ya mazao ya *blue economy,* vilevile Kigoma upande wa michikichi na mihogo na hapa Dodoma tuna eneo maalum kwa ajili uchenjuaji wa madini ambayo ni adimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kupitia hii nina uhakika sasa, ile adha kwamba viwanda vyote vime-*concentrate* ukanda moja inaenda kwisha na ninaomba nimtoe mashaka Mbunge kwamba tunaenda kutekeleza hili katika Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nami nafasi ya swali la nyongeza. Serikali ilitoa maelekezo kwa Halmashauri zote kutenga maeneo ya kongani za viwanda. Sasa ni upi mpango wa Serikali kufanya uwekezaji katika maeneo ambayo yamekwishatengwa hasa ya usindikaji wa mazao ya kilimo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kutoka Mkoa wa Manyara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Rais na tunakumbuka wakati anazindua Bunge letu alitoa maelekezo kwa Wizara yetu tuhakikishe kwamba tunaanzisha kongani za viwanda kila wilaya. Katika bajeti ya mwaka huu ambayo ilipitishwa wiki iliyopita, tayari tumeweka mipango ya kuhakikisha kwamba tunaenda kuanzisha kongani za viwanda kila wilaya. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunasogeza huduma za uwekezaji karibu na wananchi hususani katika kusaidia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua Mkoa wa Manyara ni mojawapo ya maeneo ambayo kimsingi ni *potential* kwa ajili ya kilimo cha ngano na tayari tunayo kongani ya viwanda kubwa kule, ninaomba nimuahidi Mbunge kwamba vilevile Mkoa wa Manyara upo ndani ya mipango yetu ya kuanzisha kongani za viwanda na tutaviendeleza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni.

Na. 135

**Mpango wa Pamoja wa Mageuzi ya Sekta**

**MHE. HARAN N. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakuja na mpango wa pamoja ili kutoa suluhu ya mageuzi ya sekta binafsi katika kukuza uchumi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge kutoka Jimbo la Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imekamilisha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ambapo sekta binafsi inatarajiwa kuchangia takribani 70% ya ukuaji wa uchumi. Ili kufanikisha azma hiyo, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inaendelea kukamilisha Mpango wa Pili wa Maboresho ya Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI *II*). Pia, inaandaa sera mpya ya uwekezaji na mkakati wake wa utekelezaji, kwa lengo la kuhakikisha mazingira ya uwekezaji yanakuwa rafiki zaidi kwa wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kuandaa sera, sheria na mkakati wa kukuza sekta binafsi, pamoja na kuandaa mwongozo wa kupima utendaji wa sekta binafsi, mwongozo wa upimaji wa mchango wa sekta binafsi kwenye 70% ya uchumi na mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa takwimu za biashara na uwekezaji. Ofisi pia itaendelea kuimarisha majukwaa ya sekta binafsi kupitia Tanzania *Private Sector Foundation (TPSF),* Vitengo vya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ngazi za mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali inapanga kufungua *One Stop Facilitation Centres* katika kila Mkoa na Wilaya ili kurahisisha mazingira ya biashara na uwekezaji ngazi ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, Serikali inaichukulia sekta binafsi kama mshirika mkuu wa maendeleo ya Taifa na itaendelea kuweka mazingira rafiki, thabiti na yenye kutabirika ili

sekta hiyo ikue, izalishe zaidi, iongeze ajira, ipanue wigo wa kodi na hatimaye kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haran Sanga, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninashukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali, lakini ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa, uchumi jumuishi ni mfumo wa uchumi unaohakikisha kila mtu ananufaika na maendeleo ya kiuchumi. Je, wananchi wa Kigamboni wananufaika vipi na uchumi jumuishi kama Serikali haijaweka kwenye mpango ujenzi wa Barabara ya *BRT* kutoka Kongowe - Mji Mwema - Feri na barabara ya lami kutoka Feri kwenda Pemba Mnazi ili vijana wa bodaboda, vijana wa mamalishe, machinga wa Kivukoni pamoja na Pemba Mnazi, Wavuvi wa Gezaulole, Wakulima wa Mbogamboga Mtaa wa Sala na Kibada waweze kunufaika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ninataka kujua ni lini Serikali itaanza kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira bora ya biashara MKUMBI *II* kwa maana ya kutoa utitiri wa leseni za biashara kwa wafanyabiashara hususani wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge kutoka Jimbo la Kigamboni kwa maswali yake mazuri mawili, pia Mheshimiwa Haran ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na amekuwa akichangia sana suala la uwekezaji hususani Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, ni kweli Dira yetu ya 2050 na mpango wetu wa miaka mitano wa 2026 - 2030 umezingatia kwamba tunahitaji kuja na uchumi jumuishi. Katika hili ninatambua kwamba Kigamboni ni eneo ambalo ni *very potential* kwa uwekezaji na tuna wawekezaji wengi sana wameweka viwanda Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia hili sisi kama Serikali na ndiyo maana kwenye mpango wa miaka mitano tumwekea kipaumbele kuboresha mazingira rafiki hususani miundombinu ya barabara, vilevile *BRT* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapovutia wawekezaji katika maeneo yale, wawe tayari kwenda kwa ajili ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mbunge tumepokea hoja yake na sisi kama Serikali tutaiingiza kwenye mpango yetu tuhakikishe kwamba wale wawekezaji ambao wanataka kwenda kule waweze kwenda na tuweze kupata manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni kuhusu MKUMBI *II* ni kweli kama Serikali tayari tupo mbioni kukamilisha utengenezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini na tayari huu mpango ulishapitia katika uhakiki Mheshimiwa Rais kutoka Zanzibar alikuja kwa ajili ya mapitio na tunategemea mwezi ujao tutazindua huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwa kupitia huu mpango tunaenda kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hususani kupunguza utitiri wa kodi, tozo, lakini urasimu ambao unaendelea katika kukuza sekta binafsi. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ibrahim Shayo.

**MHE. IBRAHIM M. SHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa kuuliza swali dogo. Mheshimiwa Naibu Waziri, Moshi ulikuwa ni Mji mwenye viwanda vingi sana, lakini kwa sasa viwanda vyetu Moshi vimekufa na vilivyokuwa vimebinafsishwa waliobinafsisha wameingia mitini. Je, ni lini Serikali itahakikisha

kwamba tunakwenda kuanzisha viwanda vipya na kufufua vile ambavyo vimekufa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mbunge kutoka Moshi Mjini kwa maswali yake mazuri na nilifanya ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Moshi Mjini, mojawapo ya changamoto ambayo alii-*raise* Mheshimiwa Mbunge ni suala la viwanda ambavyo vilikuwepo kule ambavyo kimsingi havifanyi kazi, lakini vilevile mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tunakuja na viwanda vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Moshi ni mojawapo ya maeneo yetu ambayo tumeya-*target* kwa ajili ya kukuza viwanda hususani kwenye upande wa kilimo, vilevile kwenye viwanda mbalimbali vya *manufacturing.* Ninaomba nimhakikishie kwamba hoja yake tumeichukua na katika mipango yetu tutaipa kipaumbele. Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, aulize swali lake.

Na. 136

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* - Ilongero**

**MHE. YOHANA S. MSITA K.n.y. MHE. HAIDERALI H. GULAMALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi *VETA* Ilongero?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali Namba 136 la Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, Mbunge wa Ilongero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)* 65 katika Wilaya Sitini na Nne (64) na Mkoa mmoja (01) wa Songwe. Ujenzi huu unafanyika katika Wilaya au Mkoa ambao hauna Chuo cha *VETA* kabisa. Jimbo la Ilongero lipo katika Wilaya ya Singida ambapo tayari ina Chuo cha *VETA*. Hivyo, wananchi wa Jimbo la Ilongero wanahimizwa kutumia Chuo cha *VETA* Singida ambacho kina huduma za bweni kwa wanafunzi wanaotoka maeneo ya mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kupanua fursa za upatikanaji na elimu ujuzi kwa ngazi mbalimbali, Serikali inaendelea na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Amali katika Jimbo la Ilongero ambayo itatoa mafunzo ya vitendo na stadi zinazohitajika katika soko la ajira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yohana Msita.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. kwa kuwa Wilaya ya Manyoni ni miongoni mwa Wilaya kubwa sana hasa kwenye Mkoa wa Singida, ina zaidi ya 58%. Tunaishukuru sana Serikali kwa sababu imeshaanza ujenzi wa *VETA,* lakini ujenzi huu umekuwa ukisuasua. Je, ni lini Chuo cha *VETA* Wilaya ya Manyoni kitakamilika ili kiweze kuanza kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yohana Msita wa Jimbo la Itigi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa ujenzi wa *VETA* kwa ujumla umefikia 65% na Serikali kama ilivyoahidi kwamba itajenga vyuo hivi vya *VETA* nchini nzima kama ilivyoahidi, tunaahidi kwamba 35% iliyobaki ikifika mwezi Septemba mwaka 2026 itakuwa imemalizika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Wilayani Sikonge ulisainiwa Juni, 2023 na chuo kingekamilika Disemba, 2023, lakini kutokana na changamoto mbalimbali mpaka tunavyoongea hivi sasa hicho chuo bado hakijakamilika. Je, ni nini sasa tamko la Serikali kuona kwamba chuo hiki kinaenda kukamilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika majibu ya jumla kwamba Serikali iliahidi kujenga vyuo hivi nchi nzima kwa zile Wilaya ambazo hazina vyuo hivi. Tayari tulishapokea shilingi bilioni 82 kama 82% ya shilingi bilioni mia moja ambazo tumepewa, lakini pia tumeshapokea asilimia ya fedha zilizobakia na nimuahidi Mbunge kwamba fedha hizi tutaenda kuzigawa hivi karibuni na vyuo vyote hivi vitakamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Stella Ikupa.

Na. 137

**Manufaa ya Uwanja wa Taifa kwa Wananchi wa Temeke**

**MHE. STELLA I. ALEX K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, wananchi wa Temeke wananufaikaje na uwepo wa Uwanja wa Taifa uliopo Wilayani humo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Benjamin Mkapa una faida nyingi kwa wananchi wa Manispaa ya Temeke na Taifa kwa ujumla. Kiuchumi unachochea mzunguko wa fedha kwa wafanyabiashara wakati wa matukio makubwa, pia unavutia wawekezaji wa matangazo makubwa na ajira kwa wananchi. Kijamii, matukio makubwa ya kidini na matamasha makubwa ya sanaa na muziki yanawaleta Wanatemeke na Watanzania wote pamoja na hivyo kudumisha amani na mshikamano wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimichezo uwepo wa uwanja huu umeifanya Manispaa ya Temeke kuwa kitovu cha michezo ya kitaifa na kimataifa jambo linaloongeza heshima na utambulisho wa eneo hilo na kutoa hamasa kwa vijana kushiriki michezo. Hivyo, miundombinu hii ni muhimu katika kuchochea maendeleo kwa wananchi wa Temeke na Tanzania kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Mariam anaishukuru Serikali kwa kujengwa kwa Uwanja huu wa Mkapa ambao unabeba watu wengi kwenye mechi mbalimbali zikiwemo mechi za Simba na Yanga na hivyo kuingiza mapato makubwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kugawa sehemu ya mapato haya na kuyaelekeza kwenye huduma za jamii katika Jimbo la Temeke? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Uwanja wa Mkapa na Uhuru unafanyiwa huduma mbalimbali ikiwemo kutengeneza bustani pamoja na usafi, lakini pamoja na huduma nyingine. Nini mpango wa Serikali kuwapa kazi hizi vijana wa Temeke wakiwemo vijana wenye ulemavu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA, NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na nimshukuru Mheshimiwa Stella Ikupa, kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Temeke ambaye anafanya kazi kubwa kwa ajili ya kuwapigania wananchi wa Temeke na ninamwombea Mungu aendelee kumtia nguvu na amtie moyo kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wa Temeke wanapata kile ambacho walitarajia wakati wanamtuma kuwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu maswali haya mawili mazuri ya nyongeza la kwanza lilikuwa kuhusiana na mgao. Mara nyingi Serikali haiandai matukio yanayofanyika katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, yenyewe inatoa miundombinu hii kwa waandaaji ambao kwa mfano mechi za Simba na Yanga timu mwenyeji ndiyo ambayo inakuwa inakodishwa uwanja huu. Mapato yanayopatikana hugawanywa kwa utaratibu maalum ambao umekubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 18% ya mapato hayo inakwenda kwama kodi ya ongezeko la thamani, asilimia tatu inakwenda kwa BMT, asilimia Nne inakwenda kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, 15% inakwenda kama gharama za ukodishaji wa uwanja na asilimia Saba kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli ile na asilimia Sita inakwenda kwa Chama cha Soka cha Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wote hawa moja ya mambo wanayoyafanya ni kuhakikisha wanarudisha kwa ajili ya shughuli mbalimbali zinazofanyika Tanzania na hasa kwa Manispaa ya Temeke ambayo uwanja huu umewekwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachofanya kwa sasa ni kuhakikisha tunaendelea kuimarisha makusanyo haya ili kiwango ambacho kinagawiwa kwa wadau hawa ambao nao hurudisha kwa Manispaa ya Temeke na maeneo mengine mbalimbali kwa ajili ya huduma hasa za michezo kinaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasimamia utaratibu wa kuhakikisha tunaendelea kukusanya mapato haya ili yawe na manufaa na tija kubwa zaidi kama ambavyo imekuwa ikitokea kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwenye swali lake la pili, kuhusiana na huduma mbalimbali. Katika hili Serikali imetoa zabuni kwa makampuni ambayo yanatoa huduma mbalimbali zinazofanyika katika Uwanja wa Benjamini Mkapa wakati wa matukio yanayotokea pale. Tumetoa zabuni kwa makampuni ya ulinzi na makampuni ya usafi hali kadhalika. Kampuni za ulinzi tunao walinzi 25 pale, lakini tunao vijana 40 ambao wanafanya shughuli za usafi na wote hawa ni wakazi wa Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kuhusiana na kutenga kwa ajili ya watu wenye ulemavu moja kwa moja, hili ni wazo zuri na ninaomba nilichukue kwa ajili ya mashauriano na wenzangu kuona kama miongoni mwa vikundi vya wajasiriamali ambapo sasa hivi tunavyo vikundi vinne pale, kila kimoja kikiwa na wanachama 50, tuone kama tunaweza kutenga vikundi ambavyo vitakuwa vya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali panapokuwa na matukio kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Uwanja wa Nangwanda Sijaona uliopo Mkoani Mtwara ni miongoni mwa viwanja ambavyo vinaingiza mapato makubwa sana mechi inapofanyika: Je,

Serikali kwa kushirikiana na mmiliki wa uwanja huu ina mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa uwanja huu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na nimshukuru Mheshimiwa Chikota kwa swali zuri la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Nangwanda Sijaona haumilikiwi moja kwa moja na Serikali, ni uwanja wa miongoni mwa wadau wetu, Chama Cha Mapinduzi. Kama ambavyo nilishajibu mara kadhaa hapa, tunayo mazungumzo na Chama Cha Mapinduzi kuona namna ambavyo tunaweza kuhakikisha tunaweza kuvifanyia ukarabati kwa utaratibu unaofaa viwanja vingi ambavyo vinamilikiwa na taasisi hii na kuona namna ambavyo mapato yatafanyiwa mgawanyo baada ya uendeshaji kati ya Chama Cha Mapinduzi na Serikali ambayo itakuwa imefanya ukarabati wa viwanja hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Uwanja wa Nangwanda Sijaona ni miongoni mwa viwanja ambavyo vipo katika fikra zetu. Tutakapokubaliana na wamiliki wa kiwanja hiki ambao ni Chama Cha Mapinduzi tutakwenda kukifanyia ukarabati na kuhakikisha kinakuwa katika hali nzuri kwa ajili ya kufanya shughuli za michezo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto.

Na. 138

**Mnara wa Redio Tanzania – Kiteto**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza: -

Je, lini mnara wa Redio Tanzania uliojengwa Kiteto utaanza kufanya kazi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo hiki ni sehemu ya mradi unaotekelezwa na Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)*. Hadi kufikia tarehe 14 Aprili, 2026 ujenzi na ufungaji wa miundombinu ya mitambo ya redio katika kituo hiki umefikia 90% na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2026. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita,

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Niipongeze Serikali kwa majibu mazuri, mafupi, safi. Sasa swali dogo tu la nyongeza. Kwa siku ambazo si nyingi sana ni lini upo tayari ututembelee Kiteto ili kuweza ku-*monitor* mradi huu muhimu sana kwa wananchi wa Kiteto?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa zuri la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto na nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya kuwapigania Wanakiteto. Hili la kuambatana naye kwenda Kiteto wala siyo suala la mjadala, atakapokuwa tayari Mheshimiwa Mbunge anifahamishe tujadiliane kuhusiana na ratiba ya Bunge na shughuli nyingine za Serikali, tufunge safari kwa ajili ya kwenda Kiteto.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, aulize swali lake.

Na. 139

**Ujenzi wa Uzio Uwanja wa Ndege Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga uzio wa Uwanja wa Ndege Urambo ili kuutunza vema Uwanja huo na kuwa salama?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuimarisha ulinzi na usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Urambo na hivyo inakubaliana na pendekezo la ujenzi wa uzio katika kiwanja hicho. Katika hatua za utekelezaji, suala hili tayari limejumuishwa katika rasimu ya Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* wa miaka mitano ijayo, ili kuwezesha upangaji na upatikanaji wa rasilimali fedha kupitia bajeti ya maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ukarabati, uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia *TAA* inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa Kiwanja cha Ndege cha Urambo kinaendelea kuwa salama. Hatua hizo ni pamoja na utekelezaji wa maelekezo ya kitaifa kuhusu ulinzi na usalama wa viwanja vya ndege, pamoja na kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi wanaozunguka eneo la kiwanja kupitia dhana ya ulinzi shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kiwanja hicho kinamiliki hati ya ardhi, jambo linalosaidia kulinda mipaka yake dhidi ya uvamizi na matumizi yasiyoidhinishwa, hususan katika mazingira ambayo kiwango cha shughuli za kiuendeshaji bado ni cha chini. Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki kadri itakavyohitajika ili kuhakikisha usalama na maendeleo endelevu ya miundombinu hiyo muhimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yametupa matumaini sisi Wananchi wa Urambo. Ninaomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninatanguliza ombi maalum, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akijibu ameeleza wazi kabisa kwamba, Serikali inatambua kwamba ule uwanja ni muhimu na ni wa kihistoria na kwamba tayari wameshauweka katika mpango wa maendeleo, tunaishukuru sana Serikali kwa kutambua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa kwa niaba ya wananchi wa Urambo ujenzi wa uzio wa Uwanja wa Ndege wa Urambo uwekwe katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa uwanja wa ndege wa Urambo upo kati kati ya mji na kwa msingi huo unachangia mwonekano wa mji. Je, Serikali ipo tayari kuweka utaratibu maalum wa usafi wa uwanja na ulinzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Margaret Sitta kwa maswali yake mawili ya nyongeza ambayo kimsingi hoja yake ya kwanza ni ombi. Ninapenda kupokea kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kwamba ombi lake limepokelewa, tutalichakata. Na kwa kuwa tumelipa msukumo mkubwa ninaamini tutakuwa kwenye hatua nzuri ya kwenda kulifanyia kazi kama ambavyo tumesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jambo lake la pili, amesisitiza kuhusiana na mwonekano wa uwanja. Huu ni uwanja wa kihistoria kama nilivyosema na mama yetu Mama Sitta ni mmoja kati ya watu ambao wanapigania sana uwanja wa Urambo pamoja na uwanja wa Tabora na maendeleo ya jimbo lake kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe, tumeshaweka utaratibu hivi ninavyozungumza, pengine nitumie nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Uchukuzi kuwaelekeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kuweka mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba tunapata watoa huduma watakaoweza kuimarisha ulinzi na usalama na usafi katika eneo hili ili hoja ambayo anaipigania mara kwa mara iweze hatimaye kufuatiliwa.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya mifugo na Uvuvi, swali la Mheshimiwa John John Nchimbi, Mbunge wa Nyasa, litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo.

Na. 140

**Kupatiwa Mkopo wa Boti za Uvuvi Wilaya ya Nyasa**

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO K.n.y. MHE. JOHN J. NCHIMBI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa mikopo nafuu ya Boti za Uvuvi za *Fiber* kwa Wavuvi wa Wilaya ya Nyasa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa John John Nchimbi, Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutoa shilingi bilioni 200 kwa vijana ndani ya siku 100 baada ya kuingia madarakani kwa ajili ya kufanya biashara ndogo, za kati na kampuni changa. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Maendeleo ya

Vijana, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*TADB*) ilitoa tangazo tarehe 4 Machi, 2026 ili kuujulisha umma juu ya fursa ya mikopo nafuu kwa vijana ili kupata mitaji na kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mikopo hiyo inalenga kutoa vifaa na pembejeo muhimu za ufugaji samaki kwa vizimba, zana za uvuvi, ufugaji wa kuku, ufugaji wa nguruwe, ufugaji wa mbuzi na kondoo, miundombinu ya ubaridi, uchakataji wa dagaa pamoja na mwani katika maeno yote ya wavuvi hapa nchini; wakiwemo wavuvi wa Wilaya ya nyasa. Ninatoa rai kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kuwahamasisha vijana kujiunga kwenye vikundi na vyama vya ushirika ili waweze kunufaika na mikopo hii isiyokuwa na riba na yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa John John Nchimbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa nyingi kuwa vizimba vya samaki havijengeki Ziwa Nyasa. Swali la kwanza; je, Serikali ipo tayari kupeleka watafiti kwa ajili ya kuchunguza namna ya kufanya ili vizimba hivyo viweze kujengeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali ipo tayari kuwajengea uwezo vijana wa Wilaya ya Kyela wa kuwahusisha katika minyororo ya thamani ya uvuvi ili kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana katika eneo hilo, lakini pia kuwapa mikopo ya asilimia fulani ya kuweza kupata boti za *fibre*?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Timida Fyandomo kwa sababu tangu ameingia Bungeni hapa amekuwa akijitahidi sana

kuhakikisha kuwa hoja za vijana zinasikika na sisi Serikali tunazipokea na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza linahusiana na utafiti juu ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba ziwa Nyasa. Ninaomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba ufugaji wa vizimba kwetu sisi Wizara lengo letu ni kuhakikisha kwamba unafanyika katika maziwa yote makuu nchini, lakini na maziwa madogo. Kwa hiyo kwa yale maziwa ambayo bado tunayafanyia tafiti au bado tupo katika taratibu za kuyafanyia tafiti tunaendelea kuhakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha pia huko tunaweka ufugaji wa samaki kwa vizimba ikiwemo Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe wasiwasi, tayari tumeanza utaratibu wa kuhakikisha tunafanya tafiti za kutosha ili kuona namna gani tunaweza tukauanzisha ufugaji huu katika Ziwa letu Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili, amezungumzia suala la boti za *fibre* kwa vijana wa Wilaya ya Kyela Mkoani Mbeya. Ziwa Nyasa linanufaisha mikoa mikuu mitatu ya Ruvuma, Mbeya na Njombe. Ni kweli kwamba tunahitaji kuendelea kuwawezesha vijana wetu katika wilaya zetu zote za Mbeya na hasa zinazozunguka ziwa hili ili waweze kuingia katika sekta yetu ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara imetenga shilingi bilioni 9.5 kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi kwa kutoa boti hizi za kisasa. Tumetenga bajeti hii kwa ajili ya kununua boti 100 za kisasa na boti 76 shikizi. Nimtoe wasiwasi, kwamba katika wale wananchi 2,100 ambao tumelenga kuwanufaisha kwa fedha hii basi vijana wa Wilaya ya Kyela Mkoani Mbeya nao watanufaika. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Kwa ajili ya muda wa maswali kwa siku ya leo, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, aulize swali lake.

Na. 141

**Mradi wa Maji Makonde - Newala Vijijini**

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Makonde utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Makonde kupitia Mradi wa Maji wa Miji 28 kwa gharama ya shilingi bilioni 84.7. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu vitatu vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 26 kwa siku, ujenzi wa matanki manne yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 13, sanjari na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 40%, ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2026 na kunufaisha zaidi ya wananchi 600,000 waishio kwenye Wilaya za Newala, Tandahimba pamoja na Mji wa Nyanyamba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Esmail Nawanda

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mradi wa Makonde ni mradi mkubwa sana ambao Serikali imekubali yenyewe kwa kusema jumla ya watu

600,000 wanakwenda kunufaika katika Wilaya za Newala, Tandahimba pamoja na Mtwara. Hivi tunapozungumza mkandarasi hayupo *site*, na alishawasilisha *certificate* za madai ya jumla bilioni 11.2. Je, ni Serikali italipa fedha hizo ili mkandarasi aendelee na shughuli yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika mradi huo wa Makonde kuna miradi miwili pacha, Mradi wa Lukohe pamoja na Mradi wa Malatu, miradi hii yote kandarasi *CTC Construction Company* amefanya kazi na amewasilisha jumla ya *certificate* tatu zenye jumla ya shilingi 6,000,000,000 na hayupo *site*. Je, Serikali ina kauli gani ya kuhakikisha mkandarasi anarudi ili miradi hii iweze kukamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika jimbo la Newala Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kabisa, kwamba mradi huu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, ni mradi mkubwa na ni wa kimkakati. Asili yake ni mradi uliojengwa mwaka 1954, ambapo ukarabati wake ulianza mwaka 2022. Kuna zaidi ya matenki manne ambayo yatajengwa Newala Mjini, Newala Vijijini, Tandahimba pamoja na Nanyamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu tayari fedha ambazo mkandarasi ameshalipwa zaidi ya bilioni 20.7 ambapo mradi umefikia 40% kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu pia kwamba, mkandarasi anadai takribani bilioni 10.8 ambazo tayari zipo kwenye mchakato na zitakapokamilika mkandarasi atalipwa, ambaye ni *ECC*. Tunaamini kwamba mradi huu unatakiwa ukamilike na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mradi wa pili ambapo mkandarasi pia naye anadai; kama ambavyo nilijibu hapa kuwa uwepo wa madai ya wakandarasi ni ishara tosha kwamba Serikali ina dhamira ya kweli kuhakikisha kwamba inatatua changamoto za wananchi na ndiyo maana tumeamua kuwekeza miradi mingi ili kuhakikisha kwamba wananchi wanatatuliwa changamoto zao, wakiwemo wananchi wa Newala Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, hizi bilioni sita tutahakikisha kwamba mkandarasi analipwa ili arudi *site* na kuhakikisha kwamba anaendelea na mradi na kuukamilisha kwa wakati, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya kutoka Wizara ya Maji.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, aulize swali lake.

Na. 142

**Kurejesha Kiwanda cha Chai Lupembe**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarejesha Kiwanda cha Chai cha Wakulima wa Chai Lupembe (MUVYULU)?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba nijibu swali namba 142 kama lilivyoulizwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha Lupembe Tea Factory kilichopo wilaya ya Lupembe kilibinafsishwa mwaka 2004 kwa Kampuni ya *Dhow Mercantile Limited*. Ubinafsishaji huo uliipa

kampuni hiyo 70% ya hisa na 30% ya hisa kubaki kwa Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Chai (MUVYULU). Baada ya ubinafsishaji, kulizuka mgogoro kati ya pande hizo mbili; hivyo, uendeshaji wa kiwanda na umiliki wa kiwanda uliosababisha *DML* kufungua kesi mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye pande hizo mbili zilikubaliana ya kumaliza mgogoro huo nje ya Mahakama chini ya usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina; ambapo kikao cha mwisho kilifanyika tarehe 13 Machi, 2026. Maazimio ya kikao hicho yanaendelea kufanyiwa kazi, ambapo ikikamilika, zoezi la kurejesha kiwanda litafanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, wananchi wa Lupembe wanasubiri kwa hamu sana kiwanda hiki cha chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa Mahakama Kuu ilitoa amri kiwanda kirejeshwe kwa wananchi tangu mwaka 2022, lakini pia Mheshimiwa Rais kwa kuwapenda wananchi wa Lupembe na ili kuwapelekea tabasamu wananchi hawa alikwishaelekeza kiwanda hiki kirejeshwe kwa wananchi tangu 2022 akiwa pale Mtwango. Je, ni nani anayechelewesha huu mchakato mpaka leo kiwanda hakijarudi kwa wananchi wa Lupembe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wananchi wangu wa Tarafa ya Lupembe kwa maana ya Kata za Idamba, Filiga, Lupembe, Matengwe, Ukalawa pamoja na Kidegembye na Lupembe yenyewe wanalima sana chai kwenye mvua nyingi, wanakaa kwenye mabanda kwa muda mrefu, lakini bei ya chai ni 360 ambayo ni ndogo sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bei ya chai hadi shilingi 1,000 kwa kilo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mbunge Edwin Swalle kwa kupigania sana zao la chai humu Bungeni. Ninaomba nikubaliane naye kwamba kuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba, kiwanda hiki kinarudi kwa wakulima kwa ajili ya kuendelea na shughuli za uzalishaji ili kuongeza thamani ya zao la chai, zao ambalo ni la kimkakati kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIRDO* ambayo ni taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, ilishaanza zoezi hilo la tathmini mwaka 2024 ikikamilisha tathmini ya majengo na mitambo, changamoto ambayo walikumbana nayo ilikuwa ni kufanya tathmini ya ardhi. Chama cha Ushirika cha *MUVYULU* ilitakiwa kutoa hati hiyo ambayo kwa kuchelewesha kwao kulipelekea *TIRDO* kukwama na zoezi la kukamalisha zoezi la tathmini la kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kikao ambacho kilifanyika tarehe 13 Machi, 2026 chini wa Wizara ya Kilimo ambacho kilihusisha Ofisi ya Msajili wa Hazina, Wizara ya Viwanda na Biashara, Bodi ya Chai, Mamlaka ya Wilaya kule Njombe, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Chama cha Ushirika chenyewe pamoja na mwekezaji, walikubaliana kwamba Chama cha Ushirika kiwasilishe hati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafarijika kulitaarifu Bunge lako kwamba hati hiyo imeshawasilishwa tayari, wakati utawala wa mkoa na tayari ameshawasilisha kwa Bodi ya Chai. Hivyo, maelekezo yetu ni *TIRDO* kurudi kwa ajili ya kukamilisha tathmini hiyo ili Hazina wakamilishe malipo kwa mwekezaji, kiwanda hicho kirudi kwa wakulima na kuendelea na uzalishaji na ongezeko la thamani ya zao la chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, aulize swali lake.

Na. 143

**Ujenzi wa Barabara ya Lami Kasindaga – Runazi**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kasindaga – Kyebitembe – Karambi hadi Runazi kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kasindaga hadi Runazi yenye urefu wa kilometa 37.6 ni barabara ya mkoa, inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Kagera. Kwa sasa, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa hii barabara ambayo inahudumiwa na *TANROADS* kutokana na mvua zinazoendelea imeharibika sana kiasi kwamba haiwezi kuhudumia wananchi wa maeneo hayo; je, Serikali ina mkakati gani wa kuikarabati kwa kipindi hiki ili iendelee kutoa huduma kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; barabara hii inahudumia Tarafa ya Kimwani ambayo ina wakazi wengi wa Wilaya ya Muleba na ndiyo inabeba uchumi wa Wilaya ya Muleba. Je, Serikali haioni uharaka wa kutafuta hizo pesa

tukaifanyia upembuzi wa kina ili ikajengwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara nyingi ambazo ni za kiwango cha changarawe katika kipindi hiki cha mvua zimeharibika ikiwepo na hii barabara ambayo nimeisema. Hata hivyo, nimwelekeze tu Meneja wa Mkoa wa Kagera kwamba, waweze kufanya kinachowezekana pale ambapo panaweza pakafanyika, basi mkandarasi ambaye amepewa kazi ya kukarabati hiyo barabara aweze kuwepo kwenye hiyo barabara ili yale maeneo yote ambayo wananchi wanakwama aweze kuyarekebisha ili barabara iweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Kagera kwa maana ya Meneja wa Mkoa, wameshawasilisha maombi ya kuiweka barabara hii kwenye usanifu katika bajeti ambayo kama itapita, basi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hilo zoezi la kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, litakuwa ni kazi ambayo tutaifanya katika mwaka wa fedha ambao tutauanza Julai. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha kwa siku ya leo.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Nasimama kwa kanuni ya 76 kuomba mwongozo wako kwa jambo lililotokea mapema leo Bungeni wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, akijibu swali Na. 131 linalohusu

ujenzi wa soko Wilaya ya Mkalama ambapo ameliambia Bunge lako Tukufu kwamba, hivi sasa maafisa wako *site* kufanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mbunge, maafisa wangu wameenda kufuatilia baada ya kuwasiliana nao nikiwa hapa, wameenda kwenye Ofisi ya *DC*, wameenda kwenye Ofisi ya Mkurugenzi, wameenda kwenye Ofisi ya Mkuu wa Idara na Mipango. Taarifa iliyopo ni kwamba afisa wa mwisho alionekana tarehe 9 Septemba, 2024. Naomba mwongozo wako kwa sababu tunapokuwa hapa ndani Waheshimiwa Wabunge, tuna *access* na majimbo yetu, tunajua nini tunakifanya. Tunapopewa majibu ambayo hayaridhishi inatuumiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jesca Kishoa ameuliza mwongozo wake kwa kanuni ya 79 na swali alilouliza kwamba ni yeye ana swali la msingi na kwamba hajaridhika labda majibu ambayo ametoa Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa maana yeye anaona ni kinyume cha hivyo. Kwa hiyo, kwa mwongozo wangu na kwa uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge, tutarudi kwenye *Hansard* tuweze kuangalia jibu alilojibu na swali alilouliza na uhalisia uliopo kwenye *site,* baadaye tutatoa majibu kwa mwongozo huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijatangaza matangazo ya wageni waliopo, ninaomba tukumbushane kidogo tu kuhusiana na maswali.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni ya 54(4) tunaambiwa kwamba, Wabunge watakaouliza maswali ya nyongeza wasizidi watatu, labda Spika akiona vinginevyo. Kwa namna ambavyo tunapewa muda hapa wa maswali, swali moja tunatakiwa liishe kwa muda wa dakika sita. Kwa hiyo, siyo rahisi sana Wabunge watatu kuuliza swali la nyongeza ikiwa litakuwa refu.

Kwa hiyo, ninasisitiza maswali ya nyongeza yawe mafupi. Hata wale wenye maswali ya msingi, wanapokuwa wanajua wana swali la msingi, kwa utawala bora wa Shughuli za Bunge, ni vyema wasiulize maswali ya nyongeza. Tayari una swali la msingi, na wewe unataka tena swali la nyongeza, unawanyima fursa wenzako ambao wanataka kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa hiyo, ninaomba tuendelee kufuata taratibu za kanuni zetu na pia swali la nyongeza haliruhusiwi kusomwa kwa mujibu wa kanuni ya 54. Kwa hiyo, ninaomba nikumbushe tena Waheshimiwa Wabunge, tuwe makini katika kuuliza maswali mafupi ili tusiweze kuyasoma. Baada ya maelezo hayo mafupi naamini kabisa tutakwenda vizuri, taratibu tutaelewa na mambo yatakuwa mazuri.

Sasa, matangazo yaliyopo ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii:-

Kuna wageni ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, wageni wa Mheshimiwa Joel Arthur Nanauka, ambaye pia ni Waziri wetu wa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana ambao ni Ndugu Jenifa Omolo, Katibu Mkuu; Dkt. Kedmon Mapana, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Tully Mwambapa, Mkurugenzi Mtendaji *CRDB Bank Foundation;* na Dkt. Zuena Kilugwe, Mhadhiri Chuo Kikuu cha Mzumbe. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Gray Nanauka, Baba Mzazi wa Mheshimiwa Waziri. Karibu sana baba yetu katika Bunge letu na tunaye pia, Ndugu Angela Nanauka, Mama Mzazi wa Mheshimiwa Waziri. Karibu sana mama yetu. *(Makofi)*

Tunaye pia, Ndugu Rachel Kyomo, Mke wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Joyceline Nanauka, Mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Jackline Nanauka, Mdogo wake Mheshimiwa Waziri na Ndugu Esther Gawele, Dada wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana familia ya Mheshimiwa Waziri wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni 21 wa Mheshimiwa Paul Christian Makonda ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, hao ni

viongozi wa jamii ya Kabila la Kimaasai *(Malaigwanani)*. Karibuni sana *Malaigwanani* kutoka huko Arusha. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini, Ndugu Obed Laizer, mpigakura wake kutoka Jimbo la Longido Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Wageni wengine sita wa Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini kutoka Chama cha Mabroka wa Madini Tanzania (CHAMMATA). *(Makofi)*

Kuna Mgeni wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi Mbunge, ambaye ni Naibu Waziri, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Huyu ni Ndugu Dillip Kumarjain Mwekezaji kutoka Chunya Mkoani Mbeya; karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mkurugenzi Halmashauri Wilaya ya Urambo Mkoani Tabora, Ndugu Grace Quintine. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 29 wa Mheshimiwa Sitta wa Urambo *Jogging Club* kutoka Mkoani Tabora, wakiongozwa na Ndugu Ismail. Karibuni sana wageni wetu kutoka huko Tabora. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Makatibu wa CCM Kata za Wilaya ya Rorya, Mkoani Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni Maafisa 21 kutoka Taasisi ya Mwene Ngalu Kapufi Faundation, Mkoa wa Katavi na Rukwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 40 na Walimu 10 wa Shule ya Awali na Msingi Mirabelle’s ya Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu wa hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tuna pia Wanakwaya 32 wa Dayosisi ya Kaskazini Mashariki Ushirika wa Mombo Lushoto na Wanakwaya wa Kanisa la Kilutheri

Tanzania Dayosisi ya Dodoma. Karibuni sana Wanakwaya wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wapo pia Maspika na Manaibu Spika 54 kutoka Vyuo mbalimbali nchini Tanzania. Maspika na Naibu Spika wa vyuo hao, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna vilevile wanafunzi 40 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* cha Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka *CBE*. *(Makofi)*

Kuna tangazo lingine hapa linatoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa kuwa leo siku ya Jumatatu, tarehe 20 Aprili, 2026 kutakuwa na semina itakayotolewa na Wizara ya Nishati kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta na mikakati ya kupunguza athari nchini. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa saba kamili mchana mara baada ya kusitisha kikao cha Bunge. Waheshimiwa wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu sana. *(Makofi)*

Katibu tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Sasa ninamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana. Karibu sana Mheshimiwa Waziri wetu, Mheshimiwa Joel Arthur Nanauka, Waziri wa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa taarifa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais,

Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kuendelea kuitunuku nchi yetu amani, upendo na utulivu na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine katika Bunge la Kumi na Tatu, Mkutano wa Tatu wa Bunge la Bajeti, kujadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Mpango wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Hotuba hii ya Bajeti ikiwa ni mara yangu ya kwanza tangu kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuliongoza Taifa letu kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Aidha, nimpongeze kwa kuendelea kusimamia misingi ya Taifa letu na kuihakikishia jamii ya Kimataifa kuwa, Tanzania ina fursa za uhakika na ni mahali salama kwa uwekezaji katika Sekta mbalimbali ikiwemo viwanda, madini, maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa hizi zimejielekeza katika kuleta maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Sote ni mashahidi wa jinsi uongozi wake unavyogusa Watanzania katika kuwaletea maendeleo na kukuza ustawi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara wa kuanzisha Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana. Hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kutambua

nafasi na mchango mkubwa wa vijana katika kuleta maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru kwa kuniteua kuwa Waziri chini ya Ofisi yake na ninaahidi kuwa, dhamana aliyonipa nitaitekeleza kwa uaminifu, ufanisi na uadilifu mkubwa, ili kutimiza matarajio yake katika kutatua changamoto za vijana na kusimamia maendeleo yao kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini na ufuatiliaji anaoufanya katika kuhakikisha malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Wakati wote amekuwa mstari wa mbele katika kutoa miongozo mbalimbali ya kuhakikisha ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za kiuchumi zinazoleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha pili kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Aidha, ninampongeza kwa uongozi wake madhubuti na juhudi zake za kuendeleza ustawi wa vijana. Tunatambua na kuthamini mchango wake mkubwa katika kuimarisha fursa za ajira, kukuza ujasiriamali na kuboresha mazingira ya elimu na mafunzo kwa vijana. Maono yake yamekuwa chachu ya maendeleo na yanawapa matumaini vijana wengi kufikia ndoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, ninampongeza kwa kuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 - 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru kwa kuendelea kutuongoza vyema na kuweka dira katika utekelezaji wa majukumu ya kuendeleza vijana nchini. Ninapenda kukiri kuwa, kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimejifunza mengi sana kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali. Ninasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mussa Azzan Zungu, na Naibu Spika Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuchaguliwa kuliongoza na kulisimamia Bunge kwa hekima na umahiri mkubwa kwa kushirikiana na Wenyeviti wote wa Bunge. Aidha, ninapenda kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu mbalimbali yanayochochea maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia kwa namna wanavyoshirikiana nami katika utekelezaji wa majukumu ya kusimamia Sekta ya Maendeleo ya Vijana kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kuwa misingi kuhusu masuala ya vijana iliyowekwa kupitia iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) inaendelea kuwa chachu katika kuendeleza sekta ya maendeleo ya vijana nchini. Vilevile, ninawapongeza Wabunge wenzangu kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mbunge Viti

Maalum na Wajumbe wote wa Kamati kwa michango, ushauri na miongozo wanayoendelea kutupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, Kamati hii imekuwa msaada mkubwa sana kwangu ikizingatiwa kuwa Ofisi ni mpya na Waziri ni Mpya, hakika ninashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana itaendelea kushirikiana kwa karibu na Kamati hii kwa manufaa ya vijana na maslahi ya Taifa letu. Aidha, ninamshukuru Katibu wa Bunge ndugu Baraka Idelphonce Leonard kwa ushirikiano wake thabiti kupitia wasaidizi wake wanaosimamia Kamati mbalimbali. Ushirikiano huu umeimarisha utendaji wa Kamati na kuendeleza dhana ya uwajibikaji na uwazi katika shughuli za Bunge. Ni kwa mshikamano huu tunapata nguvu ya kusonga mbele na kutimiza matarajio ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuwashukuru kwa dhati Viongozi wenzangu na Watendaji wa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa ushirikiano, ubunifu, usimamizi na utekelezaji wa mikakati yake. Kipekee, ninapenda kumshukuru Bi. Jenifa Christian Omolo, Katibu Mkuu; na Dkt. Kedmon Elisha Mapana, Naibu Katibu Mkuu, kwa uchapakazi wao, umahiri na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli zangu za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru vilevile Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na Watumishi wote kwa ushirikiano wao na juhudi wanazozifanya katika kufanikisha malengo ya Wizara. Ninaliahidi Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na falsafa ya: "Kufanya Kazi kwa Kasi; Kufikika na Matumizi ya Teknolojia ili Kuwafikia Vijana Wengi Zaidi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwa kumpoteza Kiongozi wetu mpendwa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la

Isimani, Iringa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pole pia kwa kuondokewa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Peramiho, Ruvuma na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Kundi la Wafanyakazi. Kwa hakika tutaendelea kuwakumbuka na kuwaenzi kwa michango yao na mambo makubwa waliyofanya katika Sekta ya Maendeleo ya Vijana na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa pole kwa Watanzania waliokumbwa na kadhia mbalimbali kama vile ajali, moto na kadhia nyingine. Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema majeruhi wote na tunamwomba azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya utangulizi, ninaomba sasa nijielekeze katika maeneo mahususi ya hotuba hii ambayo ni: Hali halisi ya vijana nchini; Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Maendeleo ya vijana kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Fungu 104 - Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya vijana nchini. Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, zinaonesha kuwa Tanzania Bara ina jumla ya vijana 20,612,566 wenye umri wa miaka 15 hadi 35 ambao ni sawa na 34.4% ya idadi ya watu wote. Aidha, kwa mujibu wa Utafiti wa Nguvu Kazi wa Mwaka wa Fedha 2020/2021, vijana wanachangia zaidi ya 55% ya nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinaonesha wazi kuwa vijana ndiyo sehemu kubwa zaidi ya nguvu kazi inayoshiriki katika shughuli za kiuchumi nchini. Hivyo, maendeleo ya vijana yana uhusiano wa moja kwa moja na tija ya uzalishaji, ukuaji wa sekta mbalimbali za uchumi, pamoja na uwezo wa Taifa katika kuzalisha mali na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, pamoja na ukubwa wa nguvu kazi ya vijana iliyopo nchini, nguvu kazi hii imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ukosefu wa ajira ambapo kwa mujibu wa utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2021, vijana wameendelea kukabiliwa na ukosefu wa ajira kwa 12.2%; wanaume ikiwa ni asilimia 8.1 na wanawake 16.1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nguvu kazi iliyopo ina upungufu wa ujuzi wa mahitaji wa soko la ajira kwa kiwango cha chini cha 76.9% badala ya 54%; kiwango cha kati 19.9% badala ya 34% na kiwango cha juu ni asilimia 3.2 badala ya 12% kwa nchi zenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, changamoto nyingine ni pamoja na vijana kutokidhi vigezo vya mikopo vilivyowekwa na taasisi za kifedha, upatikanaji mdogo wa mitaji na fursa za biashara, matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana, upungufu wa malezi na mwongozo stahiki, athari za shinikizo rika pamoja na matumizi yasiyo sahihi ya mitandao ya kijamii na kuongezeka kwa tatizo la afya ya akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto za vijana, Serikali imefanya jitahada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutunga Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 Toleo la mwaka 2024 na kutekeleza Programu mbalimbali za uwezeshaji kwa vijana. Pamoja na jitihada hizo, changamoto za vijana zimeendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hivyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uamuzi wa makusudi wa kuanzisha wizara maalum kupitia Tangazo la Serikali Na. 685 na 686 linalotoa mgawanyo wa majukumu ya wizara ambayo majukumu yake ni kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera zinazohusu maendeleo ya vijana; uratibu wa maendeleo ya vijana, dhana ya kujitolea; uratibu wa elimu ya uraia kwa vijana, ustawi wa vijana, ushirikishwaji na uwezeshaji wa vijana kiuchumi; uratibu wa majukwaa ya vijana; kuboresha utendaji na

maendeleo ya rasilimali watu; na kusimamia Taasisi zilizo chini ya Ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ni ushahidi wa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kuhakikisha vijana wanakuwa mstari wa mbele katika safari ya kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya vijana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Katika kusimamia programu za uwezeshaji vijana kiuchumi, Wizara imetoa mikopo ya vifaa yenye thamani ya shilingi 824,463,770 kwa vijana 126 katika Mkoa wa Mwanza (39); Mtwara (40); Mbeya (22); Rukwa (10) na Arusha (15) kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuwawezesha kujiajiri na kuajiri wengine. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha mifumo ili kupunguza changamoto na vikwazo vilivyokuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, mikopo inatolewa kwa vikundi na kwa kijana mmoja mmoja; lakini pia, mikopo ina kipindi cha rehema (*grace period*) kuanzia miezi mitatu hadi miezi sita, isipokuwa kwa miradi maalum ya kilimo, uvuvi na ufugaji kipindi cha rehema ni miezi nane; riba imepunguzwa hadi asilimia tano kwa kipindi chote cha mkopo; lakini pia, imejikita kwenye uwezeshaji wa vifaa badala ya fedha pekee; na Wizara imeingia makubaliano na taasisi za kifedha kwa ajili ya kutoa mikopo na mafunzo kwa vijana ambapo, wanufaika hupatiwa mafunzo kabla ya mkopo na wakati wa uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya biashara ndogo, za kati na kampuni changa *(Start-Ups)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Februari, 2026, Ofisi ya Rais Maendeleo ya vijana ilikabidhiwa hundi yenye thamani ya shilingi bilioni 200 na kupewa jukumu la usimamizi na uratibu. Fedha hizo zinatolewa kupitia Sekta mbalimbali zikiwemo; Sekta ya Vijana,

Kilimo, Madini, Mifugo na Uvuvi, Viwanda na Biashara, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya kukabidhiwa jukumu la uratibu, kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Wizara yangu imeanzisha Programu ya Kitaifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi na kuandaa Mwongozo wa Utekelezaji wa programu hiyo. Mwongozo huo umejikita katika kuweka viwango vya ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa wakopaji na wakopeshaji wa fedha hizi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo pia umeainisha taratibu za utoaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo na sifa za wakopaji sambamba na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini. Utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya uwezeshaji wa vijana kiuchumi umeanza na hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya maombi 30,384 ya mikopo ya miradi ya vijana yamepokelewa na yanaendelea kufanyiwa uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya kuwezesha Vijana Kiuchumi, kiasi cha shilingi bilioni 48.6 kimetolewa kwa awamu ya kwanza katika sekta za uzalishaji na huduma ambazo ni; kilimo, mifugo na uvuvi, biashara na viwanda vidogo, sanaa na ubunifu, maendeleo ya jamii, pamoja na teknolojia na huduma za kidijiti. Uwekezaji katika sekta hizo umezingatia maeneo yenye fursa kubwa za ajira na uzalishaji mali, ambapo vijana wengi wanajishughulisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu itakapokamilika itanufaisha vijana takribani 10,000. Aidha, katika awamu ya pili ya utekelezaji wa programu hiyo, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana imepokea kiasi cha shilingi bilioni 2.5, ambacho kinatarajiwa kunufaisha vijana wapatao 888 kupitia miradi 36 katika Sekta za Viwanda, biashara ndogondogo, Kilimo, Uvuvi na mifugo ambapo ajira 4,440 zinatarajia kuzalishwa. Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa inawanufaisha makundi yote ya vijana kwa usawa bila kujali itikadi zao au maeneo yao ya kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana pia wamekuwa wakiwezeshwa kupitia asilimia nne ya makusanyo ya ndani ya Halmashauri ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, vikundi 5,199 vya vijana vilinufaika na mikopo yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 52.168. Kupitia mikopo hii, vijana wameweza kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi, kukuza biashara, kuongeza ajira na kuinua hali za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kwa kuendelea kuratibu na kusimamia utengaji wa fedha zitokanazo na mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuwawezesha vijana kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kukuza ujuzi kwa vijana. Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano pamoja na Wizara ya elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* katika kukabiliana na changamoto ya ajira kwa vijana kupitia Programu ya kukuza ujuzi, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi yametolewa kwa vijana 5,746 katika Vyuo na Taasisi za mafunzo 46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa njia ya utarajali kwa vijana 2,500 na mafunzo maalum ya kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi kwa vijana 7,826 vile vile yametolewa. Pia, wizara itaendelea kushirikiana na Wizara nyingine za Kisekta zinazotekeleza programu za kukuza ujuzi kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana inasimamia vituo vitatu vya Maendeleo ya Vijana vya Sasanda (Songwe), Marangu (Kilimanjaro) na Ilonga (Morogoro) vyenye lengo la kuimarisha utoaji wa mafunzo ya muda mfupi ili kuwapatia vijana ujuzi katika eneo la Kilimo, TEHAMA na Ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, vituo hivyo vilisitisha kutoa huduma kutokana na uhaba wa wakufunzi na uchakavu

wa miundombinu (majengo na madarasa). Kutokana na hali hiyo, Wizara imefanya tathmini ya uchakavu wa miundombinu katika Vituo vya Sasanda (Songwe) na Ilonga (Morogoro) kwa lengo la kufanya ukarabati kwa awamu ili vianze kutoa huduma. Baada ya kukarabatiwa, vituo hivyo vinatarajiwa kuwa na uwezo wa kudahili jumla ya vijana 300 kila robo mwaka kwa kila kituo, sawa na vijana 1,200 kwa mwaka kwa kila kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la utoaji elimu na fursa kiuchumi. Kupitia makongamano, warsha na majukwaa ya vijana, Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana imetoa elimu kwa vijana 15,753 kuhusu elimu ya afya ya akili; ujasiriamali; uongozi wa biashara; utunzaji wa hesabu na elimu ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vijana hao pia walipata elimu kuhusu fursa zilizopo katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Vilevile vijana walipata elimu kutoka *PPRA* kuhusu takwa la Sheria ya Ununuzi wa Umma inayoelekeza kutengwa kwa 30% ya zabuni za Umma kwa ajili ya makundi maalum ambapo kati ya hizo 10% ni kwa ajili ya vijana. Kupitia elimu hiyo, vijana waliweza kujisajili katika mfumo wa Kielektroniki wa Manunuzi ya Serikali *(NeST)* ambapo vikundi 299 vya vijana vyenye jumla ya vijana 2,226 vimenufaika kwa kupata zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 13.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kuimarisha ushirikishaji wa vijana na kusikiliza maoni yao. Baada ya kuundwa kwa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya vijana, kulikuwa na dhamira ya kufahamu kwa kina mahitaji ya vijana, mawazo yao pamoja na mitazamo yao kuhusu masuala mbalimbali yanayogusa maisha yao ya kila siku. Hivyo, Wizara iliandaa ziara za kukutana na vijana kwa lengo la kutoa jukwaa la wazi la kusikiliza sauti zao, kuelewa changamoto wanazokumbana nazo, lakini pia kupokea mapendekezo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizo zimewezesha Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kuelewa changamoto za vijana. Hivyo, kuwa katika nafasi ya kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati inayolenga kuboresha elimu ya uraia, kukuza uzalendo

na kuwajengea vijana mazingira bora ya kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na dhamira hiyo, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana ilifanya ziara maalum katika Mikoa sita ya Songwe, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Dar es Salaam na Dodoma, ambapo jumla ya vijana 8,120 walitembelewa katika maeneo 18 wanayofanyia kazi. Katika majadiliano hayo, hoja 186 ziliibuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa hoja hizo ulibaini kuwa hoja zilizoongoza kuchangiwa na vijana wengi ilikuwa ni: Ukosefu wa ajira (13.47%); maslahi duni ya vibarua wanavyofanya (9.68%); miundombinu ya kufanyia biashara kutokuwa rafiki (9.68%); changamoto za usafiri na usafirishaji (9.82%); upatikanaji wa mikopo ya asilimia nne mapato ya ndani ya Halmashauri (10.52%); ukosefu wa mitaji (10.53%); vigezo vigumu vya mikopo ya elimu ya juu asilimia 6.99; hofu ya kutoa maoni asilimia 6.45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine zilizoibuliwa zilikuwa ni mfumo wa elimu usioendana na soko la ajira asilimia 5.91; utitiri wa kodi na ushuru asilimia 5.03; kutokuwa na elimu ya ujasiriamali asilimia 4.84; urasimu wa kupata leseni na vibali asilimia 4.23; na kukosekana kwa Baraza la Vijana la Taifa asilimia 3.23. Takwimu hizo zinaonesha kuwepo kwa uelewa na mwamko wa vijana katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisera. Aidha, zoezi hili limekuwa chachu ya uwajibikaji, ushiriki wa vijana katika maendeleo na kujiamini katika kutoa maoni. Wizara itaendelea kupokea maoni na mapendekezo ya vijana na kutafutia ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kukuza majadiliano ya kitaifa. Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana iliratibu kongamano lililowakutanisha zaidi ya washiriki 1,200 Jijini Dar es Salaam tarehe 8 Januari, 2026 ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kongamano hilo pia lilihudhuriwa na Wizara za Kisekta zikiwemo: Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara ya Viwanda na Biashara; na Wizara ya

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Lengo la kongamano hilo lilikuwa kuwaweka vijana pamoja na kusikiliza maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kongamano hilo, vijana walipata fursa ya kuwasilisha changamoto zinazowakabili zikiwa ni pamoja na kukosa vitambulisho vya wajasiriamali, utitiri wa kodi, kukosa maeneo ya kufanyia kazi, kutotambuliwa, kukosekana mifumo rafiki ya usajili na gharama za leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta inaendelea kutafutia ufumbuzi changamoto hizo. Hatua hii imeendelea kuwaunganisha vijana na Serikali na kuwafanya kuwa sehemu ya kutafuta majawabu ya changamoto zinazowakabili, kuimarisha mawasiliano na kuhamasisha uzalendo kwa kuwajengea vijana hisia za kuthaminiwa na kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kuongeza ushiriki na ushirikishwaji, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana ilizindua Majukwaa ya Vijana yanayojulikana kwa jina la Vijana *Platforms* katika Mikoa sita ambayo ni Dar es Salaam, Singida, Mwanza, Shinyanga, Mtwara na Tabora. Kupitia majukwaa hayo jumla ya vijana 7,500 walihudhuria na zaidi ya washiriki 20,000,000 walifuatilia kupitia mitandao ya kijamii *(Instagram, Facebook, YouTube na TikTok)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzinduzi wa majukwaa hayo ulikuwa mubashara kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Lengo la majukwaa haya ni kukutanisha vijana wa makundi mbalimbali, ili kwa pamoja waweze kujadili kwa kina masuala yanayohusu maendeleo ya vijana katika ngazi mbalimbali za vijiji na mijini, lakini pia kutoa mapendekezo ya namna bora ya ushiriki katika ujenzi wa Taifa. Mapendekezo hayo yatatumika kama dira na mwelekeo wakati wa uandaaji wa Mipango, Sera na Maamuzi ya Serikali yanayohusu masuala ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uzinduzi huo, Wizara pia ilizindua namba maalum za huduma kwa wateja (*Call Centre)*. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya vijana 1,641, wanawake wakiwa 519 na wanaume 1,122 wamewasilisha changamoto na

mapendekezo kuhusu masuala ya vijana ikiwemo fursa za mikopo. Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana imeyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu vigezo na utaratibu wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uratibu wa masuala ya vijana. Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana iliratibu kikao kazi cha Maafisa Maendeleo ya Vijana wa Mikoa na Halmashauri kilichofanyika tarehe 17-18 Disemba, 2025 hapa Mkoani Dodoma. Kikao hicho kililenga kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na utekelezaji wa programu za vijana kuanzia ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mikoa hadi Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inaandaa mfumo wa uratibu wa masuala ya vijana nchini na Kanzidata ya Kitaifa itakayokusanya taarifa za masuala ya vijana. Lengo la kuandaliwa kwa mfumo huo ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa afua na ushiriki wa vijana katika shughuli za maendeleo ya vijana na kuwezesha wadau kutoka katika sekta ya umma na binafsi kutekeleza programu za uwezeshaji vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inasimamia Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, Sura ya 441 ambayo inatoa utaratibu wa uanzishwaji wa mabaraza ya vijana nchini. Hata hivyo, kutokana na mahitaji ya sasa ya vijana, Serikali imeanza mapitio ya Sheria hiyo ili kukidhi mahitaji hayo sambamba na kuhakikisha vijana wanapata nafasi pana ya kushiriki katika kupanga na kuamua mustakabali wa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya maboresho hayo Wizara imefanya ziara ya mafunzo kwa kutembelea Zanzibar na nchi ya Namibia kwa lengo la kujifunza juu ya uendeshaji wa Mabaraza hayo hususan Muundo wa Baraza la Vijana na masuala ya fedha na miradi inayotekelezwa na Baraza la Vijana. Kwa sasa Wizara inaendelea kukusanya maoni kwa wadau wengine ikiwemo vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kuimarisha ustawi na makuzi kwa vijana, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Stadi za Maisha

unaolenga kuwajengea vijana uwezo wa kujitambua, uwezo wa kuhimili changamoto za maisha, kufanya maamuzi sahihi na kuwasiliana kwa ufanisi. Kupitia mwongozo huu, Serikali inalenga kujenga kizazi chenye afya njema ya akili, chenye kujiamini na uwezo wa kujitegemea katika kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji, Zanzibar imeratibu uzinduzi wa mbio za Mwenge wa Uhuru uliofanyika tarehe 2 Aprili, 2026 katika Uwanja wa Mpira Gombani, Mkoa wa Kusini Pemba. Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenge wa Uhuru utakimbizwa katika mikoa 31 na halmashauri 195 za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru, miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo zinatarajiwa kukaguliwa na kuzinduliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujumbe wa mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2026 unalenga katika ujenzi wa Amani, Umoja na Mshikamano wa Kitaifa chini ya kauli mbiu inayosema: "Tanzania ni yetu Sote, Tushikamane kwa pamoja kuleta Maendeleo." Kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru wananchi wanaendelea kuhamasishwa kushiriki mapambano dhidi ya dawa za kulevya, malaria, UKIMWI, rushwa na kuzingatia lishe bora kwa afya imara. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Mwongozo wa Mbio za Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2002, Toleo la Mwaka 2026 ambao ulizinduliwa siku ya Uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto na mikakati ya utekelezaji ya kukabiliana nayo. Kwa kuwa, Wizara hii ni mpya, imeanza kutekeleza majukumu yake katika mazingira ya kuanzisha mifumo na kujenga misingi imara ya maendeleo ya vijana ndani ya Taifa letu. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo:-

(i) Ongezeko la uhitaji wa mikopo ukilinganisha na kiasi cha fedha kinachotengwa;

(ii) Baadhi ya vijana kukosa ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira;

(iii) Uelewa mdogo wa masuala ya stadi za maisha, elimu ya uraia, uzalendo, afya ya uzazi, athari za matumizi ya dawa za kulevya na matatizo ya afya ya akili; na

(iv) Miradi ya vijana kutokuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hizo Wizara imejipanga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

(i) Kuendelea kushirikisha wadau wa maendeleo ili kuchangia bajeti za programu mbalimbali za vijana;

(ii) Kuendelea kutoa elimu kuhusu mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya vijana kwa kushirikiana na Taasisi za Kifedha;

(iii) Kuendelea kutoa elimu kuhusiana na stadi za maisha, elimu ya uraia na uzalendo ili kujenga kizazi cha vijana kinachojua haki na wajibu wao, kinachopenda nchi yao na kinachoshiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa;

(iv) Kuendelea kutoa ujuzi kwa vijana kupitia vituo vya maendeleo ya vijana ili vijana waweze kupata mafunzo ya muda mfupi kuhusu kilimo, ujasiriamali, ujasiri pamoja na TEHAMA;

(v) Kuendelea kutoa elimu na kujenga uwezo kupitia Mwongozo wa Kitaifa wa mafunzo ya Stadi za Maisha na Mwongozo wa Uratibu wa Programu ya Stadi za Maisha kwa Vijana;

(vi) Kuendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta katika kukabiliana na changamoto za ajira ikiwemo: kukuza

ujuzi kwa njia ya Uanagenzi; kurasimisha ujuzi uliopatikana katika mfumo usio rasmi wa mafunzo (*Recognition for Prior Leaning Skills*); kupata mafunzo ya Uzoefu wa Kazi *(Internship skills);* na Mafunzo ya kukuza ujuzi kwa walio makazini *(Upskilling skills),* kupitia programu ya kukuza ujuzi inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano. Program zingine ni pamoja na Jenga Kesho iliyobora (*Build Better Tomorrow)* inayosimamiwa na Wizara ya Kilimo na Programu ya *Mining for a Brighter Tomorrow* inayosimamiwa na Wizara ya Madini;

(vii) Uchambuzi wa fursa (opportunity mapping) utafanyika kwa lengo la kubaini na kutambua fursa zilizopo katika maeneo mbalimbali, pamoja na kukusanya taarifa muhimu zitakazowezesha kuwashirikisha vijana kuhusu fursa hizo. Hatua hii italenga kuhakikisha vijana wanapata uelewa sahihi wa rasilimali na nafasi zilizopo katika mazingira yao, ili waweze kuzitumia kikamilifu kwa maendeleo yao binafsi na ya jamii kwa ujumla. Hii ni pamoja na fursa zilizopo katika Wizara za kisekta; na

(viii) Kuandaliwa kwa Mfumo wa uratibu wa masuala ya vijana utakaowezesha kukusanya, kuhakiki na kuhifadhi taarifa sahihi kuhusu vijana ili kuwa na Kanzidata itakayojumuisha mahitaji, sifa, ujuzi na maeneo ya kipaumbele. Mfumo huu utatumika katika uombaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Taarifa hizi zitatumika kuwezesha utambuzi wa uwezo na changamoto zao kwa ufanisi zaidi, pamoja na kurahisisha mchakato wa kuwaunganisha na fursa mbalimbali za ajira, mafunzo, ubunifu na uwezeshaji, kulingana na vigezo vinavyolingana na wasifu wao. Hatua hii itachangia kuongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za maendeleo na kuinua ustawi wao kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) kwa Mwaka wa Fedha

2026/2027 yameandaliwa kwa kuzingatia Miongozo mbalimbali ikiwemo:-

(i) Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/2027- 2028/2029;

(ii) Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050;

(iii) Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031;

(iv) Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya 2007 Toleo la mwaka 2024;

(v) Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025-2030;

(vi) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439;

(vii) Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana wa Miaka Mitano 2026-2030; na

(viii) Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 *(Sustainable Development Goals – SDGs, 2030)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu pia umezingatia: Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne 2023-2030; Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134; Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa wakati akihutubia Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025; na Maelekezo mengine ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya mpango; katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mpango wa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana utatekelezwa kupitia vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Kuimarisha ukuzaji wa biashara na uwezeshaji wa vijana kiuchumi kwa lengo la kuwezesha vijana wengi

kujiajiri na kuajiriwa katika sekta za biashara na uzalishaji;

(ii) Kuimarisha uratibu na ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa;

(iii) Kuimarisha uratibu wa elimu ya uraia, uzalendo na uratibu wa Mwenge wa Uhuru; na

(iv) Kuimarisha ustawi na makuzi kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zitakazotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 zitatokana na vipaumbele vilivyoainishwa katika Ibara ya 39. Kwanza ni kuimarisha uratibu na ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuimarisha uratibu na ushirikishwaji wa vijana kwa kuandaa Mfumo wa Taifa wa uratibu wa masuala ya maendeleo ya vijana nchini; kuandaa Kanzidata ya Kitaifa itakayokusanya taarifa za masuala ya vijana; kufanya mapitio ya Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa Sura ya 441; kuandaa mkakati wa Kitaifa wa vijana, amani na usalama na kuwezesha vijana kushiriki katika majukwaa na programu mbalimbali za Kikanda, Maziwa Makuu na Kimataifa, kuhusu amani na usalama; lakini pia kukusanya maoni na mrejesho kwa masuala ya vijana nchini kupitia dawati la huduma kwa wateja la Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007, Toleo la Mwaka 2024 yenye malengo ya kuimarisha maendeleo ya kiuchumi kwa vijana, kukuza ajira na ujasiriamali; kuendeleza stadi za maisha na ujuzi kwa vijana; kuimarisha ushiriki wa vijana katika maamuzi na uongozi; kulinda na kuendeleza haki na ustawi wa vijana; kuimarisha huduma za afya na ustawi wa vijana; na kukuza maadili, uzalendo na uwajibikaji kwa vijana;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha vilevile upatikanaji wa matumizi ya TEHAMA kwa vijana; kukuza vipawa, ubunifu na

michezo; kuimarisha ujumuishwaji wa vijana wote wakiwemo vijana, wanawake na watu wenye ulemavu; kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya maendeleo ya vijana; kuendeleza tafiti, takwimu na mifumo ya taarifa za vijana; pamoja na kuimarisha ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika masuala ya maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kuimarisha uratibu wa elimu ya uraia, uzalendo na Mwenge wa Uhuru, Wizara itaendelea kuratibu majukwaa ya vijana katika mikoa na halmashauri nchini; kuratibu utoaji wa elimu ya uraia na uzalendo katika halmashauri 184; kuratibu mbio za Mwenge wa Uhuru na wiki ya vijana ya kitaifa; na kuratibu maadhimisho ya siku ya wanaojitolea Kimataifa siku ya vijana Afrika pamoja na Siku ya Vijana Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ustawi na makuzi kwa vijana, Wizara itaendelea kuandaa na kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa mafunzo ya Stadi za Maisha; kuandaa programu ya Kitaifa ya kushughulikia masuala ya ustawi wa vijana; kuandaa Mwongozo wa Msaada wa Kisaikolojia kwa Vijana; na kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ukuzaji wa biashara na uwezeshaji wa vijana kiuchumi, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu ujasiriamali na ujuzi wa usimamizi wa biashara kwa vikundi vya vijana nchini; kutoa mikopo nafuu kwa vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine; kukarabati vituo vitatu vya mafunzo kwa vijana vya Sasanda, Ilonga na Marangu ili viweze kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za kilimo biashara, TEHAMA na ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itafanya utafiti wa uanzishwaji wa vituo vya ubunifu vya Kitaifa kwa vijana pamoja na kuanzisha vituo vya ubunifu kwa vijana *(VIJANA Hub)* vitakavyolenga kukuza ubunifu, kuendeleza vipaji, kutoa huduma za uratibu wa mawazo ya biashara, pamoja na kuwaunganisha

vijana na fursa za masoko, teknolojia na mitaji kwa ajili ya kuongeza ushindani na tija katika shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine ni kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa fursa za uwezeshaji kiuchumi ndani na nje ya nchi; kufanya mapitio ya mwongozo wa utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana wa mwaka 2022; na kuandaa mfumo wa kielektroniki wa uwezeshaji wa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia itafanya utafiti wa uanzishwaji wa Benki ya Vijana kwa lengo la kuchambua kwa kina ili kuwa na taasisi maalum ya kifedha itakayojikita katika mahitaji ya vijana. Dhamira ya Serikali ni kuweka msingi wa mfumo wa kifedha unaoendana na mazingira na uwezo wa vijana wengi, hususan wale wanaoanza shughuli za kiuchumi, ili kuondoa vikwazo vilivyopo katika upatikanaji wa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Vijana, itakayoanzishwa, itakuwa chombo muhimu cha kimkakati kitakachowezesha upatikanaji wa huduma za kifedha zilizo rafiki kwa vijana, kuchochea ubunifu wa bidhaa za kifedha zinazolingana na mahitaji yao, lakini pia kupanua wigo wa uwekezaji kwa vijana, na hatimaye kuongeza ajira na mchango wa vijana katika kukuza uchumi shindani na jumuishi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 35,957,298,000 kwa mchanganuo ufuatao: kiasi cha shilingi 30,104,264,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya kiasi hicho shilingi 1,227,961,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 28,876,303,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Pili, kiasi cha shilingi 5,853,034,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,000,000,000 ni fedha za ndani za maendeleo na shilingi 853,034,000 ni fedha za nje za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika

kuiwezesha Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/2026 yametokana na ushirikiano wa Wizara za kisekta, wadau wa maendeleo, mashirika mahsusi yanayojishughulisha na masuala ya vijana, taasisi za fedha, vyombo vya habari, taasisi zisizo za Kiserikali, taasisi za kidini, waandishi wa habari, vijana na wananchi kwa ujumla. Vijana Tuyajenge Tanzania ni Yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninasimama mbele yenu nikiwa na heshima kubwa na moyo wa shukrani. Safari yangu ya kufika hapa isingewezekana bila msaada wa familia yangu, ambao wamekuwa nguzo na faraja yangu wakati wa changamoto na chanzo cha matumaini yangu kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru wazazi wangu Bwana Gray Nanauka na Bibi Angela Nanauka kwa malezi na maadili waliyoniwekea ambayo yameniongoza hadi kufika hatua hii. Sambamba nao, ninawashukuru ndugu zangu wote kwa kunitia moyo na kunikumbusha thamani ya mshikamano wa kifamilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, ninamshukuru mke wangu kipenzi Rachel Nanauka na watoto wangu wapendwa Joyous, Joyceline na Jonel kwa uvumilivu na upendo wao usio na kifani. Hakika familia yangu imekuwa taa na mwanga wangu na leo ninapopokea heshima ya kuzungumza mbele ya Bunge hili Tukufu, ninaitambua na kuishukuru kwa dhati. Hii siyo tu heshima yangu, bali ni heshima yao pia. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo uliojaa furaha na matumaini ninapenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini kwa kuniamini na kunichagua ili kushirikiana nao katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu. Ushirikiano wao na maoni yao, ndivyo vilivyowezesha mafanikio tuliyonayo leo. Imekuwa miezi sita ya utendaji ulioacha alama kubwa kwa Jimbo la Mtwara Mjini na kwa unyenyekevu mkubwa ninawaahidi sitawaangusha. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa Mbunge na Waziri kwa mara ya kwanza, ninajifunza kila siku na nitaendelea kujifunza ili

kuhakikisha ninawatumikia wananchi wa jimbo langu na vijana kwa ufanisi mkubwa. Niko tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge, viongozi wenzangu, Watendaji wa Serikali na wadau wote wa maendeleo, ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba waendelee kuniombea, kunishauri na kunipa ushirikiano wenu wa dhati kwa pamoja tunaweza kuleta mabadiliko chanya na kujenga mustakabali bora kwa vijana wa Taifa letu. Tanzania ni yetu sote, tushikamane kwa pamoja kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha ninapenda kukumbusha mambo makubwa mawili; mosi, dhamira ya Serikali kupitia Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kuwapa vijana nafasi muhimu kwenye kuweka mipango, kushiriki kuweka vipaumbele na kuwa sehemu muhimu ya utekelezaji wa mipango ya Serikali. Wizara yetu itaendelea kuwaweka vijana katikati ya shughuli zetu za kila siku na katika kufanya hivyo, kama tulivyoanza, tutaendelea kuhakikisha vijana wote wanapata nafasi bila kubaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawashirikisha wa mjini na vijijini, wenye elimu na wasio na elimu, vijana kutoka vyama vyote vya siasa na hakuna kijana atakayebaguliwa katika kufaidika na fursa. Hii ni Wizara ya Vijana wote na wote watanufaika kwa haki na usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wakati maeneo mengine wanatafsiri vijana kama tatizo, Serikali ya Awamu ya Sita, kupitia Wizara ya Maendeleo ya Vijana, inawaona vijana kama ni mtaji mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwetu sisi vijana sio *liability* ila ni *asset,* kwetu sisi vijana wa nchi hii ni mtaji mkubwa katika kufanikisha maendeleo ya nchi yetu na utekelezaji wa Dira 2050, ili Taifa letu liendelee tunahitaji ubunifu wa vijana, mawazo ya vijana na nguvu ya vijana. Sawasawa na maono ya Mheshimiwa Rais, mikakati ya Wizara ni kuwafanya vijana wa nchi hii wasiwe watazamaji bali washiriki na wamiliki wa uchumi wa Taifa letu, tutawasikiliza na kuwashirikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha bajeti ya shilingi 35,957,298,000 ikijumuisha shilingi 30,104,264,000 za Matumizi ya kawaida na shilingi 5,853,034,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hotuba yangu hii, pamoja na kitabu cha hotuba tulichowasilisha na randama tulizowasilisha ziingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu. Aidha, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara, yani www.vijana.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA JOEL ARTHUR NANAUKA (MB.), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA, AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA KWA MWAKA 2026/2027 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka 2025/26. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka 2026/27.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kuendelea kuitunuku nchi yetu amani, upendo na utulivu na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine katika mkutano wa 13 wa Bunge la Bajeti, kujadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2025/26 pamoja na Mpango na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2026/27. Vilevile, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Hotuba hii ya

Bajeti ikiwa ni mara yangu ya kwanza tangu kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana.

**3.** **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuliongoza Taifa letu kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Aidha, nimpongeze kwa kuendelea kusimamia misingi ya Taifa letu na kuihakikishia jamii ya Kimataifa kuwa, Tanzania ina fursa za uhakika na ni mahali salama kwa uwekezaji katika Sekta mbalimbali ikiwemo viwanda, madini, maliasili na utalii. Fursa hizi zimejielekeza katika kuleta maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Sote ni mashahidi wa jinsi uongozi wake unavyogusa Watanzania katika kuwaletea maendeleo na kukuza ustawi wao.

**4.** **Mheshimiwa Spika**, kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara wa kuanzisha Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana. Hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kutambua nafasi na mchango mkubwa wa vijana katika maendeleo ya Taifa. Aidha, ninamshukuru kwa kuniteua kuwa Waziri chini ya Ofisi yake na ninaahidi kuwa, dhamana aliyonipa nitaitekeleza kwa uaminifu, ufanisi na uadilifu mkubwa, ili kutimiza matarajio yake katika kutatua changamoto za vijana na kusimamia maendeleo yao kwa manufaa ya Watanzania.

**5.** **Mheshimiwa Spika**, ninapenda pia kumpongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini na ufuatiliaji anaoufanya katika kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Wakati wote amekuwa mstari wa mbele katika kutoa miongozo mbalimbali ya kuhakikisha ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za kiuchumi zinazoleta maendeleo.

**6.** **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuiongoza

Zanzibar kwa kipindi cha pili kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Aidha, ninampongeza kwa uongozi wake Madhubuti na juhudi zake za kuendeleza ustawi wa vijana. Tunatambua na kuthamini mchango wake mkubwa katika kuimarisha fursa za ajira, kukuza ujasiriamali, na kuboresha mazingira ya elimu na mafunzo kwa vijana. Maono yake yamekuwa chachu ya maendeleo na yanawapa matumaini vijana wengi kufikia ndoto zao.

**7. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.)**, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampongeza kwa kuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025 – 2030. Aidha, ninamshukuru kwa kuendelea kutuongoza vyema na kuweka dira katika utekelezaji wa majukumu ya kuendeleza vijana nchini. Napenda kukiri kuwa, kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimejifunza mengi sana kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali – **Nasema asante sana.**

**8. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb)** na Naibu Spika **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb)** kwa kuchaguliwa kuliongoza na kulisimamia Bunge kwa hekima na umahiri mkubwa kwa kushirikiana na Wenyeviti wa Bunge. Aidha, ninapenda kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu mbalimbali yanayochochea maendeleo ya Taifa letu. Ninawashukuru pia kwa namna wanavyoshirikiana nami katika utekelezaji wa majukumu ya kusimamia Sekta ya Maendeleo ya Vijana kwa manufaa ya Watanzania wote. Kwa namna ya pekee ninamshukuru **Mheshimiwa Deus Clement Sangu**, Mbunge wa Jimbo la Kwela, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu. Nikiri kuwa misingi kuhusu masuala ya vijana iliyowekwa kupitia iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inaendelea kuwa

chachu katika kuendeleza sekta ya maendeleo ya vijana nchini. Vilevile, ninawapongeza wabunge wenzangu kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwakilisha Wananchi katika Bunge lako tukufu.

**9. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma** (Mbunge Viti Maalum), Makamu Mwenyekiti, **Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima** (Mbunge Viti Maalum) na Wajumbe wote wa Kamati kwa michango, ushauri na miongozo wanayoendelea kutupatia. Ni ukweli usiopingika kuwa, Kamati hii imekuwa msaada mkubwa sana kwangu ikizingatiwa kuwa **Ofisi ni mpya! na Waziri ni Mpya! – Hakika ninashukuru sana!** Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana itaendelea kushirikiana kwa karibu na Kamati hii kwa manufaa ya vijana na maslahi mapana ya Taifa letu. Aidha, ninamshukuru Katibu wa Bunge **Ndugu Baraka Ildephonce Leonard** kwa ushirikiano wake thabiti kupitia wasaidizi wake wanaosimamia Kamati mbalimbali. Ushirikiano huu umeimarisha utendaji wa Kamati na kuendeleza dhana ya uwajibikaji na uwazi katika shughuli za Bunge. Ni kwa mshikamano huu tunapata nguvu ya kusonga mbele na kutimiza matarajio ya wananchi wetu.

**10. Mheshimiwa Spika**, sina budi kuwashukuru kwa dhati Viongozi wenzangu na Watendaji wa Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana kwa ushirikiano, ubunifu, usimamizi na utekelezaji wa mikakati yake. Kipekee, ninapenda kumshukuru **Bi. Jenifa Christian Omolo** - Katibu Mkuu; na **Dkt. Kedmon Elisha Mapana** - Naibu Katibu Mkuu, kwa uchapakazi wao, umahiri na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli zangu za kila siku. Vilevile, ninawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na Watumishi wote kwa ushirikiano wao na juhudi wanazozifanya katika kufanikisha malengo ya Wizara. Ninaliahidi Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na falsafa ya: ‘’**Kufanya Kazi kwa Kasi**; **Kufikika na Matumizi ya Teknolojia ili Kuwafikia Vijana Wengi Zaidi’’.**

**11. Mheshimiwa Spika**, ninaomba nitumie fursa hii kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa pole kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwa kumpoteza Kiongozi wetu mpendwa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani-Iringa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. Pia ninatoa pole kwa kuondokewa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Peramiho - Ruvuma na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi). Kwa hakika tutaendelea kuwakumbuka na kuwaenzi kwa michango yao na mambo makubwa waliyofanya katika Sekta ya Maendeleo ya Vijana na Taifa kwa ujumla. Vilevile, ninaungana na Mhe. Waziri Mkuu kutoa pole kwa Watanzania waliokumbwa na kadhia mbalimbali kama vile ajali, moto na kadhia nyingine.

**Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema majeruhi wote na tunamuomba azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.**

**12. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo ya utangulizi, ninaomba sasa nijielekeze katika maeneo mahususi ya hotuba hii ambayo ni: Hali halisi ya vijana nchini; Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Maendeleo ya vijana kwa mwaka 2025/26; na Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Fungu 104 – Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2026/27.

## HALI HALISI YA VIJANA NCHINI

**13. Mheshimiwa Spika,** Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, zinaonesha kuwa Tanzania Bara ina jumla ya vijana 20,612,566 wenye umri wa miaka 15 hadi 35 ambao ni sawa na asilimia 34.4 ya idadi ya watu wote. Aidha, kwa mujibu wa Utafiti wa Nguvu Kazi wa Mwaka 2020/21, vijana wanachangia zaidi ya asilimia 55 ya nguvu kazi ya Taifa. Takwimu hizi zinaonesha wazi kuwa vijana ndio sehemu kubwa zaidi ya nguvu kazi inayoshiriki katika shughuli za kiuchumi nchini. Hivyo, maendeleo ya vijana yana uhusiano wa moja kwa moja na tija ya uzalishaji, ukuaji wa

sekta mbalimbali za uchumi, pamoja na uwezo wa Taifa katika kuzalisha mali na huduma.

**14.** **Mheshimiwa Spika,** ni ukweli usiopingika kuwa, pamoja na ukubwa wa nguvu kazi ya vijana iliyopo nchini, nguvu kazi hii imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: **Kwanza,** ukosefu wa ajira ambapo kwa mujibu wa Utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2021, vijana wameendelea kukabiliwa na ukosefu wa ajira kwa asilimia 12.2 (Me 8.1% na Ke 16.1%); **Pili,** nguvu kazi iliyopo inaupungufu wa ujuzi wa mahitaji wa soko la ajira kwa kiwango cha chini cha asilimia 76.9 badala ya asilimia 54; kiwango cha kati asilimia 19.9 badala ya asilimia 34 na kiwango cha juu ni asilimia 3.2 badala ya asilimia 12 kwa nchi zenye Uchumi wa kati. **Tatu**, changamoto nyingine ni pamoja na vijana kutokidhi vigezo vya mikopo vilivyowekwa na Taasisi za fedha, upatikanaji mdogo wa mitaji na fursa za biashara, matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana, upungufu wa malezi na mwongozo stahiki, Athari za shinikizo rika pamoja na matumizi yasiyo sahihi ya mitandao ya kijamii, na kuongezeka kwa tatizo la afya ya akili.

**15.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua changamoto za vijana, Serikali imefanya jitahada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutunga Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 Toleo la mwaka 2024 na kutekeleza Programu mbalimbali za uwezeshaji kwa vijana. Pamoja na jitihada hizo, changamoto za vijana zimeendelea kuwepo. Kwa kutambua hivyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uamuzi wa makusudi wa kuanzisha Wizara maalumu kupitia Tangazo la Serikali Na. 685 na 686 linalotoa mgawanyo wa majukumu ya Wizara ambayo ni kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera zinazohusu maendeleo ya vijana; uratibu wa maendeleo ya vijana, dhana ya kujitolea; uratibu wa elimu ya uraia kwa vijana, ustawi wa vijana, ushirikishwaji na uwezeshaji wa vijana kiuchumi; uratibu wa majukwaa ya vijana; kuboresha utendaji na Maendeleo ya Rasilimali Watu; na kusimamia Taasisi zilizo chini ya Ofisi. Hatua hii ni ushahidi wa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** katika kuhakikisha vijana wanakuwa mstari wa mbele katika safari ya kulijenga Taifa letu.

**UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA VIJANA KWA MWAKA 2025/26.**

**Kuendelea Kusimamia Programu za Uwezeshaji Vijana Kiuchumi.**

**16. Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia programu za uwezeshaji vijana kiuchumi, Wizara imetoa mikopo ya vifaa yenye thamani ya shilingi 824,463,770 kwa Vijana 126 katika Mkoa wa Mwanza (39); Mtwara (40); Mbeya (22); Rukwa (10) na Arusha (15) kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuwawezesha kujiajiri na kuajiri wengine. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha mifumo ili kupunguza changamoto na vikwazo vilivyokuwepo hapo awali. Kwa sasa, mikopo inatolewa kwa vikundi na kwa kijana mmoja mmoja; ina kipindi cha rehema (***grace period***) kuanzia miezi mitatu (3) hadi miezi sita (6), isipokuwa kwa miradi maalumu ya kilimo, uvuvi na ufugaji kipindi cha rehema ni miezi nane (8); riba imepunguzwa hadi asilimia tano (5) kwa kipindi chote cha mkopo; imejikita kwenye uwezeshaji wa vifaa badala ya fedha pekee; na Wizara imeingia makubaliano na Taasisi za kifedha kwa ajili ya kutoa mikopo na mafunzo kwa vijana ambapo, wanufaika hupatiwa mafunzo kabla ya mkopo na wakati wa uzalishaji.

**17. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza ahadi ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya biashara ndogo, za kati na kampuni changa (Start-Ups), tarehe 5 Februari, 2026, Ofisi ya Rais Maendeleo ya vijana ilikabidhiwa hundi yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 200** na kupewa jukumu la usimamizi na uratibu. Fedha hizo zinatolewa kupitia Sekta mbalimbali zikiwemo: Sekta ya Vijana; Kilimo; Madini; Mifugo na Uvuvi; Viwanda na Biashara; Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; na Wizara ya Fedha.

**18. Mheshimiwa Spika**, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya kukabidhiwa jukumu la uratibu, kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, Wizara yangu imeanzisha Programu ya

Kitaifa ya Uwezeshaji vijana Kiuchumi na kuandaa Mwongozo wa Utekelezaji wa programu hiyo. Mwongozo huo umejikita katika kuweka viwango vya ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa wakopaji na wakopeshaji wa fedha hizi za umma. Mwongozo pia umeainisha taratibu za utoaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo na sifa za wakopaji sambamba na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini. Utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya uwezeshaji wa vijana kiuchumi umeanza na hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya maombi 30,384 ya Mikopo ya miradi ya vijana yamepokelewa na yanaendelea kufanyiwa uchambuzi.

**19.** **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya kuwezesha vijana kiuchumi, kiasi cha shilingi bilioni 48.6 kimetolewa kwa awamu ya kwanza katika sekta za uzalishaji na huduma ambazo ni; kilimo, mifugo na uvuvi, biashara na viwanda vidogo, sanaa na ubunifu, maendeleo ya jamii, pamoja na teknolojia na huduma za kidijitali. Uwekezaji katika sekta hizo umezingatia maeneo yenye fursa kubwa za ajira na uzalishaji mali, ambapo vijana wengi wanajishughulisha. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu itakapokamilika inatarajia kunufaisha vijana takribani 10,000. Aidha, katika awamu ya pili ya utekelezaji wa programu hiyo, Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana imepokea kiasi cha Shilingi bilioni 2.5, ambacho kinatarajiwa kunufaisha vijana wapatao 888 kupitia miradi 36 katika Sekta za Viwanda, biashara ndogondogo, kilimo, Uvuvi na mifugo ambapo ajira 4,440 zinatarajia kuzalishwa. Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa inawanufaisha makundi yote ya vijana kwa usawa bila kujali itikadi zao au maeneo yao ya kijiografia.

**20.** **Mheshimiwa Spika**, vijana pia wamekuwa wakiwezeshwa kupitia asilimia nne (4) ya makusanyo ya ndani ya Halmashauri ambapo kwa mwaka 2025/26, vikundi 5,199 vya vijana vilinufaika na mikopo yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 52.168. Kupitia mikopo hii, vijana wameweza kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi, kukuza biashara, kuongeza ajira, na kuinua hali za maisha. Ninaomba nimpongeze Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kwa kuendelea kuratibu na kusimamia

utengaji wa fedha zitokanazo na mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuwawezesha vijana kiuchumi.

**Kukuza Ujuzi kwa Vijana**

**21. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Ajira na Mahusiano pamoja na Wizara ya elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) katika kukabiliana na changamoto ya ajira kwa vijana kupitia Programu ya kukuza ujuzi, ambapo katika mwaka 2025/26 mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi yametolewa kwa vijana 5,746 katika Vyuo na Taasisi za mafunzo 46. Vilevile, mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa njia ya utarajali kwa vijana 2,500 na mafunzo maalum ya kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi kwa vijana 7,826 yametolewa. Pia, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta zinazotekeleza programu za kukuza ujuzi kwa vijana.

**22. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana inasimamia vituo vitatu vya Maendeleo ya Vijana vya Sasanda (Songwe), Marangu (Kilimanjaro) na Ilonga (Morogoro) vyenye lengo la kuimarisha utoaji wa mafunzo ya muda mfupi ili kuwapatia vijana ujuzi katika eneo la Kilimo, TEHAMA na Ujasiriamali. Hata hivyo, vituo hivyo vilisitisha kutoa huduma kutokana na uhaba wa Wakufunzi na uchakavu wa miundombinu (majengo na Madarasa). Kutokana na hali hiyo, Wizara imefanya tathmini ya uchakavu wa miundombinu katika Vituo vya Sasanda (Songwe) na Ilonga (Morogoro) kwa lengo la kufanya ukarabati kwa awamu ili vianze kutoa huduma. Baada ya kukarabatiwa, vituo hivyo vinatarajiwa kuwa na uwezo wa kudahili jumla ya vijana 300 kila robo mwaka kwa kila kituo, sawa na vijana 1,200 kwa mwaka kwa kila kituo.

**Utoaji wa Elimu na Fursa za Kiuchumi**

**23. Mheshimiwa Spika**, kupitia makongamano, warsha na majukwaa ya vijana, Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana imetoa elimu kwa vijana 15,753 kuhusu elimu ya afya ya akili; ujasiriamali; uongozi wa biashara; utunzaji wa hesabu; na elimu ya mikopo. Aidha, vijana hao pia walipata elimu kuhusu fursa zilizopo katika

Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Mamlaka ya Mapato Tanzania – TRA. Vilevile vijana walipata elimu kutoka PPRA kuhusu takwa la Sheria ya Ununuzi wa Umma inayoelekeza kutengwa kwa asilimia 30 ya zabuni za Umma kwa ajili ya makundi maalum ambapo kati ya hizo asilimia 10 ni kwaajili ya vijana. Kupitia elimu hiyo, vijana waliweza kujisajili katika mfumo wa Kielektroniki wa manunuzi ya Serikali (NeST) ambapo vikundi 299 vya vijana vyenye jumla ya vijana 2,226 vimenufaika kwa kupata zabuni zenye thamani ya Shilingi bilioni 13.2

**Kuimarisha Ushirikishaji wa Vijana na Kusikiliza Maoni Yao**

**24. Mheshimiwa Spika**, baada ya kuundwa kwa Ofisi ya Rais Maendeleo ya vijana, kulikuwa na dhamira ya kufahamu kwa kina mahitaji ya vijana, mawazo yao pamoja na mitazamo yao kuhusu masuala mbalimbali yanayogusa maisha yao ya kila siku. Hivyo, Wizara iliandaa ziara za kukutana na vijana kwa lengo la kutoa jukwaa la wazi la kusikiliza sauti zao, kuelewa changamoto wanazokumbana nazo na kupokea mapendekezo yao. Jitihada hizo zimewezesha Ofisi ya Rais -Maendeleo ya Vijana kuelewa changamoto za vijana. Hivyo, kuwa katika nafasi ya kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati inayolenga kuboresha elimu ya uraia, kukuza uzalendo na kuwajengea vijana mazingira bora ya kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa.

**25. Mheshimiwa Spika,** kutokana na dhamira hiyo, Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana ilifanya ziara maalum katika Mikoa sita (6) ya Songwe, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Dar es Salaam na Dodoma, ambapo jumla ya vijana 8,120 walitembelewa katika maeneo 18 wanayofanyia kazi. Katika majadiliano hayo, hoja 186 ziliibuliwa. Uchambuzi wa hoja hizo ulibaini kuwa hoja zilizoongoza kuchangiwa na vijana wengi ilikuwa ni: Ukosefu wa ajira (13.47%); maslahi duni ya vibarua wanavyofanya (9.68%); Miundombinu ya kufanyia biashara kutokuwa rafiki (9.68%); Changamoto za usafiri na usafirishaji (9.82%); upatikanaji wa mikopo ya asilimia nne (4) mapato ya ndani ya Halmashauri (10.52%); ukosefu wa mitaji (10.53%); vigezo vigumu vya mikopo ya elimu ya juu (6.99%); hofu ya kutoa maoni (6.45%);

**26. Mheshimiwa Spika**, hoja nyingine zilizoibuliwa zilikuwa ni mfumo wa elimu usioendana na soko la ajira (5.91%); utitiri wa kodi na ushuru (5.03%); kutokuwa na elimu ya ujasiriamali (4.84%); urasimu wa kupata leseni na vibali (4.23%); na kukosekana kwa Baraza la Vijana la Taifa (3.23%). Takwimu hizo zinaonesha kuwepo kwa uelewa na mwamko wa vijana katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisera. Aidha, zoezi hili limekuwa chachu ya uwajibikaji, ushiriki wa vijana katika maendeleo, na kujiamini katika kutoa maoni. Wizara itaendelea kupokea maoni na mapendekezo ya vijana na kuzitafutia ufumbuzi.

**Kukuza Majadiliano ya Kitaifa Kupitia Kongamano la Wajasiriamali na Bodaboda**

**27. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana iliratibu kongamano lililowakutanisha zaidi ya washiriki 1,200 Jijini Dar es Salaam tarehe 08 Januari, 2026 ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kongamano hilo pia lilihudhuriwa na Wizara za Kisekta zikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano; Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za u onia Serikali za Mitaa; Wizara ya Viwanda na Biashara; na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu. Lengo la kongamano hilo lilikuwa kuwaweka vijana u oni na kusikiliza maoni yao.

**28. Mheshimiwa Spika**, kupitia kongamano hilo, Vijana walipata fursa ya kuwasilisha changamoto zinazowakabili zikiwa ni u oni na kukosa vitambulisho vya wajasiriamali, utitiri wa kodi, kukosa maeneo ya kufanyia kazi, kutotambuliwa, kukosekana mifumo rafiki ya usajili na gharama za leseni. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta inaendelea kutafutia ufumbuzi changamoto hizo. Hatua hii imeendelea kuwaunganisha vijana na serikali na kuwafanya kuwa sehemu ya kutafuta majawabu ya changamoto zinazowakabili, kuimarisha mawasiliano, na kuhamasisha uzalendo kwa kuwajengea vijana hisia za kuthaminiwa na kusikilizwa.

**Kuongeza Ushiriki na Ushirikishaji wa Vijana Kupitia Jukwaa la Vijana (Vijana *Platform*)**

**29. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana ilizindua Majukwaa ya Vijana **(Vijana *Platforms*)** katika Mikoa 6 ambayo ni; Dar es Salaam, Singida, Mwanza, Shinyanga, Mtwara na Tabora. Kupitia majukwaa hayo jumla ya vijana 7,500 walihudhuria na zaidi ya washiriki 20,000,000 walifuatilia kupitia mitandao ya kijamii (*Instagram, facebook, Youtube na Tiktok)*. Pia, uzinduzi wa majukwaa hayo ulikuwa mubashara kupitia vyombo mbalimbali vya Habari. Lengo la majukwaa u oni kukutanisha vijana wa makundi mbalimbali, ili kwa u oni waweze kujadili kwa kina masuala yanayohusu maendeleo ya vijana katika ngazi mbalimbali za Vijijini na Mijini, na kutoa mapendekezo ya namna bora ya ushiriki katika ujenzi wa Taifa. Mapendekezo hayo yatatumika kama dira na mwelekeo wakati wa uandaaji wa Mipango, Sera na Maamuzi ya Serikali yanayohusu masuala ya vijana.

**30. Mheshimiwa Spika,** katika uzinduzi huo, Wizara pia ilizindua namba maalum za huduma kwa wateja (*Call Centre*). Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya vijana **1,641** (KE 519, ME 1,122) wamewasilisha changamoto na mapendekezo kuhusu masuala ya vijana ikiwemo fursa za mikopo. Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana imefanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa ikiwa ni u oni na kutoa elimu kuhusu vigezo na utaratibu wa upatikanaji wa mikopo.

**Uratibu wa Masuala ya Vijana**

**31. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana, iliratibu kikao kazi cha Maafisa Maendeleo ya Vijana wa u onia Halmashauri kilichofanyika tarehe 17-18 Disemba, 2025 Mkoani Dodoma. Kikao hicho kililenga kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na utekelezaji wa programu za vijana kuanzia ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mikoa hadi Taifa. Aidha, Wizara inaandaa mfumo wa uratibu wa masuala ya vijana nchini na Kanzidata ya Kitaifa itakayokusanya taarifa za masuala ya vijana. Lengo la kuandaliwa kwa mfumo u oni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa afua na ushiriki wa vijana katika shughuli za maendeleo ya vijana

na kuwezesha wadau kutoka katika sekta ya Umma na Binafsi kutekeleza programu za uwezeshaji vijana.

**32. Mheshimiwa Spika,** Wizara inasimamia Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, Sura ya 441 ambayo inatoa utaratibu wa uanzishwaji wa mabaraza ya vijana nchini. Hata hivyo, kutokana na mahitaji ya sasa ya vijana, Serikali imeanza mapitio ya Sheria hiyo ili kukidhi mahitaji hayo sambamba na kuhakikisha vijana wanapata nafasi pana ya kushiriki katika kupanga na kuamua mustakabali wa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Katika kufanya maboresho hayo Wizara imefanya ziara ya mafunzo kwa kutembelea Zanzibar na nchi ya Namibia kwa lengo la kujifunza juu ya uendeshaji wa Mabaraza hayo hususan Muundo wa Baraza la Vijana na masuala ya fedha na miradi inayotekelezwa na Baraza la Vijana. Kwa sasa Wizara inaendelea kukusanya maoni kwa wadau wengine ikiwemo vijana.

**Kuimarisha Ustawi na Makuzi ya Vijana**

**33. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ustawi na makuzi ya vijana, Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Stadi za Maisha unaolenga kuwajengea vijana uwezo wa kujitambua, kuhimili changamoto za maisha, kufanya maamuzi sahihi na kuwasiliana kwa ufanisi. Kupitia mwongozo huu, Serikali inalenga kujenga kizazi chenye afya njema ya akili, chenye kujiamini na uwezo wa kujitegemea katika kufikia malengo.

**Uratibu wa Mwenge wa Uhuru**

**34. Mheshimiwa spika**, Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji - Zanzibar imeratibu uzinduzi wa mbio za Mwenge wa Uhuru uliofanyika tarehe 02 Aprili, 2026 katika uwanja wa Mpira Gombani Mkoa wa Kusini Pemba. Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alikuwa **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mwenge wa Uhuru utakimbizwa katika Mikoa 31 na Halmashauri 195 za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru, miradi na shughuli mbambali za maendeleo zinatarajiwa

kukaguliwa na kuzinduliwa. Ujumbe wa mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2026 unalenga katika ujenzi wa **Amani, Umoja na Mshikamano wa Kitaifa** chini ya kauli mbiu isemayo ‘’***Tanzania ni yetu Sote, Tushikamane kwa Pamoja Tulete Maendeleo’’.*** Kupitia mbio za Mwenge wa Uhuru wananchi wanaendelea kuhamasishwa kushiriki mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya; Malaria; UKIMWI; Rushwa; na kuzingatia Lishe bora kwa afya imara. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Mwongozo wa mbio za Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2002 Toleo la mwaka 2026 ambao ulizinduliwa siku ya Uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa.

### Changamoto za Utekelezaji na Mikakati ya Kukabiliananazo

**35. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Wizara hii ni mpya, imeanza kutekeleza majukumu yake katika mazingira ya kuanzisha mifumo na kujenga misingi imara ya maendeleo ya vijana ndani ya Taifa letu. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo:-

(i) Ongezeko la uhitaji wa mikopo ukilinganisha na kiasi cha fedha kinachotengwa;

(ii) Baadhi ya vijana kukosa ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira;

(iii) Uelewa mdogo wa masuala ya stadi za maisha, Elimu ya Uraia, uzalendo, afya ya uzazi, athari za matumizi ya dawa za kulevya, na matatizo ya afya ya akili; na

(iv) Miradi ya vijana kutokuwa endelevu.

**36. Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto hizo Wizara imejipanga kutekeleza mikakati ifuatayo: -

(i) Kuendelea kushirikisha wadau wa maendeleo ili kuchangia bajeti za programu mbalimbali za vijana;

(ii) Kuendelea kutoa elimu kuhusu mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya vijana kwa kushirikiana na Taasisi za Kifedha;

(iii) Kuendelea kutoa elimu kuhusu stadi za maisha, elimu ya uraia na uzalendo ili kujenga kizazi cha vijana kinachojua haki na wajibu wao, kinachopenda nchi yao na kinachoshiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa;

(iv) Kuendelea kutoa ujuzi kwa vijana kupitia vituo vya Maendeleo ya vijana ili vijana waweze kupata mafunzo ya muda mfupi kuhusu kilimo, ujasiriamali, ujasiri na TEHAMA;

(v) Kuendelea kutoa elimu na kujenga uwezo kupitia Mwongozo wa Kitaifa wa mafunzo ya Stadi za Maisha na Mwongozo wa uratibu wa programu ya stadi za maisha kwa vijana;

(vi) Kuendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta katika kukabiliana na changamoto za ajira ikiwemo kukuza ujuzi kwa njia ya Uanagenzi (Apprenticeship skills), kurasimisha ujuzi uliopatikana katika mfumo usio rasmi wa mafunzo (Recogniton for Prior Leaning Skills); kupata mafunzo ya Uzoefu wa Kazi (Internship skills), na Mafunzo ya kukuza ujuzi kwa walio makazini (Upskilling skills) kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano; Jenga Kesho iliyobora (Build Better Tomorrow) inayosimamiwa na Wizara ya Kilimo na Programu ya *Mining for a Brighter Tommorrow* (MBT) inayosimamiwa na Wizara ya Madini;

(vii) Uchambuzi wa fursa (opportunity mapping) utafanyika kwa lengo la kubaini na kutambua fursa zilizopo katika maeneo mbalimbali, pamoja na kukusanya taarifa muhimu zitakazowezesha kuwashirikisha vijana kuhusu fursa hizo. Hatua hii italenga kuhakikisha vijana wanapata uelewa sahihi wa rasilimali na nafasi zilizopo katika mazingira yao, ili waweze kuzitumia kikamilifu kwa maendeleo yao binafsi na ya jamii kwa ujumla. Hii ni pamoja na fursa zilizopo katika Wizara za kisekta; na

(viii) Kuandaliwa kwa Mfumo wa uratibu wa masuala ya vijana utakaowawezesha kukusanya, kuhakiki na kuhifadhi taarifa sahihi kuhusu vijana ili kuwa na Kanzidata itakayojumuisha mahitaji, sifa, ujuzi na maeneo yao ya kipaumbele. Mfumo huu utatumika katika uombaji wa mikopo kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana. Taarifa hizi zitatumika kuwezesha utambuzi wa uwezo na changamoto zao kwa ufanisi zaidi, pamoja na kurahisisha mchakato wa kuwaunganisha na fursa mbalimbali za ajira, mafunzo, ubunifu na uwezeshaji, kulingana na vigezo vinavyolingana na wasifu wao. Hatua hii itachangia kuongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za maendeleo na kuinua ustawi wao kiuchumi na kijamii.

**MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27**

**37. Mheshimiwa Spika**, Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana (Fungu104) kwa Mwaka 2026/27 yameandaliwa kwa kuzingatia Miongozo mbalimbali ikiwemo: Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27- 2028/29; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31); Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la mwaka 2024; Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030; Sheria ya Bajeti, Sura ya 439; Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31) na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 (Sustainable Development Goals – SDGs, 2030).

**38. Mheshimiwa Spika,** Mpango huu pia umezingatia Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne (20232030); Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134; Hotuba ya Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa wakati akihutubia Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025 (Dodoma) na Maelekezo mengine ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

**Vipaumbele vya Mpango**

**39. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2026/27, Mpango wa Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana utatekelezwa kupitia vipaumbele vifuatavyo: -

(i) Kuimarisha ukuzaji wa biashara na uwezeshaji wa vijana kiuchumi kwa lengo la kuwezesha vijana wengi kujiajiri na kuajiriwa katika sekta za biashara na uzalishaji;

(ii) Kuimarisha uratibu na ushirikishaji wa vijana katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa;

(iii) Kuimarisha uratibu wa elimu ya uraia, uzalendo na uratibu wa Mwenge wa Uhuru; na

(iv) Kuimarisha ustawi na makuzi kwa vijana.

**SHUGHULI ZITAKAZOTEKELEZWA KWA MWAKA 2026/27**

**40. Mheshimiwa Spika,** shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2026/27 zitatokana na vipaumbele vilivyoainishwa katika ibara ya 39.

**Kuimarisha Uratibu na Ushirikishaji wa Vijana katika Masuala ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa**

**41. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuimarisha uratibu na ushirikishaji wa vijana kwa kuandaa Mfumo wa Taifa wa uratibu wa masuala ya maendeleo ya vijana nchini; Kuandaa Kanzidata ya kitaifa itakayokusanya taarifa za masuala ya vijana; Kufanya Mapitio ya Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa Sura ya 441; Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Vijana, Amani na Usalama; na Kuwezesha Vijana kushiriki katika majukwaa na programu mbalimbali za Kikanda, Maziwa Makuu na Kimataifa, kuhusu Amani na Usalama; na kukusanya maoni na mrejesho kwa masuala ya vijana nchini kupitia dawati la Huduma kwa Wateja. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 yenye malengo ya kuimarisha maendeleo ya kiuchumi kwa vijana; kukuza ajira na ujasiriamali; kuendeleza stadi za maisha na ujuzi

kwa vijana; kuimarisha ushiriki wa vijana katika maamuzi na uongozi; kulinda na kuendeleza haki na ustawi wa vijana; kuimarisha huduma za afya na ustawi wa vijana; kukuza maadili, uzalendo na uwajibikaji kwa vijana; kuimarisha upatikanaji na matumizi ya TEHAMA kwa vijana; kukuza vipaji, ubunifu na michezo; kuimarisha ujumuishwaji wa vijana wote wakiwemo vijana, wanawake na watu wenye ulemavu; kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya maendeleo ya vijana; kuendeleza tafiti, takwimu na mifumo ya taarifa za vijana; pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala ya maendeleo ya vijana.

**Kuimarisha Uratibu wa Elimu ya Uraia, Uzalendo na Mwenge wa Uhuru**

**42. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uratibu wa elimu ya uraia, uzalendo na Mwenge wa Uhuru, Wizara itaendelea kuratibu majukwaa ya vijana katika mikoa na Halmashauri nchini; Kuratibu utoaji wa elimu ya uraia na uzalendo katika halmashauri 184; Kuratibu mbio za Mwenge wa Uhuru na wiki ya vijana kitaifa; Kuratibu maadhimisho ya siku ya wanaojitolea Kimataifa, siku ya vijana Afrika pamoja na siku ya Vijana Kimataifa.

**Kuimarisha Ustawi na Makuzi kwa Vijana**

**44. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ustawi na makuzi kwa vijana, Wizara itaendelea kuandaa na kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa mafunzo ya Stadi za Maisha; kuandaa programu ya Kitaifa ya kushughulikia masuala ya ustawi wa vijana; kuandaa Mwongozo wa msaada wa kisaikolojia kwa vijana; na kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa vijana.

**Kuimarisha Ukuzaji wa Biashara na Uwezeshaji wa Vijana Kiuchumi**

**45. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ukuzaji wa biashara na uwezeshaji wa vijana kiuchumi, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu ujasiriamali na ujuzi wa usimamizi wa biashara kwa vikundi vya vijana nchini; kutoa mikopo nafuu kwa

vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine; kukarabati vituo vitatu vya mafunzo kwa vijana vya Sasanda, Ilonga na Marangu ili kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za kilimo biashara, TEHAMA na ujasiriamali; Aidha, Serikali itafanya utafiti wa uanzishwaji wa vituo vya ubunifu vya kitaifa kwa vijana pamoja na kuanzisha vituo vya ubunifu kwa vijana (VIJANA *Hub*) vitakavyolenga kukuza ubunifu, kuendeleza vipaji, kutoa huduma za uratibu wa mawazo ya biashara, pamoja na kuwaunganisha vijana na fursa za masoko, teknolojia na mitaji kwa ajili ya kuongeza ushindani na tija katika shughuli zao za kiuchumi; kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa fursa za uwezeshaji kiuchumi ndani na nje ya nchi; kufanya mapitio ya Mwongozo wa utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana wa mwaka 2022; kuandaa mfumo wa kielektroniki wa uwezeshaji wa vijana.

**46. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia itafanya utafiti wa uanzishwaji wa **Benki ya Vijana** kwa lengo la kuchambua kwa kina ili kuwa na taasisi maalum ya kifedha itakayojikita katika mahitaji ya vijana. Dhamira ya Serikali ni kuweka msingi wa mfumo wa kifedha unaoendana na mazingira na uwezo wa vijana wengi, hususan wale wanaoanza shughuli za kiuchumi, ili kuondoa vikwazo vilivyopo katika upatikanaji wa mitaji. Benki ya Vijana, itakayoanzishwa, itakuwa chombo muhimu cha kimkakati kitakachowezesha upatikanaji wa huduma za kifedha zilizo rafiki kwa vijana, kuchochea ubunifu wa bidhaa za kifedha zinazolingana na mahitaji yao, kupanua wigo wa uwekezaji wa vijana, na hatimaye kuongeza ajira na mchango wa vijana katika kukuza uchumi shindani na jumuishi wa Taifa**.**

## MUHTASARI WA MAOMBI YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27

**47. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2026/27, Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 35,957,298,000** (***Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Tisa Hamsini na Saba, Laki mbili Tisini na Nane Elfu***) kwa mchanganuo ufuatao: -

(i) Kiasi cha **Shilingi 30,104,264,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya kiasi hicho **Shilingi 1,227,961,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 28,876,303,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); na

(ii) Kiasi cha **Shilingi 5,853,034,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,000,000,000** ni fedha za ndani za maendeleo na **Shilingi 853,034,000** ni fedha za nje za maendeleo.

**HITIMISHO**

**48. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/26 yametokana na ushirikiano wa Wizara za Kisekta, Wadau wa Maendeleo, Mashirika Mahsusi yanayojishughulisha na masuala ya Vijana, Taasisi za fedha, vyombo vya habari, Taasisi zisizo za kiserikali, Taasisi za kidini, Waandishi wa Habari, Vijana na Wananchi kwa ujumla. ***Vijana Tuyajenge Tanzania ni Yetu!!!.***

**47. Mheshimiwa Spika**, Leo ninasimama mbele yenu nikiwa na heshima kubwa na moyo wa shukrani. Safari yangu ya kufika hapa isingewezekana bila msaada wa familia yangu. Wamekuwa nguzo na faraja yangu wakati wa changamoto, na chanzo cha matumaini yangu kila siku.

**48. Mheshimiwa Spika,** Ninapenda kuwashukuru wazazi wangu **Bw. Gray Nanauka na Bibi. Angela Nanauka** kwa malezi na maadili waliyoniwekea, ambayo yameniongoza hadi kufika hatua hii. Sambamba nao, ninawashukuru ndugu zangu wote kwa kunitia moyo na kunikumbusha thamani ya mshikamano wa kifamilia. **Kipekee kabisa,** ninamshukuru Mke wangu kipenzi **Rachel Nanauka na Watoto wangu wapendwa Joyous, Joyceline na Jonel** kwa uvumilivu na upendo wao usio na kifani. Hakika familia yangu imekuwa taa na mwanga wangu, na leo ninapopokea heshima ya kuzungumza mbele ya Bunge hili tukufu,

ninaitambua na kuishukuru kwa dhati. Hii siyo tu heshima yangu, bali ni heshima yao pia. **Mungu awabariki sana.**

**49. Mheshimiwa Spika**, kwa moyo uliojaa furaha na matumaini napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini kwa kuniamini na kunichagua ili kushirikiana nao katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu. Ushirikiano wao na maoni yao, ndivyo vilivyowezesha mafanikio tuliyonayo leo. Imekuwa miezi sita (6) ya utendaji ulioacha alama kubwa kwa Jimbo la Mtwara Mjini. Kwa unyenyekevu mkubwa ninawaahidi sitawaangusha. **Asanteni sana.**

**50. Mheshimiwa Spika**, Nikiwa Mbunge na Waziri kwa mara ya kwanza ninajifunza kila siku na nitaendelea kujifunza ili kuhakikisha ninawatumikia wananchi wa jimbo langu na vijana kwa ufanisi mkubwa. Niko tayari kushirikiana na Wabunge, Viongozi wenzangu, Watendaji wa Serikali na Wadau wote wa Maendeleo ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Ninaomba muendelee kuniombea, kunishauri na kunipa ushirikiano wenu wa dhati. Kwa pamoja tunaweza kuleta mabadiliko chanya na kujenga mustakabali bora kwa vijana wa Taifa letu. ***Tanzania ni yetu sote, Tushikamane kwa*** **pamoja** ***kuleta maendeleo***!!!.

**51. Mheshimiwa Spika,** katika kuhitimisha ningependa kukumbusha mambo makubwa mawili: **Mosi**, Dhamira ya Serikali kupitia Mhe Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuwapa vijana nafasi muhimu kwenye kuweka mipango, kushiriki kuweka vipaumbele na kuwa sehemu muhimu ya utekelezaji wa mipango ya Serikali. Wizara Yetu, itaendelea kuwaweka vijana katikati ya shughuli zetu za kila Siku. Na katika kufanya hivyo, kama tulivyoanza, tutaendelea kuhakikisha vijana wote wanapata nafasi bila kubaguliwa. Tutawashirikisha wa Mjini na vijijini, Wenye elimu na wasio na elimu, vijana Kutoka vyama vyote vya siasa na hakuna kijana atakayebaguliwa katika kufaidika na fursa. **Hii ni Wizara ya Vijana wote na wote watanufaika kwa haki na usawa.**

**52. Mheshimiwa Spika**, **Pili**, wakati maeneo mengine watatafsiri vijana kama tatizo, Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara ya Maendeleo ya vijana inawaona Vijana kama ni mtaji mkubwa

kwa Maendeleo ya Nchi Yetu, Kwetu sisi vijana sio **"liability"** Ila ni **"asset".** Kwetu sisi vijana wa Nchi hii ni mtaji mkubwa katika kufanikisha Maendeleo ya Nchi Yetu na utekelezaji wa Dira 2050. Ili Taifa letu liendelee tunahitaji ubunifu wa vijana, Mawazo ya vijana na Nguvu ya Vijana. Sawa sawa na Maono ya Mhe Rais, Mikakati ya Wizara ni kuwafanya vijana wa Nchi hii wasiwe watazamaji bali washiriki na wamiliki uchumi wa Taifa letu. **TUTAWASIKILIZA NA TUTAWASHIRIKISHA!**

**53. Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha bajeti ya shilingi **35,957,298,000** ikijumuisha shilingi **30,104,264,000** za Matumizi ya kawaida na shilingi **5,853,034,000** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**54. Mheshimiwa Spika**, Naomba Hotuba yangu hii, pamoja Kitabu cha Hotuba tulichowasilisha na Randama tuliyowasilisha ziingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge lako Tukufu. Aidha, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni https://www.vijana.go.tz

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Joel Arthur Nanauka, kwa hotuba hiyo, hoja hii imeungwa mkono na wote wamesimama.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijaendelea na ratiba inayofuata ninaomba niwatambue wageni wa Mheshimiwa Spika, ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, kutoka Chama cha Wananchi *CUF*. Kuna Ndugu Mirambo Kamil Yusuf, Mwenyekiti wa *CUF* Taifa; Ndugu Haroub Shamsi Makamu, Mwenyekiti *CUF* Zanzibar; Ndugu Miraji Mtimbwiliko, Makamu Mwenyekiti *CUF* Bara na Ndugu Hamad Masoud, Katibu Mkuu *CUF*. Karibuni sana viongozi wetu kutoka Chama cha Wananchi *CUF*. *(Makofi)*

Wakati ninawataja familia ya Mheshimiwa Waziri wetu nilimruka Ndugu Jonel Nanauka, ambaye ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Sasa ninamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kwa ajili ya kutoa taarifa. Mwenyekiti atasoma taarifa, Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Makamu Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti. Karibu sana Makamu Mwenyekiti.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusoma taarifa hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma na ninamshukuru kwa kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na kunipatia afya njema hadi siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za kuwaletea Watanzania maendeleo ikiwemo kuanzishwa kwa Wizara hii ya Maendeleo ya Vijana. Vilevile ninakishukuru chama changu pamoja na UWT Taifa kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Viti Maalum nikiwakilisha Kundi la Vyuo na Vyuo Vikuu. Kwa namna ya pekee ninampongeza sana Mwenyekiti wetu wa UWT Taifa, Mama Mary Chatanda, kwa kuendeleza uongozi thabiti kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaishukuru familia yangu, hususani mume wangu Ndugu Wilson Mashauri Makaranga na watoto wangu, kwa kunipa ushirikiano katika kulitumikia Taifa hili. Baada ya shukrani hizi naomba kusoma Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha

2026/2027. Kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana ilianzishwa Tarehe 19 Disemba, 2025 kupitia Tangazo la Serikali Na. 685. Awali majukumu yanayotekelezwa na Ofisi hii yalikuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye ulemavu. Kwa hiyo basi, taarifa hii itahusisha utekelezaji wa majukumu ya iliyokuwa Idara ya Vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Bila kuathiri Masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, inayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo:-

(i) Msingi na mawanda ya uchambuzi;

(ii) Uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(iv) Ufafanua maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa kwa Serikali; na

(v) Taarifa ya uchambuzi na kuonesha msimamo wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana yanaweka Masharti ya Kanuni za Bunge; Kanuni ya 6(5)(a) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa bajeti na makadirio ya ofisi hii. Aidha, Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Bunge

imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoanishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mawanda ya uchambuzi wa taarifa. Taarifa ya Kamati inahusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hizo ilizitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taaarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoishia na kufanya

ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 25 Machi, 2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana, Fungu 104 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;

(ii) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo;

(iii) Utekelezaji wa vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uzingatiaji na Ushauri wa Kamati. Tarehe 9 Aprili, 2025, Bunge lilipokea na kujadili taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Katika mjadala huo, Kamati iliwasilisha oni moja kuhusu utekelezaji wa Mradi Na. 4,952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Kamati iliitaka Serikali kupelekea fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kuongeza mtaji na uwezo wa Mfuko huo kuhudumia vijana wengi zaidi nchini katika upatikanaji mikopo kupitia Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitika kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 25 Machi, 2026, Serikali haikuwa imepeleka fedha zozote katika Mfuko kama ilivyoidhinishwa na Bunge katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Hali hii inakinzana na nia thabiti ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kushughulikia changamoto za vijana nchini. Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha hizo kwa haraka ili kuiwezesha Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mkoa wa Tanga.

Kamati ilikagua mradi mmoja ambao ni sehemu ya mradi uliotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi bilioni 1,000,000,000 Mradi Na. 4,952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyofafanuliwa awali katika taarifa hii, hadi tarehe 25 Machi, 2026, Serikali haikuwa imepeleka fedha kwa ajili ya mradi huo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Mfuko huo ulikuwa na bakaa ya shilingi milioni 824,463,700 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana kutoka katika bajeti ya mwaka 2024/2025. Kupitia fedha hizo katika Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana umeweza kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 336,815,000 katika mikoa ya Mwanza na Mtwara. Kamati imetaarifiwa kuwa Ofisi ya Rais, Fungu 104 ipo katika hatua za mwisho za kutoa mikopo kwa vikundi vinne vya vijana katika Mikoa ya Mbeya, Arusha na Rukwa kiasi cha shilingi milioni 487,648,770.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa Bunge lako Tukufu linapata taarifa kuhusu mikopo inayotolewa kupitia mradi Na. 4,952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana *(YDF)*, Kamati ilitembelea na kukagua ufanisi wake katika Kikundi cha Mali hai kilichopo Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga. Kikundi kilianza kikiwa na mtaji wa shilingi laki 100,000 iliyotokana na michango ya ada ya kujiunga na unachama wa kikundi. Serikali ilitambua juhudi za kikundi hiki kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kukikopesha mtaji wa shilingi milioni 20,000,000/= katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zimekiwezesha kikundi hiki kuwa na uwezo wa kununua mashine za kuzalisha malighafi za ujenzi kama vile kufyatua tofali, kutengeneza karavati, kuzalisha tofali ndogo maarufu kama *paving blocks*. Aidha, kikundi hicho kimeweza kuunganisha nishati ya umeme katika eneo la uzalishaji hali inayopunguza gharama za matumizi ya mafuta na kuongeza ufanisi na tija ya mradi. Kikundi kimepata mafanikio mengi kwani mtaji wa kikundi kwa sasa umefikia shilingi milioni 52,000,000 ambao umewezesha wanachama wa kikundi kuweza kulipwa

shilingi laki 200,00 kila mwezi. Aidha, kikundi hiki kimeongeza ajira mpya zaidi ya 20 na kusaidia kukuza ujuzi kwa vijana 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza Serikali kwa kutambua mchango wa vijana na kuja na mradi huu unaowezesha vijana kupata mitaji. Aidha, Kamati inawapongeza wanachama wa Kikundi cha Malihai katika kutunza mtaji na kuendelea kuwa kikundi cha mfano kwa vijana nchini. Kamati inatoa wito wa vijana kujitokeza na kuunda vikundi vya uzalishaji mali ili wapate fursa ya kukopa na kujikwamua kiuchumi. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Maendeleo ya Vijana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu Yaliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana hadi Machi, 2026. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kuimarisha ushirikishwaji na usikilizaji wa kero za vijana;

(ii) Kukuza majadiliano ya Kitaifa kupitia kongamano la wajasiriamali na bodaboda;

(iii) Kuongeza ushiriki na ushirikishwaji wa vijana kupitia Jukwaa la Vijana *Vijana Platform*;

(iv) Kupokea Mwongozo wa Kitaifa wa fursa za uwezeshaji kiuchumi ndani na nje ya nchi; na

(v) Kuboresha Mwongozo wa Kitaifa wa matumizi ya stadi za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Mpango na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana, Fungu 104 imepanga kuwa na vipaumbele vinne mahususi kama ifuatavyo:-

(i) Uratibu na Uhamasishaji wa Vijana;

(ii) Kutoa elimu ya Uraia, Uzalendo na Uratibu wa Mwenge wa Uhuru;

(iii) Ukuzaji wa Biashara na uwezeshaji wa Vijana kiuchumi; na

(iv) Ustawi wa Makuzi kwa Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza vipaumbele hivyo, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana itatekeleza shughuli mbalimbali, baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na:

(i) Kuratibu mapitio ya Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa Sura 441;

(ii) Kuboresha mwongozo wa Kitaifa wa fursa za uwezeshaji kiuchumi ndani na nje ya nchi;

(iii) Kuboresha mwongozo wa Kitaifa wa mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana nchini;

(iv) Kufanya tathmini na kutoa elimu ya uraia na uzalendo kwa vijana ili kujenga kizazi kinachojua haki na wajibu wao kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ili kutekeleza mpango na vipaumbele vyake katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) inakadiria kutumia shilingi 30,104,264,000 kwa ajili ya mishahara na Matumizi Mengineyo *(OC)*. Katika fedha hizi, mishahara ni shilingi 1,227,961,000 na matumizi mengine ni shilingi 28,876,303,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio ya matumizi mengineyo ni makubwa kwa sababu ofisi hii ni mpya na itakuwa na shughuli nyingi za usimamizi na uratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Kwa Fungu 104 inakadiriwa kutumia kiasi cha shilingi

5,853,034,000 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, shilingi 5,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 853,034,000 ni fedha za nje. Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana kwa kuweka juhudi za kutenga fedha za ndani kwa 85.4% kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hali hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kushughulikia changamoto za vijana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Rais - Maendeleo ya Vijana, sasa ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni ya jumla Kamati inapendekeza yafuatayo: -

(i) Serikali iendelee kutengeneza fursa kwa vijana, kupata elimu na ujuzi ambao utawawezesha katika kushindana kwenye soko la ajira ili waweze kujitegemea;

(ii) Serikali ihakikishe kuwa inasimamia na kutekeleza majukumu yote yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha unaokwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni mahsusi. Changamoto ya fedha za miradi ya maendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuwa:

(i) Moja ihakikishe inatoa fedha za miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge;

(ii) Iweke mikakati ya kutangaza fursa za mikopo kwa vijana kupitia vipindi vya radio, runinga na mitandao ya kijamii ili kuwafikia vijana wengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya upatikanaji wa ardhi katika shughuli za kiuchumi kwa vijana. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa:-

(i) Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi zishirikiane katika kutambua mahitaji ya vijana na kuwapatia nafasi ya umiliki wa ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji na uwekezaji katika viwanda vidogo;

(ii) Itoe elimu kwa wananchi hususani kundi la vijana kuhusu umuhimu wa kumiliki ardhi kwani ardhi ni nyenzo kuu ya uchumi;

(iii) Ihakikishe inatoa na kuzitambulisha katika taasisi za fedha hatimiliki za kimila kwa wananchi hasa kundi la vijana vijijini ili ardhi hiyo iweze kuwasaidia katika upatikanaji wa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa utambuzi wa makundi ya vijana katika mnyororo wa ajira nchini, Kamati inashauri Serikali kuwa:

(i) Iandae kanzidata itakayobainisha na kuonesha Idadi ya vijana walio katika ajira rasmi na ambao wamejiari katika sekta binafsi na isiyo rasmi ili kuweza kutambua mchango wa vjiana katika kuchangia pato la Taifa;

(ii) Iendelee kuainisha fursa za ajira katika utumishi wa umma, sekta binafsi ndani na nje ya nchi ili kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa ujenzi wa vituo atamizi *(incubators)* kwa ajili ya kukuza ujuzi kwa vijana. Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Ihakikishe inajenga vituo atamizi *(incubators)* kwa ajili ya kuwajengea vijana ujuzi na ubunifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii kabla ya kupokea mikopo hali itakayowajengea uwezo wa kuzalisha, kulipa mikopo na kutunza akiba;

(ii) Iandae na kuratibu majukwaa yatakayowawezesha vijana kuwa na fikra tunduizi kwa ajili ya kukabiliana na

changamoto ya mabadiliko ya teknolojia na hali ya siasa za ndani na nje ya nchi, ili kuwafanya vijana kuwa walinzi wa kwanza wa amani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ninapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa imani yao kwangu kwa kunichagua kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, napenda kutumia fursa hii kuwaahidi ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu, Pia kwa pekee nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma kwa kushirikiana katika kuongoza Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Wajumbe kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara na uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao ninaomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Joel Nanauka Mbunge, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Jenifa Omolo na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Kedmon Mapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana - Fungu 104 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS MAENDELEO YA VIJANA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana **(Fungu 104**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana ilianzishwa tarehe 19 Disemba, 2025 kupitia Tangazo la Serikali **Na.685**. Awali majukumu yanayotekelezwa na Ofisi hii yalikuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenyeulemavu. Kwa hiyo basi, taarifa hii itahusisha utekelezaji wa majukumu ya iliyokuwa Idara ya Vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, bila kuathiri masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, inayohusu taarifa yoyote ya Kamati

inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (05) kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inahusu Msingi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi na tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027;

(iv) Sehemu ya nne inafafanua Maoni na Ushauri wa Kamati unaotolewa kwa Serikali; na

(v) Sehemu ya tano inahitimisha taarifa ya uchambuzi na kuonesha msimamo wa Kamati.

**1.2 Msingi wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana yanaweka Masharti ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 6 (5)(a) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7 (1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya ofisi hii.

Aidha, Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,**ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na, Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoanishwa katika taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati inahusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana **(Fungu 104)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo: -

(i) Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hizo ilizitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taaarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 25 Machi, 2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu

ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya hatua hiyo, Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;

(ii) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

(iii) Utekelezaji wa Vipaumbele; na

(iv) Hali ya upatikanaji wa Fedha

**2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 09 Aprili, 2025**,** Bunge lilipokea na kujadili taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika mjadala huo, Kamati iliwasilisha oni moja kuhusu utekelezaji wa Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Kamati iliitaka Serikali kupelekea fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kuongeza mtaji na uwezo wa mfuko huo kuhudumia vijana wengi zaidi nchini katika upatikanaji mikopo kupitia mfuko huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitika kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 25 Machi, 2026, Serikali haikuwa imepeleka fedha zozote katika mfuko kama ilivyoidhinishwa na Bunge katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Hali hii inakinzana na nia thabiti ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kushughulikia changamoto za vijana nchini. Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha hizo kwa haraka ili kuiwezesha Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mkoa wa

Tanga. Kamati ilikagua mradi mmoja ambao ni sehemu ya mradi uliotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000/=** Mradi Na. 4952 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyofafanuliwa awali katika taarifa hii, hadi tarehe 25 Machi, 2026, Serikali haikuwa imepeleka fedha kwa ajili ya mradi huo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Mfuko huo ulikuwa na bakaa ya **Shilingi 824,463,770/=** kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana kutoka katika bajeti ya mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia fedha hizo katika Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana umeweza kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi **336,815,000/=** katika mikoa ya Mwanza na Mtwara. Kamati imetarifiwa kuwa Ofisi ya Rais (Fungu 104) ipo katika hatua za mwisho za kutoa mikopo kwa vikundi vinne vya vijana katika mikoa ya Mbeya, Arusha na Rukwa kiasi cha **Shilingi 487,648,770/=.**

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa Bunge lako Tukufu linapata taarifa kuhusu mikopo inayotolewa kupitia Mradi **Na. 4952** Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF), Kamati ilitembelea na kukagua ufanisi wake katika Kikundi cha Mali hai kilichopo Wilaya ya Muheza Mkoa wa Tanga. Kikundi kilianza kikiwa na mtaji wa **Shilingi 100,000/=** iliyotokana na michango ya ada ya kujiunga na unachama wa kikundi. Serikali ilitambua juhudi za kikundi hiki kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kukikopesha mtaji wa **Shilingi 20,000,000/=** katika mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** fedha zimekiwezesha kikundi hiki kuwa na uwezo wa kununua mashine za kuzalisha malighafi za ujenzi kama vile kufyatua tofali, kutengeneza karavati, kuzalisha tofali ndogo maarufu kama paving blocks. Aidha, kikundi hicho kimeweza kuunganisha nishati ya umeme katika eneo la uzalishaji hali inayopunguza gharama za matumizi ya mafuta na kuongeza ufanisi na tija ya mradi.

**Mheshimiwa Spika,** kikundi kimepata mafanikio mengi kwani mtaji wa kikundi kwa sasa umefikia **Shilingi 52,000,000/=** ambao

umewezesha wanachama wa kikundi kuweza kulipwa **Shilingi 200,000/=** kila mwezi. Aidha, kikundi hiki kimeongeza ajira mpya zaidi ya 20 na kusaidia kukuza ujuzi  kwa vijana 50.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Serikali kwa kutambua mchango wa vijana na kuja na Mradi huu unaowezesha vijana kupata mitaji. Aidha, Kamati inawapongoza wanachama wa Kikundi cha Malihai katika kutunza mtaji na kuendelea kuwa kikundi cha mfano kwa vijana nchini. Kamati inatoa wito wa vijana kujitokeza na kuunda vikundi vya uzalishaji mali ili wapate fursa ya kukopa na kujikwamua kiuchumi. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Maendeleo ya Vijana nchini.

**2.3 Majukumu yaliyotekelezwa na Ofisi ya Rais -Maendeleo ya Vijana hadi Machi, 2026**

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa Ofisi ya Rais- Maendeleo ya Vijana imefanikiwa kutekeleza majukumu mblimabli kama ifuatavyo:-

i) Kuimarisha Ushirikishwaji na Usikilizaji wa Kero za Vijana;

ii) Kukuza Majadiliano ya Kitaifa Kupitia Kongamano la Wajasiriamali na Bodaboda;

iii) Kuongeza Ushiriki na Ushirikishwaji wa Vijana kupitia Jukwaa la Vijana (Vijana Platform);

iv) Kuboresha Mwongozo wa Kitaifa wa fursa za uwezeshaji kiuchumi ndani na nje ya nchi; na

v) Kuboresha Mwongozo wa Kitaifa wa mafunzo ya stadi za maisha.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Vipaumbele vya Ofisi ya Rais- Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) imepanga kuwa na vipaumbele vinne mahususi kama ifuatavyo:-

(i) Uratibu na Uhamasishaji wa Vijana;

(ii) Kutoa elimu ya Uraia, Uzalendo na Uratibu wa Mwenge wa Uhuru;

(iii) Ukuzaji wa Biashara na uwezeshaji wa Vijana kiuchumi; na

(iv) Ustawi wa Makuzi kwa Vijana

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza vipaumbele hivyo, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana itatekeleza shughuli mbalimbali. Na baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na:-

(i) Kuratibu mapitio ya Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa Sura 441;

(ii) Kuboresha mwongozo wa Kitaifa wa fursa za uwezeshaji kiuchumi ndani na nje ya nchi;

(iii) Kuboresha mwongozo wa Kitaifa wa mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana nchini; na

(iv) Kufanya tathmini na kutoa elimu ya uraia na uzalendo kwa vijana ili kujenga kizazi kinachojua haki na wajibu wao kwa Taifa.

### 3.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza mpango na vipaumbele vyake katika mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana **(Fungu 104**) inakadiria kutumia **Shilingi 30,104,264,000/=** kwa ajili ya mishahara na Matumizi Mengineyo (OC). Katika fedha hizi, Mshahara ni **Shilingi 1,227,961,000/=** na Matumizi Mengineyo ni Shilingi **28,876,303,000/=.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kamati umebaini kuwa makadirio ya matumizi mengineyo ni makubwa kwa sababu Ofisi hii ni mpya na itakuwa na shughuli nyingi za usimamizi na uratibu.

**Kielelezo Na.1: Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa Fungu 104**

| AINA YA MATUMIZI | MWAKA 2026/2027 | ASILIMIA |
|---|---|---|
| Mshahara | 1,227,961,000 | 4.08 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 28,876,303,000 | 95.92 |
| **JUMLA KUU** | **30,104,264,000** | **100** |

**Chanzo**:Randama ya Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana 2026 ya Usanifu wa Kamati

### 3.3 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa **Fungu 104** inakadiriwa kutumia kiasi cha Shilingi **5,853,034,000/=** kwa mwaka **wa fedha 2026/2027** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Aidha, **Shilingi 5,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 853,034,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais-Maendeleo ya Vijana kwa kuweka juhudi za kutenga Fedha za ndani kwa **asilimia 85.4** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo. Hali hii inaonesha dhamira ya dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita kushughulikia changamoto za vijana nchini**.**

**Kielelezo Na.2 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Fungu 104**

| Aina ya Matumizi | Fedha zilipotengwa | Mwaka 2026/2027 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Miradi ya Maendeleo | Fedha za Ndani | 5,000,000,000 | 85.4 |
| | Fedha za Nje | 853,034,000 | 14.6 |
| **Jumla kuu** | | **5,853,034,000** | **100** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais ya Usanifu wa Kamati

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Sp ika,** baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais -Maendeleo na Vijana,sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa kamati kama ifuatavyo:-

### 4.1 Maoni ya Jumla

(i) Serikali iendelee kutengeneza Fursa kwa Vijana kupata elimu na ujuzi ambao utawawezesha katika kushindana kwenye soko la ajira ili waweze kujitengemea; na

(ii) Serikali ihakikishe kuwa inasimamia na kutekeleza majukumu yote yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha unaoisha

### 4.2 Maoni Mahsusi

a) Changamoto ya Fedha za Miradi ya Maendeleo Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i) Ihakikishe inatoa fedha za Miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge;

ii) Iweke mikakati ya kutangaza fursa za mikopo kwa Vijana kupitia vipindi vya radio, runinga na mitandao ya kijamii ili kuwafikia vijana wengi nchini.

b) Changamoto ya upatikanaji wa Ardhi katika shughuli za Kiuchumi kwa vijana.

**Kamati inaishauri Serikali kuwa:-**

i) Ihakikishe kuwa Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Wizara ya Ardhi zishirikiane katika kutambua mahitaji ya vikundi vya vijana na kuvipatia nafasi ya umiliki wa Ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji na uwekezaji katika viwanda vidogo;

ii) Itoe elimu kwa wananchi hususani kundi la vijana kuhusu umuhimu wa kumiliki ardhi kwani ardhi ni nyenzo kuu ya uchumi;

iii) Ihakikishe inatoa na kuzitambulisha katika taasisi za fedha hatimiliki za kimila kwa wananchi hasa kundi la vijana vijijini ili ardhi hiyo iweze kuwasaidia katika upatikanaji wa mitaji.

c) Utambuzi wa Makundi ya Vijana katika Mnyororo wa Ajira Nchini.

**Kamati inaishauri Serikali kuwa:-**

(i) Iandae kanzidata itakayobainisha na kuonesha Idadi ya vijana walio katika ajira rasmi na ambao wamejiari katika sekta binafsi na isiyo rasmi ili kuweza kutambua mchango wa vjiana katika kuchangia pato la Taifa;

(ii) Iendelee kuanisha fursa za ajira katika utumishi wa umma na sekta binafsi ndani na nje ya nchi ili kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini.

d) Ujenzi wa Vituo Atamizi (Incubators) kwa ajili ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana.

**Kamati inaishauri Serikali kuwa:-**

(i) Ihakikishe inajenga vituo atamizi (incubators) kwa ajili ya kuwajengea vijana ujuzi na ubunifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii kabla ya kupokea mikopo hali itakayowajengea uwezo wa kuzalisha, kulipa mikopo na kutunza akiba; na

(ii) Iandae na kuratibu majukwaa yatakayowawezesha vijana kuwa na fikra tunduizi kwa ajili ya kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya teknolojia na hali ya siasa za ndani na nje ya nchi ili kuwafanya vijana kuwa walinzi wa kwanza wa amani katika Taifa letu

**SEHEMU YA TANO**

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa Imani yao kwangu kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, napenda kutumia fursa hii kuwaahidi ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu.

**Mheshimiwa Spika,** ninawashukuru Wajumbe kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara na uchambuzi wa Bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa taarifa hii, hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard) majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe.Hawa Chakoma Mchafu, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Dkt. Regina Christopher Malima, - **M/Mwenyeiti**
3. Mhe.Mohamed Abrahman Mwinyi, Mb- Mjumbe
4. Mhe.Mariam Nassoro Kisangi, Mb - Mjumbe

5. Mhe.Tinnar Andrew Chenge, - Mjumbe
6. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb - Mjumbe
7. Mhe.Said Ibrahim Mzimba, Mb - Mjumbe
8. Mhe.Lucy Similya Kombani, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Nasriya Nassir Ali, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Shadya Haji Omary, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mohamed Kassim Salum, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Athumin Omary Mapalilo, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Pascal Lucas Lutandula, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Kafiti William Kafiti, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Edefonce Joachim Canoni, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Happiness Daniel Ngwando, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Joel Arthur Nanauka Mb, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Bi. Jenifa C. Omolo na Naibu Katibu Mkuu, Dr. Kedmon E.Mapana .

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana (Fungu 104) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja**.**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Hawa Chakoma Mchafu, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
20 Aprili, 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshapokea taarifa zote mbili kutoka kwenye Wizara na kutoka kwenye Kamati, sasa tunaanza na uchangiaji. Tunaanza na Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mheshimiwa Zainabu Abdallah Issa na Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, ajiandae.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujaalia afya njema na kuwa pamoja hai katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee sana kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Ilemela kwa kuendelea kuniamini, nami kama kijana ninawaahidi kuendelea kuchapa kazi ndani ya Bunge na nje ya Bunge, kwa maana hiyo niwahakikishie kwamba wana jembe, mimi ni mtu wa vitendo na siyo mtu wa maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tena nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwaamini vijana katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa. Ndugu zangu ninaomba tu niwajulishe kwamba dhamira ya Rais katika kuhakikisha inawainua vijana kiuchumi imeendelea kudhihirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa, Taifa lolote ili liweze kuendelea linahitaji nguvu ya vijana, kwa hiyo vijana pamoja na kuwa nguvu kazi, tunaamini

vijana ni mtaji na si *liability* katika Taifa letu. Dira yetu ya 2050 inahitaji kuwaongezea ujuzi na uimara vijana wote katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, kama Serikali na kama nchi kwa ujumla tunashukuru sana kwa kuendelea kuwaamini vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza sana Rais hata ukiangalia Bunge hili, wengi asilimia kubwa ni vijana. Kwa maana hiyo Taifa hili sasa linaongozwa na vijana na vijana tuliomo katika Bunge hili hatuna budi kuhakikisha tunawasimamia vijana wenzetu ili waweze kujikwamua kiuchumi. Vijana tumekuwa tukilalamika kuomba nafasi na kupewa nafasi za uwakilishi. Sasa nafasi tumepewa, ni jukumu letu ni kuhakikisha tunaonyesha njia kwa vijana wenzetu kwa kuleta maendeleo thabiti katika Taifa letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze sana Waziri, kaka yangu Joel Nanauka. Rais hakukosea ametuleta Rais kijana, mzalendo, mchapakazi, muadilifu, mwenye hofu ya Mungu, tunamwamini na vijana tuko nyuma yake. Nasi tutampa ushirikiano wa kudumu na kuhakikisha yale matamanio ya Rais, matamanio ya Serikali, matamanio ya vijana wa nchi hii yanakwenda kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niongelee sasa mambo matatu leo nitaenda kusisitiza. Awali ya yote kwa sababu Rais amekuwa na nia thabiti ya kuwainua vijana. Wakati anafanya kampeni aliahidi kutoa zaidi ya bilioni 200 kwa vjijana wetu na bilioni 200 hizo zimeshaanza kutoka. Kwa hiyo, ndugu zangu ninaomba niwahakikishie kwamba vijana wote pesa hizi zilizotoka ni kwa ajili ya vijana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizi zilizotoka haziangalii itikadi ya chama, dini wala kabila, vijana wote wenye sifa watakwenda kukopeshwa pesa hizi. Nami nimhakikishie Waziri, vijana tuko nyuma yake kuhakikisha hizi bilioni 200, ambazo Serikali imetenga, ambazo Rais amezielekeza kwa vijana, basi zinakwenda kufanya kazi ya kuwainua vijana mbalimbali kwenye Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa kuendelea kutimiza ahadi yake, leo Wizara ya Vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, tumeahidiwa kupata zaidi ya bilioni nane na mpaka saa hizi zaidi ya bilioni 2.5 zimeshatolewa kwa Wizara hii, pongezi kubwa kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo bado tunaamini hizi bilioni 200 bado zinahitaji kusimamiwa na Wizara hii ya Vijana. Tunafahamu pesa nyingi zimeweza kupelekwa katika Wizara Mtambuka, Wizara za Kisekta ili kuweza kukamilisha mahitaji kwa vijana. Tumeona kwamba kwa wale ambao vijana wana-*deal* na kilimo, pesa zao ziko Wizara ya Kilimo, wanao-*deal* na madini ziko Wizara ya Madini na sekta nyingine, lakini ninaomba tuwahakikishie kwamba vijana tutaendelea kutumia hii fursa na tuendelee kuitumia hii fursa kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kumekuwa na malalamiko pesa hizi hazitoki kwa wakati, kumekuwa na malalamiko vijana hawapati pesa hizi lakini pesa hizi zimekuwa zikitoka japo ninaweza nikasema kwamba bado Serikali inatakiwa iongeze pesa hizi ili kila kijana aweze kunufaika na mikopo hii na pesa ambazo zimetolewa na Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuchangia Wizara hii, vijana tunajukumu kubwa la kuhakikisha ajenda ya maendeleo na dira yetu ya 2050 tunakwenda kuitekeleza. Ukiangalia hata sensa za 2022 vijana ndiyo asilimia kubwa zaidi ya 60%, Maana yake nini? Dira hii ya 2050 bila kuwaimarisha vijana haitoweza kutekelezeka. Nasi vijana ndiyo lazima tuchukue msingi huu, ni lazima tusimame pamoja kuhakikisha dira hii tunakwenda kuitimiza kwa wivu mkubwa, kuhakikisha kila kijana ananufaika na pesa hizi ambazo Rais amezitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niendelee kuipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga pesa kwa ajili ya maendeleo ya vijana, kupitia Wizara hii zaidi ya bilioni tano zimetengwa kwa ajili ya maendeleo ya vijana. Kupanga ni jambo moja na utekelezaji ni jambo lingine. Katika miaka minne iliyopita kabla ya Wizara hii haijaanzishwa, Wizara hii ilikuwa inatengewa bilioni moja wakati ule ni Wizara ya Ajira, Kazi na Vijana, sasa hii

Wizara inajitegemea, tunaomba hii bilioni tano kwa ajili ya maendeleo ya vijana iweze kutengwa na iweze kutolewa kwa wakati ili iweze kunufaisha vijana wetu. Kwa hiyo, katika eneo hilo ninaomba tuendelee kuiomba sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie wasaa huu vilevile kuomba sana vile Vyuo vya Maendeleo ya Vijana kwa maana Chuo chetu cha Morogoro cha Ilonga pamoja na Chuo chetu cha Songwe, Sasanda, Serikali iendelee kutoa pesa zaidi ya bilioni mbili zimeidhinishwa, sasa ninaiomba sana Serikali kuanzishwa kwa mafunzo haya ya muda mfupi yatakwenda kunufaisha vijana wengi katika maeneo ya kilimo, katika maeneo ya ujasiriamali, katika maeneo ya uzalendo kuhakikisha kila kijana ananufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine niombe tu kitu kimoja kwamba Serikali sasa ije na mpango wa kuwaandaa vijana wake, na hili nimekuwa nikichangia na nimekuwa nikiongea na Waziri wa Mipango, kwamba sasa ifikie wakati Serikali lazima ije na mpango wa kuhakikisha inawatoa vijana wake kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Mfano, vijana leo wa *Form Four* wakimaliza wale ambao hawajafanikiwa kufaulu wanakwenda wapi? Vijana wa *Form Six* ambao hawakufaulu wanakwenda wapi? Vijana wanaomaliza Chuo Kikuu nini mpango wa Serikali kuhakikisha unawainua kiuchumi vijana hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali ije na mpango huu, dira yetu ya 2050 itakwenda kutekelezeka kwa sababu tutajua mahitaji ya vijana hawa. Leo tumetoa bilioni 200 hatujafanya *research* je, ni vijana wangapi watakwenda kunufaika na kiwango hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine labda kwa kumalizia kwa sababu tuko kwenye Wizara *hot* ya vijana na wanatusikiliza nitaomba muda wako kidogo na mimi kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati hii vijana ndiyo kimbilio letu, kwa hiyo uniwie radhi kidogo tuna madini mazuri ya kuwaona kwamba vijana wengi wanakwenda kunufaika na Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kilimo kupitia *BBT* tuendelee kuweka msisitizo, vijana wengi watakwenda kuajiriwa hapa. Tunafahamu tuna vijana wanatoka *SUA*, ni ajabu kumwona *graduate* wa *SUA* anakwenda kutafuta kazi wakati kuna nguvu kazi Serikali inaweza ikatoa mitaji na vijana hawa wakaenda kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana wanaomaliza mikataba JKT wakimaliza wanarudi mtaani, kwa nini tusiwaanzishie mashamba ya wao kujiajiri na kuweza kuchangia pato la Taifa? Kwa hiyo, tunafahamu tuna uhaba wa sukari, vijana waende tuwaanzishie mashamba na mitaji waende wakalime. Tunayo mahitaji ya alizeti, kwa maana ya kilimo kama nchi tuna mahitaji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa kumalizia tunapotoa bajeti hii ni lazima Serikali sasa ije na mpango kuhakikisha pesa zinazotoka zimekwenda kufanya nini? Zimesaidia vijana wangapi? Tuimarishe vitengo vya *monitoring and evaluation* ili kuona tija ya pesa hizi zinapotoka kweli zionekane zinawanufaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niombe Wizara hii imeanzishwa ni Wizara mpya, tunao vijana ambao walikuwa chini ya maendeleo ya jamii kule kwenye Halmashauri. Sasa tuombe watoke kule warudi kwenye Wizara yao ya Vijana kwa sababu sasa Wizara ya Vijana iko kamili na inaendelea na shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja, vijana tukae mkao wa kula, sasa ni wakati wetu wa kuleta maendeleo kwa nchi yetu. Asanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kafiti. Waheshimiwa Wabunge kabla sijaendelea kumtaja Mbunge anayefuata, ninaomba niwatambue na kuwatangaza wageni ambao wapo muda huu katika Bunge letu.

Wageni wa Mheshimiwa Joel Arthur Nanauka, Mbunge na Waziri wa Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, hawa ni viongozi wa siasa kutoka Wilaya ya Mtwara Mjini. Karibuni. *(Makofi)*

Kuna, wataalam kutoka Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana), pia tuna mwakilishi kutoka *UNICEF, UNFPA* na *UNDP*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wafanyakazi wa Benki ya *NMB,* karibuni sana.

Wapo wageni kutoka Dodoma *Youth Development Organization*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni kutoka *The African Leadership Initiative for Impact,* wengine ni *Restless Development* Tanzania, tunao *Emerging Generation Initiative,* tunao *Manara Foundation* na *GP Foundation,* na pia wapo hapa wanufaika wa mikopo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tunao wawakilishi wa vijana kutoka asasi za vijana na vyuo vikuu, Chuo cha Mipango na *St.* John. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao ndugu, jamaa na marafiki wa Mheshimiwa Nanauka. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo msaidizi wa nyumbani wa Mheshimiwa Waziri. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wamekuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kwanza ni wageni 30 kutoka Taasisi ya Vijana Tanzania *Next Gen Leadership* kutoka Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu kutoka Taasisi ya Tanzania *Next Gen* na karibuni wageni wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninasisitiza kuwa michango ielekezwe kwenye hotuba na muda. Ikishagonga kengele ya pili naomba tuwape fursa wengine waweze kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa atuatiwa na Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni. Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa.

**MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana. Leo nimesimama hapa kuwasilisha sauti za vijana wote wa Kitanzania, vijana wanaotaka mabadiliko ya kweli. Hatma ya Taifa hili iko mikononi mwetu sisi vijana, na hii ni kwa sababu zaidi ya 76% ya nguvu kazi ya Taifa hili ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninukuu kauli ya Nelson Mandela ambaye aliwahi kusema, *"The development of any nation cannot prosper if the generation of young people is left behind."* Maendeleo ya nchi yoyote hayawezi kupiga hatua kama kundi kubwa la vijana litaachwa nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza, kwa mapenzi makubwa aliyokuwa nayo kwa vijana wa Taifa hili na kwa kuona umuhimu kwenye historia ya nchi hii kwa mara ya kwanza kuanzisha Wizara mahususi inayohusu maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameenda mbali zaidi kwa kutoa fedha shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwawezesha vijana kiuchumi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Kwa niaba ya vijana wenzangu, tunataka kumhakikishia kwamba, sisi vijana hatutamwangusha. Tunatambua kwamba tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa tunalinda amani na utulivu wa Taifa letu ili nchi yetu iweze kupiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini, kama ambavyo nchi yetu imerithishwa hivi leo ikiwa kwenye mikono salama, sisi vijana tuna wajibu wa kuhakikisha tunaendeleza amani na utulivu wa Taifa hili ili nchi hii iendelee kubaki kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza sana Waziri wetu wa vijana Mheshimiwa Joel Nanauka, pamoja na menejimenti nzima ya Wizara, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo

wanaendelea kuifanya, na kwa ubunifu mkubwa ambao wameuonesha ndani ya muda mfupi tangu wamekabidhiwa jukumu hili na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi vijana tumeona uanzishwaji wa *Vijana Platform, platform* ambayo yeye binafsi, Mheshimiwa Waziri amezunguka mkoa kwa mkoa kwenda kusikiliza na kutatua kero za vijana. Pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza kwa kuanzisha vijana *call centre,* mfumo ambao unatoa uhuru wa vijana kuwasiliana moja kwa moja na watendaji wa Wizara, ikiwemo Mheshimiwa Waziri. Hili ni jambo la kupongezwa na la kuungwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza kwa kuja na *Vijana Uchumi Challenge* kwa ajili ya kuibua vipaji vya vijana wenye mawazo kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ushauri wangu kwenye Wizara hii, moja, kwa kuwa tuko katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, na kwa kuwa malengo ya dira hii ni kwamba tuhakikishe sekta binafsi inachangia 70% ya uchumi wa Taifa letu, na kwa kuwa nguvu kazi ya Taifa hili ni 76% ambayo kundi kubwa ni vijana, ipo haja ya Serikali kuanza kupitia upya sheria, sera, na kanuni zetu ili kuhakikisha zinafungamanishwa na ushiriki wa sekta binafsi, pia kuhakikisha kuwa vijana wanapewa nafasi na kwamba wanatambulika katika kushiriki kwenye marekebisho ya sera, kanuni pamoja na sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo tuna Sheria ya *Public Private Partnership* ya Mwaka 2023, lakini ukiitazama ile *PPP Act* na ukija kutazama Sheria ya *Procurement Act* unaona kabisa hatuwezi kufungamanisha vitu hivi viwili na tukapata tija kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia *PPP Act* inatoa fursa kwa mwekezaji mwenye wazo la kuendeleza miradi kupata hiyo fursa ya kuweza kuendeleza miradi, lakini ukija kwenye *Procurement Act* inataka utaratibu na mmlolongo mzima wa Serikali uweze kufuatwa ili mtu aweze kupatikana wa kufanya shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta *Procurement Act* mchakato unaweza kuchukua zaidi ya siku 90, lakini mbaya zaidi waombaji wanakuwa wengi pengine hata yule ambaye alikuja na lile wazo asibahatike kuweza kushiriki kufanya lile wazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya sheria zetu kufanyiwa mapitio, na sheria ambazo zimekaa kwa zaidi ya miaka 10 zifanyiwe maboresho ili ziendane na masuala ya *Public Private Partnership* pamoja na ushirikishaji wa vijana. Hili ni jambo kubwa na ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, sasa hivi tuna Wizara hii, lakini tunahitaji *instruments* za kuweza kuisimamia Wizara hii. Leo hii maafisa vijana wapo chini ya halmashauri chini ya Afisa Maendeleo ya Jamii. Ipo haja ya maafisa vijana kwenye halmashauri waripoti moja kwa moja Wizara ya vijana ili waweze kuwa na dhana ya uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mabadiliko hayo yamefanyika kwenye Wizara mbalimbali wakati halmashauri kipindi cha nyuma maafisa hawa, ma-*engineer* wa maji walikuwa chini ya halmashauri, lakini sasa hivi hawa Wakurugenzi, Maafisa wa Idara ya Maji wanaripoti moja kwa moja Wizara ya Maji na wanajibishwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawa maafisa wa vijana hawatakuwa chini ya Wizara ya Mheshimiwa Waziri, ni ngumu sana kuwawajibisha kwa sababu watakuwa chini ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maafisa vijana ambao ni wazee, uwezo wao wa kufanya kazi ni mdogo, uwezo wao wa kubuni ni mdogo. Hili jambo la kuwa na watendaji wanaoendana

na kasi ya vijana ni muhimu sana kuzingatiwa katika kuwapata hawa watendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa hivi tuna Sera ya Maendeleo ya Vijana ambayo imekuwa *reviewed* 2024. Pia tuna mkakati wa utekelezaji wa sera hii wa miaka kumi, 2024 hadi 2034, lakini hatuna mpango kazi wa muda mfupi na muda mrefu ambao utatupatia majibu, mpango kazi kuhusiana na umuhimu wa kupata masoko ya uhakika kwa vijana, mpango kazi utakaoonyesha mkakati wa kupata elimu ya ujuzi kwa vijana, mpango kazi utakaoonyesha miundombinu wezeshi kwa ajili ya kukuza ujasiriamali na uwekezaji, mpango kazi ambao utaonyesha ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ipo haja ya kuwa na mpango kazi ambao utatupa *direction* kwa ndani ya miaka hii 10, nini tunaenda kukifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni hili la benki ya vijana. Ninapongeza kwa kuwa na wazo hili na kuanza kulichakata. Ipo haja ya kuwa na benki ya maendeleo ya vijana. Kama tumeweza kuwa na Benki ya Maendeleo ya ya Kilimo tunashindwaje kuwa na benki ya maendeleo ya vijana ilhali 76% ya nguvu kazi ya Taifa hili ni vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna programu na mifuko 74 ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, lakini pengine vijana wanafahamu mifuko miwili tu. Wanafahamu mfuko wa 10% na wanafahamu na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, lakini leo tuna mfuko wa *Small and Medium Enterprises Fund,* tuna Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali, tuna Mfuko wa Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, tuna mifuko 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani mifuko hii iratibiwe na benki ya maendeleo ya vijana ili vijana sehemu zote ndani ya nchi yetu waweze kupata fursa ya mitaji kwa sababu changamoto kubwa ya vijana ni suala zima la mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa 10% kipindi cha nyuma mchakato ulikuwa unawa-*favour* baadhi ya watu na

kuwanyima baadhi ya watu nafasi. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alisimamisha mchakato huu, na baadhi ya maeneo sasa hivi *pilot* imefanyika kwa ajili ya hizi fedha za 10% kupitia benki zetu. Hata hivyo taarifa iliyopo benki nyingi mpaka sasa hawajatoa fedha hizi za 10% kwa vijana, lakini pia kuna urasimu mkubwa wa utolewaji wa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tangu maelekezo yametoka ni takribani mwaka mmoja sasa hivi. Tunatamani tupate tathmini ya uhakika, je, kupitia mfumo huu wa benki *pilot study* inakuja na majibu gani? Kuna haja ya kuendeleanao au hatuna haja ya kuendeleanao ili vijana huko kwenye halmashauri zetu waweze kupata fedha hizi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, ninataka niwaambie vijana wenzangu, tumekuwa na ulalamikaji kwamba hatushikwi mikono. Serikali imeanza kutushika mikono, tuache kulalamika vijana wenzangu, tutumie fursa hizi zilizopo ili tuweze kujikwamua kiuchumi. Tanzania itajengwa na sisi sote, tushikamane kwa pamoja kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Abdallah.

Waheshimiwa Wabunge, ninajua tuna michango mingi kwenye sekta hii ya vijana, na wachangiaji ni wengi na ninatamani wote waweze kupata fursa. Kwa hiyo, kutokana na wachangiaji kuwa wengi, tunakwenda kwa dakika nane, na ninawaomba sana mwende kwenye agenda mnayoona hii ni muhimu sana kuliko zote ili tuweze kupata fursa kuchangia wengi. Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni atafuatiwa na Mheshimiwa Latifa Juwakali.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi siku ya leo. Pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Pia, ninakishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi Wilaya ya Kalambo na viongozi wote wa Chama cha CCM Mkoa, bila kuwasahau wananchi wangu wa Wilaya ya Kalambo ambao walinipa kura za kutosha ili niweze kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake makubwa kwa kuunda Wizara ya Vijana kwa ajili ya kuwakilisha vijana, na hasa kwa kumpata Mheshimiwa Waziri kijana ambaye ana maono makubwa kwa ajili ya kuwakilisha vijana katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza kwenye mikopo. Mheshimiwa Rais amekuwa na maono makubwa kuhakikisha anawakwamua vijana kiuchumi, na hususan ukizingatia kuwa vijana ni wengi, ambao wako 76%, katika Taifa letu. Takwimu zinaonesha kuwa vijana wanaohitimu elimu ya vyuo vikuu ni kati ya vijana 500,000 mpaka 600,000 kwa mwaka. Tathmini katika miaka mitano mpaka miaka kumi tutakuwa na vijana karibu 7,000 mpaka 8,000 ambao watakuwa wamehitimu elimu mbalimbali katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa kulizingatia hilo, na kwa kuwa na maono makubwa, akaweka mpango wa kuunda Wizara ya vijana na kuweka fedha kwa ajili ya kuwasaidia vijana. Hili ni jambo kubwa sana ambalo linatakiwa kuungwa mkono kwa nguvu zote kwa maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha, shilingi bilioni 200 zimegawanyika katika Wizara za kisekta. Wazo langu, ninaishauri Serikali, fedha hizi zirudi katika sekta ya vijana ili vijana wawe wanajua kwamba fedha zetu ziko Ofisi ya Rais (Maendeleo ya

Vijana). Zimeenda kilimo, zimeenda uvuvi, na zimeenda maendeleo ya jamii, zirudi kwa vijana ili Mheshimiwa Waziri awe anazisimamia mwenyewe. Sasa kama vijana wanaenda huku wanaambiwa rudi huku, hii haitaweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, nina imani sana Mheshimiwa Nanauka. Hawa vijana wana shida ya kuwa matajiri na Mheshimiwa Rais ndoto yake ni kutengeneza vijana wengi kuwa matajiri...

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanon kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Kanoni, kwamba hata hizi Wizara mbili zilipotoa matangazo ya mikopo kwa vijana, Wizara ya vijana walisema kijana aje na andiko lisilozidi kurasa tano, halafu Wizara ya Mifugo na Uvuvi ikasema kijana aje na andiko lisilozidi kurasa mbili. Utaona hata Wizara hizi zinapokuwa nyingi zinawachanganya vijana. Kwa hiyo, anachosema ni sahihi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanoni, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa kwa mikono miwili. Ninasema hivyo kwa sababu gani? Mheshimiwa Rais ana malengo makubwa juu ya vijana wetu, na sisi kama Wabunge tunahitaji kuona vijana wanafanikiwa, na vijana wawe tayari kupokea mkopo kwa sababu hakuna mtu anayependa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vijana wanamaliza vyuo vikuu halafu wanabaki, mimi mwenyewe ni mzazi ninaangalia, kama Mheshimiwa Rais anajitoa kutoa fedha kwa ajili ya kuwainua vijana kiuchumi, Serikali isisite kutoa fedha kwa ajili ya kwenda kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanafuata hizi fedha kwenda kukopa, lakini masharti yanakuwa ni mengi. Tangazo la Serikali linasema Mheshimiwa Rais ametoa fedha kuwawezesha vijana kiuchumi. Wakienda benki wanakuta kuna masharti. Unamwambia kijana aliyetoka Chuo Kikuu aonyeshe biashara, ataonyesha biashara gani ambayo ameanzisha? Sasa hii inasababisha hizi fedha kukwama na hazitoki kama tunavyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama zinabaki benki, ni kwa manufaa ya nani? Sheria zibadilishwe, usimamizi ubadilishwe, na masharti yapungue. Kama ni dhamana, Wabunge tupo, Madiwani wapo, Wenyeviti wa Serikali wapo, na wa vitongoji wapo. Masharti yawe nafuu, wakopeshwe vijana ili waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatokea Kalambo. Vijana zaidi ya 1,500 hawana kazi, lakini wana imani kubwa sana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba hizi fedha zitawafikia na wao watanufaika kiuchumi. Hata hivyo, wanalalamika wakienda sekta ya benki wanakuta kuna masharti, wanaomba fedha mpaka miezi mitatu wanakata tamaa. Masharti yabadilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kutengeneza vijana wa dira ya miaka 25. Tunawatengeneza vipi kama hatuwezi kuwapa fursa za fedha? Wape imani hawa vijana. Uwezo wa kufanya kazi wanao. Serikali iwape imani, kusiwe na mashaka, na kusiwe na kigugumizi katika kuwapa fedha, watafanya mageuzi makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna lengo la miaka mitano miaka 20, au 25, hatuwezi kwenda bila hawa vijana. Uchumi wa nchi na uchumi wa dunia unaendeshwa na sekta binafsi. Sasa kama ni sekta binafsi, halafu mikopo inatoka kwa kusuasua, unategemea kitu gani kitatokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mashaka na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Nanauka. Asimamie, na sisi kama Wabunge tupaze sauti hizi, fedha zirudi katika Wizara yenye dhamana na vijana ili waweze kuzisimamia wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka ukanda wa kule Ziwa Tanganyika. Wale vijana wavuvi unamwambia aweke dhamana, anaweka dhamana gani? Wale vijana wengine ambao hawana shughuli, wako mtaani wataweka dhamana gani? Kwa hiyo, Serikali iamue namna ya kupunguza masharti ili vijana waweze kunufaika. Wako hapo wanasikiliza tunavyowasilisha hoja zao. Wananajaza fomu za maombi ya mikopo labda vijana 100 au 50, wanapata watu wachache kwa sababu ya masharti. Masharti yapungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, vikundi ambavyo vinasemwa, masharti ya kuunda vikundi siyo lazima. Ikiwezekana, kama kuna utaratibu, sheria zibadilishwe ili aweze kukopa mtu mmoja mmoja, kwa sababu kuna watu wanaingia kwenye vikundi na hawataki, na hawana sifa. Sasa analazimika kuingia kwenye kikundi, anakopa fedha, na mwisho marejesho yanakuwa yanakuwa ni ya shida...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Latifa Juwakali, Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma ajiandae.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niwe miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii ya Ofisi ya Rais, (Maendeleo ya Vijana).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu kwa uwasilishaji mzuri, na kwa kweli hotuba iliyowasilishwa hapa inaendelea kuonesha dira na matumaini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umaalum sana, kwa dhati ya moyo wangu, ninaomba nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono na mapenzi, lakini kiukweli Mheshimiwa Rais anawapenda sana vijana wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais mapenzi yake ameyadhihirisha katika nyanja mbalimbali, lakini kubwa zaidi ya yote kwa kutuletea hii Wizara ya Vijana. Ameenda kuwagusa vijana wa nchi hii na kuona kwamba changamoto za vijana sasa zinaenda kuwa historia katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, ninaomba nitoe rai. Mheshimiwa Waziri imani aliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kubwa na sisi wasaidizi wa vijana wa nchi hii tunamtegemea sana. Ninataka nimwambie, ameanza vizuri, amechaguliwa, unatushirikisha sisi wasemaji wa vijana, tunapanga na tunajadiliana, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutachoka, tutaendelea kuleta maoni ya vijana, tutaishauri Serikali kwa hekima, na pia tutakapoona kuna changamoto kwa maslahi ya vijana, tutaendelea kuzisema ili ziweze kupatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wanasema, kushukuru ni kuomba tena. Kwa niaba ya vijana wa nchi hii, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kututengea na kutupatia zaidi ya shilingi bilioni 200 ili ziweze kuwanufaisha vijana wa nchi hii. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais na tunampongeza kwa ujasiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nilipata nafasi kushuhudia tukio hili ambapo hizi shilingi bilioni 200 zilipotolewa nilikuwepo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, na vijana wamefarijika sana. Kabla sijaelekea kwenye mchango wangu, ninataka nitoe ushauri mdogo kwenye hizi shilingi bilioni 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lililofanywa na Serikali siyo baya, ni jema. Fedha hizi kugawanywa katika Wizara za Kisekta, tunaona kwamba fedha hizi zimekwenda katika Sekta ya Kilimo, Sekta ya Uvuvi, Sekta ya Madini, na Wizara ya Michezo. Tunaishukuru Serikali kwa mgawanyo wa fedha hizi, lakini bado vijana wana maswali wanatuuliza. Hivi ni nani *coordinator* wa hizi fedha? Nani anazisimamia hizi fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Vijana amepewa *mandate* ya kupokea tu, lakini *coordinator* wa hizi fedha ni nani? Sisi tukiwa na maswali yetu tumwulize nani kwenye Wizara za Kisekta? Vijana wakitupigia simu, tunakwenda kwa Waziri wa Vijana; kwa Waziri wa Vijana zime-*shift,* zimekwenda kwenye Wizara za Kisekta. Hatukatai kwamba kwenye Wizara za Kisekta hakuna vijana, wapo, lakini bado Wizara hizi wanatakiwa waanzishe mfumo maalum wa kuwasaidia vijana wetu hasa huku maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, wanatakiwa wapate taarifa za kutosha. Vijana hawana taarifa za kutosha kuhusiana na hii mikopo, lakini hata masharti ambayo yametolewa, sisi sote tunafahamu. Waheshimiwa Wabunge tulipochangia katika Ofisi ya Waziri Mkuu tulisema kwamba katika ngazi za halmashauri watendaji au watumishi wanao-*deal* na masuala ya vijana huko chini hawapo, na mikopo hii baadhi ya hizo Wizara ambao wame-*highlight* tangazo lao, wamesema kwamba matangazo haya yanatoka katika halmashauri. Huko katika halmashauri ni nani ambaye anamfundisha kijana kuandika hilo andiko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vijana wote wana utaalamu wa kuandika maandiko. Tunaomba sana, bado kuna haja ya kutosha ya kuwasaidia vijana. Fedha zilizotoka ni nyingi sana. Mheshimiwa Rais ameshatekeleza ahadi yake, bado tuna nafasi na muda upo, Mheshimiwa Waziri a-*coordinate* na hizi Wizara nyingine ili tuweze kuwasaidia vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana bado wana malalamiko makubwa, na kiukweli wanahaitaji kusaidiwa kwa sababu tusipowasaidia vijana hawa, fedha hizi watazipata *majujarei*.

Fedha hizi lengo lake ni kuwasaidia hata vijana hawa maskini, vijana wa vijijini na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niliombe hilo, nitoe angalizo. Mheshimiwa Waziri tunakuamini na tunatamani hili tuendelee kulisimamia ili vijana wetu waweze kupata matokeo chanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niende kwenye mchango wangu. Wote mtaungana na mimi kwamba zaidi ya 76% ya vijana wa nchi hii ndio wanaojishirikisha katika shughuli za kiuchumi. Kwa mantiki hiyo, hatuwezi kumtenganisha kijana wa Tanzania na Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050, hilo jambo haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunatakiwa tubadilishe *mindset* za vijana. Tuzibadilishe kwa kufanya mambo yafuatayo ili tuweze kuifikia hiyo Dira ya 2050. Wizara ya Vijana lazima tujipambanue, na kujipambanua kwetu sasa tuwaandae vijana ili waweze kupigania fursa ambazo siyo ajira rasmi, kwa sababu sasa hivi ajira zinapotangazwa vijana wanahisi ndiyo kipaumbele, lakini kumbe zipo ajira ambazo siyo rasmi zinazoweza kuwasaidia vijana wa nchi hii, lakini lazima tuweke miundombinu mizuri na rahisi kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii itafanywa na Serikali, lakini pia Mheshimiwa Waziri ndio ambaye tunamtegemea. Jambo la kwanza kwa Mheshimiwa Waziri tunaomba sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, jambo la kwanza na wakati muda umeisha!

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Eeeh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Malizia kidogo.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri tujikite katika mambo makuu manne. Jambo la kwanza, elimu ya ujuzi wa kisasa; jambo la pili, kilimo cha kisasa, tuwawezeshe vijana katika masuala ya kilimo; jambo la tatu, tuzirasimishe sekta ambazo siyo rasmi kuja kuwa sekta rasmi ili kuweza kuwasaidia vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, siyo kwa umuhimu, uwezeshaji wa kiuchumi na ujasiriamali kwa vijana. Hapa ndipo kwenye fursa za vijana, ninaomba sana tuyazingatie haya ili kuweza kuwasaidia vijana wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Latifa, mambo yako mazuri ambayo yamebaki unaweza ukayatuma kwa maandishi. Pia, hata wengine ambao mnaona kwamba haya mengine mtakuwa muda hautoshi kuyatoa, basi mnaweza kuleta kwa maandishi. Mheshimiwa Waziri yuko tayari kupokea hata michango kwa maandishi.

Tunaendelea na Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala ajiandae.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na uhai. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuona ipo haja ya kuanzisha Wizara hii ya Vijana. Nchi hii zaidi ya 70% ni vijana na nikinukuu maandiko ya Biblia kwenye Mithali 20:29 inasema; *"Fahari ya vijana ni nguvu zao."* Pia, inasema; *"uzuri wa wazee ni kichwa chenye mvi."* *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fahari yetu sisi vijana ni nguvu na huwezi ukaendesha Taifa au tukafanya lolote bila kuwa na nguvu. Ikitokea vita kwenye nchi hii tutawahitaji sana vijana ili wawe

mstari wa mbele kulitetea Taifa lao kuhakikisha amani inaendelea kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini wazee pia wana mchango wao, ndiyo maana nimesema kwamba uzuri wa wazee ni kichwa chenye mvi, kwa hiyo, watatusaidia busara na kutu-*control*, kutushauri kuhakikisha mambo yanaenda vizuri, lakini mambo yanayohitaji nguvu na usasa na mambo yale yanayohitaji *innovation* na mambo mengine mapya mengi sana vijana ndiyo wanaokuwa na mawazo chanya kwa kuibua vitu vipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia duniani waliofanya vitu vikubwa, mawazo mengi waliyapata wakiwa vijana. Kwa hiyo, ndiyo maana ninasema kwamba vijana ndio wenye nguvu na ndio tumaini na *engine* ya Taifa letu. Nimeona dira ya vijana, miongoni mwa vitu walivyozungumza kwenye dira yao, wanataka kuwa na Taifa la vijana wenye ujuzi, ufahamu, vijana waliowezeshwa kama walivyotaja pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaangalia kwenye bajeti yao, 14% ndiyo inazungumzia kuhusiana na uwezeshaji wa vijana. 86% kwenye bajeti yao ni matumizi ya kawaida na mishahara. Kwa kweli mimi kwenye hili nimesikitika kidogo. Kama tuna dhamira ya dhati kama Taifa na tunataka Taifa letu liende mbele na lifikie dira 2020 - 2050 sidhani kama hii shilingi bilioni tano inaweza ikaleta mabadiliko ya kutisha kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningetarajia pengine Wizara hii, yale matrilioni tunayoyasoma kwenye Wizara nyingine yangekuwa yako kwenye Wizara ya vijana. Maana tukizungumzia kilimo, tunahitaji vijana waende kule wakalime. Tukizungumzia viwanda, tunahitaji vijana kule waende wakafanye kazi. Sasa, shilingi bilioni tano hizi zinaenda kufanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna shilingi bilioni 200, ninamshukuru Mheshimiwa Rais. Hizi shilingi bilioni 200 zimetengwa kwa ajili ya vijana, na Waziri wetu sisi vijana, yule amekaa pale lakini ukimwuliza hizi fedha ziko wapi? Anakwambia, ziko kwenye

kilimo, ziko sekta ya viwanda na biashara au ziko kule sijui kwenye Wizara ya Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, mifuko yote, fedha zote zinazohusu maendeleo ya vijana ziwe kwenye Wizara husika, ya Vijana. Hata tukija tukimwuliza kwamba hizi fedha zimefanya nini? Awe na majibu kwamba hizi shilingi bilioni 200 zimefanya moja, mbili, tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nizungumzie kwenye ajira. Zaidi ya vijana 700,000 mpaka 900,000 kwa mujibu wa *World Bank,* wana-*graduate* kuingia kwenye soko la ajira. 10% ndiyo vijana wanaoingia kwenye *formal sector,* ila 90% wengine wanazurura kule au wanafanya vitu ambavyo Serikali hatutambui, wanaenda kwenye *informal sector*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, tuwe na mfumo ambao una-*track* vijana wetu. Tuwe na *Youth Tracking System* ambayo itawatambua vijana wetu waliomaliza vyuo, wanaohitimu masomo. Tujue vijana wetu wamehitimu na ujuzi gani? Pia, tujue vijana hawa wanajishughulisha na nini, na wako wapi ili tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninashauri, kwa mfano kwenye *force account*. Mwaka 2025 tulikuwa na miradi zaidi ya 29,000. Miradi hii iko kule kwenye halmashauri na kule ambako wanasimamia mpaka walimu wa shule ya msingi, sekondari, na madaktari, lakini huku tuna vijana ambao hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini miradi hii tusii-*group* vijana hata watano watano basi, tuwape hii miradi ya *force account* waende kule vijijini watekeleze kuliko kumpa Mwalimu ambaye tayari ana ajira, unampa tena akasimamie mradi wa *force account*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tupunguze utangulizi. Tunaendelea na Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka ajiandae.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niwe miongoni mwa vijana watakaoweza kuchangia kwenye hotuba hii ya Mapato na Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kijana, na ninafurahi sana leo hii kupata nafasi niweze kuchangia hotuba hii, kwa sababu kama nisingechangia ningeona kabisa sijitendei haki mimi mwenyewe, na pia siwatendei haki vijana wengi wa Kitanzania waliojenga imani kwa Wabunge vijana tuliomo humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na mapenzi yake ya dhati kabisa ya kutaka kuona vijana wa Kitanzania wanapata maendeleo, na kwa kuanzisha Wizara hii inayohusiana na maendeleo ya vijana na kumteua kaka yangu Mheshimiwa Joel Arthur Nanauka awe Waziri kwenye hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi wangu huo, ninaomba nichangie hoja. Moja ya ajenda ambayo sisi Wabunge hasa wa Chama cha Mapinduzi ilikuwa inatupatia *mileage* kubwa kwa kundi kubwa la vijana ni kuhusiana na ahadi ya Mheshimiwa Rais, tulipokuwa kwenye kampeni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi walikuwa na matumaini makubwa sana kuhusiana na ahadi hii ya Mheshimiwa Rais ya kutoa fedha shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kwenda kusaidia shughuli mbalimbali za kimaendeleo. Imani hiyo ambayo vijana hawa walikuwa nayo walikuwa wanategemea kabisa kwamba hii Wizara sasa inakwenda kutatua changamoto zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza kutoa zile fedha shilingi bilioni 200, tunamshukuru sana kwa kutimiza ahadi yake na tunajua huyu Mheshimiwa Rais ni mtu wa kutimiza ahadi, akiahidi anatekeleza. Hongera sana Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan na vijana wengi tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi fedha kutolewa na kukabidhiwa kwenye hii Wizara husika, bado malalamiko yamezidi kuwa mengi sana kwa vijana wengi. Lazima tuwe wakweli na tuelezane ukweli. Moja ya changamoto ambayo vijana wanalalamika ni urasimu, lakini kitendo cha hizi fedha kugawiwa kwenye Wizara nyingine za kisekta, kumeendelea kurudisha urasimu ambao vijana wengi wamekuwa wakilalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi vijana tulitegemea kwamba fedha hizi zitabaki kwenye Wizara ya Vijana na Waziri wa Vijana ndiye atakuwa na dhamana ya ku-*coordinate* na kusimamia fedha hizi ili kesho na keshokutwa tuweze kumwajibisha, tumwulize fedha hizi zimekwenda wapi, na zimetumikaje? Kwa hiyo, kitendo cha kuzitawanya ama kuzitapanya kwenda kwenye Wizara nyingine, kumeendelea kurudisha urasimu ambao vijana wengi wamekuwa wakipinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko haya hasa vijana wa vijijini, kwa mfano mimi ninatoka Jimbo la Ndanda. Vijana wa Msikisi, Mnawatutwe, na Chiwale wanalalamika kuhusiana na hizi fedha za shilingi bilioni 200 kwamba, kwanza hawana taarifa, lakini pia hawajui mchakato mzima wa hizi fedha wanazipataje? Hii inapelekea hali ya idadi ya vijana walioomba hii mikopo kuwa ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu, idadi ya vijana walioomba fedha hizi za shilingi bilioni 200 ni vijana 30,384. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi vijana ambao walilengwa kwenye hii mikopo wa kuanzia umri wa miaka 15 hadi miaka 35 wanakadiriwa kuwa milioni 21 mpaka milioni 20. Sasa, hii idadi ya vijana 30,384 ni sawa na 0.12%, yaani hatujafikia hata asilimia moja ya vijana ambao walilengwa kwenda kupata hii mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa hapa tumefeli, na lazima tukubali kwamba tumefeli, kwa sababu, lengo lilikuwa ni kuwafikia vijana wengi, lakini vijana walioomba ni wachache. Ile

nguvu tuliyoitumia katika kuitangaza hii mikopo kwenye majimbo yetu hatujaitumia hii nguvu kuwafikia na kuwapa taarifa vijana wengi hasa wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali, kama kweli tuna dhamira ya dhati ya kutaka kuwasaidia vijana wa Kitanzania kwenye hizi fedha za shilingi bilioni 200, kwanza, Wizara ya Vijana kupitia kaka yangu Joel Arthur Nanauka mfanye upya *review* ya ushiriki wa hizi Wizara ambazo fedha zimepelekwa. Je, walishiriki ipasavyo katika kufikisha taarifa kwa vijana? Kama taarifa ikionekana kwamba hizi Wizara hazikushiriki vizuri, basi fedha hizi zirudishwe kwenye Wizara ya Vijana, zitafutiwe namna nyingine ya kuweza kugawanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, muda uliotumika kutangaza hii mikopo ni siku chache sana. Tangazo limetoka tarehe 21 na tarehe 3 Aprili, 2026 ilikuwa ndiyo *deadline* ya hii mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi biashara zao siyo rasmi, hazijarasimishwa, hawana leseni, hawana *TIN Number* lakini muda huu mchache kijana huyu anawezaje kupata muda wa kuandaa biashara yake, atafute *TIN Number*, atafute leseni, aombe mkopo kisha apate? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tulikuwa tuna dhamira ya kuwasaidia vijana, tungeangalia changamoto za vijana katika muda ambao wangeweza kuandaa biashara na kuomba huo mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia masharti yanayotumika katika huo mkopo, kwanza uwe na *TIN Number*, uwe na leseni. Vijana wengi wa kijijini kwangu kule Mpanyani, na Chiwale biashara zao siyo rasmi, wanafanya biashara ndogo ndogo, hawana *TIN Number*, hawana leseni. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kupitia Wizara ya Vijana, wafanye *review* upya ya hii mikopo ya shilingi bilioni 200 ili tuweze kuwafikia vijana wengi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itapendeza, kwa nini hii mikopo isigawanywe kwa mtindo wa majimbo? Kwa sababu Tanzania hapa tuna majimbo 272, kama hizi shilingi bilioni 200

zingegawanywa kwa majimbo 272, inamaanisha kila jimbo lilikuwa lina uwezo wa kupata fedha shilingi 735,294,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ningepata hizi fedha shilingi 735,294,000 ningezigawanya kwenye kata zangu 16, na kila kata ingepata shilingi 45,955,000. Kama ningegawanya kwenye vijiji 70 vilivyopo kwenye Jimbo langu la Ndanda, inamaanisha kila Kijiji kilikuwa kinaweza kupata shilingi 10,500,000. Inamaanisha kila Kijiji kilikuwa kina uwezo wa kutoa vijana watano ambao wangeweza kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa Tanzania tuna vijiji visivyopungua 12,318, tungezidisha mara 350, maana yake vijana 4,311,000 wangenufaika kupitia mikopo, kuliko huko hizo fedha zilikopelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tuna dhamira ya dhati ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tuje na huu mfumo kugawa hizi fedha kupitia majimbo badala ya kuzitawanya kwenda kwenye Wizara na kurudisha urasimu ambao vijana wengi hawahitaji fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu ajiandae.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii adhimu nami kuweza kuchangia Wizara hii muhimu ya Maendeleo ya Vijana. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai nami kuweza kusimama leo katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na pongezi kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais Mheshimiwa Emmanuel John Nchimbi, na Mheshimiwa Waziri Mkuu Dkt. Lameck Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi zinaenda sambamba na utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Tumeona Mheshimiwa wetu Waziri Mkuu anahangaika kila mikoa kutafuta kero, kutafuta changamoto na kuzipatia majawabu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Kaka Joel Nanauka, akifuatana na Katibu wake Mkuu Mama Jenifa Omolo pamoja na wasaidizi wao wote, kwani wanafanya kazi nzuri na pia wameanza vizuri katika utekelezaji wa kazi za Wizara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapongeza kwa taarifa yao nzuri, kwa kweli taarifa yao imewasilishwa kwa kina, imeeleweka na imegusa maeneo mbalimbali ambayo ni kero kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini ya kwamba, kuanzishwa kwa Wizara hii ni kuhakikisha kwamba tunainua uchumi wa vijana wetu. Ili tuweze kuwafikia vijana hawa, ni lazima wataalamu wetu wa Wizara hii wafike ngazi za chini *(Local Government)* kwenye ngazi ya kata, kwenye ngazi ya Serikali za Mitaa ili waweze kuwasaidia vijana wetu hata katika kuandika maandiko ambayo yanatakiwa kwenye matangazo ya uombaji wa shilingi bilioni 200 ambalo tangazo lake lilisema, limetolewa tarehe hiyo, ambalo lilihusu fursa za mkopo za Mfuko wa Maendeleo kwa Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mambo yaliyokuwa yanahitajika ni pamoja na kuwa na eneo la sifa za mwombaji, namna ya kuomba mkopo, wametoa maelekezo, na pia wamesema mwombaji anatakiwa aambatanishe nyaraka zifuatazo: ikiwemo na andiko la mradi lisilopungua kurasa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli kule kwetu Mandepwende mtu anajua hata hilo andiko la mradi wenye kurasa tano? Hapana, tusifanye hivyo, turahisishe haya masharti, tuendane na maeneo. Kama kule wananchi wa kwetu wengi wao hawaelewi haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba wataalamu wa Wizara washuke chini kwa ajili ya kufanya usaidizi kwa vijana wetu hawa, ikiwezekana waweke hata kliniki waweze kuwasaidia waandike andiko wawakague kwamba andiko linaandikwa hivi. Vinginevyo patayarishwe fomu zenye maelekezo yote, yeye awe anajaza pale sehemu za wazi tu. Hiyo itakuwa imemsaidia kijana kuepuka na kujua hilo andiko la mradi ni kitu gani? Kwa hiyo, tuboreshe baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, tumeona Mheshimiwa Waziri amefanya ziara kwenye baadhi ya mikoa ikiwemo na Mkoa wa Ruvuma. Kwenye ukurasa wake wa saba ameeleza ya kwamba amekutana na hoja 186 ikiwemo hoja ya mikopo ya 10% ile ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza, huu mkopo wa 10% upo kwenye wanawake, vijana, wanawake asilimia nne, vijana asilimia nne na makundi maalum, yaani wenye ulemavu asilimia mbili. Huu mkopo nilikuwa napendekeza uhame kutoka kwenye halmashauri uende kwenye Wizara yake ili iwe rahisi hata kwenye kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mkopo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona vijana wengi wanahangaika wanatoka huko, wanaenda kwa Mwenyekiti wa Mtaa, mara halmashauri, mara kwa Mbunge, wanaenda kuulizia tunapataje huu mkopo? Ni kweli mkopo huu una urasimu mkubwa. Ili kuondokana na dhana hii, tunaomba huu mkopo uhamie kwenye Wizara ambayo imeweza kuwekwa peke yake, Wizara inayohusiana na maendeleo ya vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ili tuweze kuwafikia vijana wetu, lazima elimu itolewe kwenye redio na siyo redio hizi za Tanzania tu, hapana kwenye *local radio* kulingana na maeneo yetu. Kwa mfano, eneo letu la Mkoa wa Ruvuma tunazo redio nyingi tu kulingana na wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wilaya ya Tunduru iko Wapo Redio, vijana kule wanapenda kusikiliza hiyo redio. Ukiwawekea vipindi pale ukatenga muda wa saa moja au mbili huku wanasikiliza muziki, huku wanasikiliza vipindi hivyo vya

maendeleo kwa vijana, tutakuwa tumewapa elimu tena kwa gharama nafuu, kuliko kusubiri unawakusanya vijana wengi kwenye ukumbi eti unawapa elimu. Watapatikana vijana wachache tu. Hawawezi kufikia vijana wote wa lile eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Ruvuma ukienda Namtumbo unakuta kuna redio inaitwa *Site FM*, Songea Mjini *local radio* iko Redio Jogoo, *Redio Selous*, Majimaji, Mbinga na Nyasa unakuta redio inaitwa *Salvation Radio* na *Hekima Radio*. Hizi zote tukiwapa matangazo haya wataweza kuelewa badala ya kusubiri uwakusanye kwenye mkutano maalumu ndiyo unatoa elimu, hapana. Elimu hizi ziende kwenye redio zetu za kule maeneo ambako tunatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda pia kwenye eneo la urejeshaji wa mkopo hasa huu wa shilingi bilioni 200, tumeona muda wa marejesho ni kuanzia miezi mitatu hadi sita. Hii siyo sawa. Huyu kijana aliyekopa, ukimpa miezi mitatu atakuwa hata biashara yake hajaizungusha. Naomba tuongeze muda, badala ya kuanzia hii miezi mitatu, twende miezi sita. Tuanze na miezi sita angalau awe amefanya hiyo biashara yake. Tukifanya hivi hawa vijana wetu tutakuwa tumewasaidia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, pia liko eneo ambalo tunasema vijana wetu wana ukosefu wa ajira. Tunaamini ya kwamba tukiwawezesha hawa vijana, ajira yao itakuwa inatokana na hii mikopo na hawataweza kujiajiri wao wenyewe tu, wataweza kuajiri na vijana wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria, yako maeneo ambapo mikopo hii sidhani kama itawafikia kwa sababu naona kwenye hizi shughuli ambazo zimeainishwa hapa, wengine hawazifanyi kabisa na au wanafanya kwa kiasi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, afanye maboresho kwenye baadhi ya maeneo ili vijana wengi waweze kujiajiri wenyewe kuliko wanavyohangaika hivi sasa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaendesha bodaboda siyo kama wanapenda. Anachukua bodaboda ya tajiri, anaendesha, anafanya marejesho pale ya shilingi 8,000 ili mradi na yeye abakiwe na fedha kidogo, lakini kama tutawawezesha kwa utaratibu ambao tutakuwa tumeuboresha, ninaamini vijana wengi tutakuwa tumewafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ninaamini ni Wizara mtambuka na inafanya mambo mengi makubwa na mazuri. Ninaomba tuendelee kushirikiana na vijana, na watendaji wale wa kutoka kwenye halmashauri ili tuweze kuboresha Wizara hii na iweze kusonga mbele, na vijana wasiwe na maswali kwa wataalamu wa ngazi za chini. Watoke wale wa juu wa halmashauri waende wakaelekeze ngazi za chini, waandae; hata hiyo kliniki kwa ajili ya kuboresha maslahi ya vijana wetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, Mheshimiwa Asma Mwinyi atamalizia.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na maendeleo ya vijana. Nami nikiwa kama kijana, basi ninashukuru angalau nimepata nafasi hii ya kuzungumza na Serikali, na vilevile kuzungumza na vijana wenzangu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sisi kama vijana tumekuwa tuna changamoto nyingi ambazo kwa bahati mbaya zilikuwa hazipati ufumbuzi wa haraka kwa sababu zilikuwa zinashughulikiwa na idara. Tulikuwa ni idara ya vijana ambayo

ilikuwa katika ofisi ambayo inashughulikia matatizo mengine mengi. Kwa hiyo, sisi vijana tulikuwa ni kama idara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa mara ya kwanza katika uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sisi vijana tumetolewa kuwa kama idara, sasa tumekwenda kupewa Wizara rasmi ya kwenda kushughulikia matatizo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunampongeza sana kwa sababu tunaamini kwamba pamoja na matatizo mengi tuliyonayo sisi kama vijana, lakini hili la kutupa Wizara ambayo ita-*deal* na vijana pekee yake, angalau inatoa mwanga kwamba yapo mazuri mengi ambayo yanakuja kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso kaka yangu huwa anasema kwamba "Asiyeshukuru kwa kidogo, hata kwa kikubwa hawezi kushukuru." Kwa hiyo, vijana tunashukuru angalau kwa hili tu la kutupa *visa.* Sisi vijana, hili tu peke yake, tunashukuru, tunajua mambo mengine mengi yanakuja, Mheshimiwa Rais atakwenda kuyamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Waziri, ameeleza katika hotuba yake mambo ambayo ameyafanya tangu amekabidhiwa hii Wizara. Ni Wizara mpya, lakini ameeleza mlolongo wa mambo mengi sana ambayo yamefanyika ndani ya kipindi kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunampongeza yeye pamoja na watendaji wake. Tumekuwa tukiona vilevile ambavyo anaenda katika maeneo mbalimbali, anakunywa chai na bodaboda, anakula maandazi na mamalishe. Hii inaonyesha jinsi gani ambavyo Mheshimiwa Rais hakukosea kumpa Mheshimiwa Joel kuwa msimamizi wa sekta yetu sisi vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zote ambazo zinahusu vijana, mwisho wa siku zinaongea katika eneo moja. Vijana inawezekana tunaambiwa tunahitaji vitu vingi, lakini tunahitaji kitu kimoja tu, fedha. Tunahitaji fedha, siyo kitu kingine

chochote kile. Sasa fedha inapatikana kupitia njia mbalimbali; kuna ajira, kuna ujasiriamali, na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata mipango mingine yote ambayo tutakuwa nayo, kama kijana hatakuwa na fedha ina maana hatuna uhakika kama vijana tutakwenda kuridhika, kwa sababu changamoto nyingine kubwa sana ambayo inatajwa ni ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama vijana tukitendewa haki katika eneo hili kwenye hii Wizara yetu ya Vijana, vijana tukapata yale ambayo tunahitaji, ina maana hata tatizo la ajira kwa nchi yetu litakwenda kupungua kwa kiasi kikubwa sana, kwa sababu vijana wengi ndiyo ambao wanahitaji ajira. Ni kwa bahati mbaya kwamba ukiangalia jinsi ambavyo mambo yanaenda, hatuoni kama kuna mwanga wa tatizo la ajira kumalizika kwa siku za karibuni. Kwa hiyo, ambacho kinaweza kikafanywa na Serikali ni kutuwezesha sisi vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Waziri amekuja na jambo zuri kuhusiana na Benki ya Vijana, tunapongeza sana kwa hili, lakini kabla Benki ya Vijana haijaanza, sisi vijana hapa katikati tunaishije?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tulipewa shilingi bilioni 200, lakini naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengine wote ambao wamesema kwamba zile shilingi bilioni 200 zimeenda tofauti na vile ambavyo sisi vijana tulikuwa tumetarajia, zimeenda katika maeneo mengine mengi ambayo wengine hatuwezi kukajua huku kuna kiasi gani wala utatuma kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kipindi hiki ambacho bado tunasubiri Benki ya Vijana ianze, tumeshuhudia majanga mbalimbali ambayo yametokea kwenye nchi yetu, tumeshuhudia sehemu nyingi ambazo zimekuwa na changamoto, Serikali imepeleka ruzuku. Kwa hiyo, changamoto ya ajira kwa vijana, changamoto ya ukosefu wa kipato kwa vijana sasa hivi tunaomba Serikali basi ichukulie kama ni suala la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikichukulia kama ni suala la dharura, ina maana hata ile shilingi bilioni 200 ambayo tumepewa, ambayo imeenda katika maeneo mengine tofauti, Serikali tunaomba ituongezee sisi vijana. Tunaomba Serikali itukopeshe twende tukapambane kutafuta fedha, tutarudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo Serikali inapeleka ruzuku ili mambo fulani yafanyike vizuri, lakini sisi hatutaki ruzuku, ninaomba mtukopeshe hizo fedha, na tutengenezewe mazingira mazuri ya kuzirejesha. Vilevile ninaomba tutengenezewe mazingira mazuri ya sisi kukubalika tuweze kukopesheka, kwa sababu changamoto kubwa ambayo inatukabili vijana ni kwamba ukienda utaambiwa njoo na dhamana, au vitu mbalimbali ambavyo lazima upeleke kwa ajili ya kupata mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ikitudhamini yenyewe, Serikali ina watu mpaka ngazi ya kijiji, mpaka ngazi ya kitongoji ina watu ambao ni wasimamizi. Kwa hiyo, nikiomba mkopo, itajulikana Dotto anakaa sehemu fulani, Mwenyekiti wake wa Mtaa ni fulani, Mtendaji wa Kijiji ni fulani. Kwa hiyo, siwezi kutoroka na hizo fedha hata kama sina dhamana, lakini niaminiwe kwa kitambulisho cha *NIDA*, kwa vyeti vyangu vya shule, kwa uongozi wa Serikali ambao uko pale. Mniamini mnikopeshe ile fedha halafu mwone baada ya muda mrefu kama sitakuja kurejesha. Tukirejesha na wenzetu watapata; na mkitupatia, changamoto ya ajira itabaki ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama leo mwanafunzi ambaye amemaliza chuo kikuu anaweza akaenda Kariakoo pale, akaongea na mtu mwenye duka akamwambia naomba tisheti 10 niende nikauze nikishauza nitakurejeshea fedha yako nami nipate cha kwangu, mtu mwenye duka anamwamini yule mwanafunzi, kwa nini Serikali isituamini sisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani tuliyonayo kwa Serikali yetu ni kubwa sana na haya mambo ambayo tunayaomba, tunayaomba tukiamini kwamba yanawezekana. Tumesikia fedha ambazo zimeenda sijui *content creators*, sijui nini, kila sehemu

ambazo fedha zimeenda unaanza kuona watu wanakuwa wengi katika lile eneo. Siyo kwamba watu wanafanya vile vitu, lakini ndiko wameona ambako kuna fedha. Kwa hiyo hata zile fedha shilingi bilioni 200 zingebakizwa kwa vijana, sisi vijana ndiyo tunajua tunataka tufanye nini? Msitulazimishe kwenda sijui kufanya hiki, kufanya hiki, au kufanya hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wangepeleka kwa vijana pale, sisi tutajua zile shilingi bilioni 200, Mheshimiwa Joel atajua yeye na vijana wenzake tuzigawane vipi twende tukafanye kazi tuweze kurudisha marejesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, changamoto kubwa ambayo inatukabili sisi vijana, ni kuwa walalamishi. Tunakuwa walalamishi kwa sababu kuna kikundi kidogo cha watu ambao wamejipa usemaji wa vijana kwamba wao ndio wasemaji wa vijana, lakini kile kikundi siyo kikundi sahihi, ni kikundi ambacho hakina suluhisho la vijana lolote. Ni kikundi ambacho kinatufundisha sisi vijana kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuongea na vijana wenzangu Waheshimiwa Wabunge. Vijana wenzangu Tanzania, tusikubali kuingizwa kwenye huo mkenge wa kuwa walalamishi kwa sababu ya watu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye tayari ameshaonesha mwanga kwamba matatizo ya vijana yanawezekana. Tusikilize sauti zinazotoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kijana mwenzetu ambaye ameaminiwa, huyo ndiye awe msemaji wetu vijana. Tusikubali wahuni wengine wakabeba ajenda ya kutusemea sisi vijana wakati sisi vijana tupo, na tunajua kwamba matatizo yetu yanatafutiwa ufumbuzi kwa jinsi ambavyo Dira imeoneshwa na Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kuwaasa vijana wenzangu Wabunge pamoja na vijana wenzangu kote kule walipo, tukatae wahuni, tumsikilize Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Waziri wetu. Hao ndio wamebeba

maono ya Sekta ya Vijana na siyo mtu mwingine yeyote yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunamalizia na Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi.

**MHE. ASMA ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kusimama, nami nichangie hoja katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunipendekeza kugombea Jimbo la Welezo. Pia ninaomba kumshukuru pia Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, kwa kazi nzuri anayoifanya na pia kwa maendeleo mazuri anayotuletea, na hususan katika Jimbo letu la Welezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Katibu wetu, Mheshimiwa Mary Chatanda, kwa kazi yake nzuri ambayo anaifanya. Nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipowashukuru wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua kuwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hii ya leo ninaomba kuunga mkono jambo la ajira ambalo tayari limeshaongelewa, na ni jambo linalowagusa wananchi wangu moja kwa moja, na sisi wengine ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi, takwimu zinaonesha kwamba zaidi ya 50% ni vijana nchini kwetu, lakini pia ni asilimia kubwa ambayo pia Jimbo la Welezo, bado vijana wanakosa ajira. Hili la ajira siyo kwa Jimbo la Welezo tu, lakini nchi nzima. Ninavyosema vijana, ninaongelea vijana wa miaka 15

mpaka 35, na hawa takwimu inaonesha ni milioni 33.16 ya Tanzania Bara, na ni 53.7% ya Watanzania wote; na kwa upande wa Visiwani ni milioni 1.08 ambayo ni sawa na 57.4%. Vijana hawa wote bado wana changamoto kubwa ya ajira inayowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongelea ajira, siongelei tu ajira yoyote, ninaongelea ajira zenye staha, yenye heshima, ajira ambayo inawawezesha vijana hawa wakaishi, wakanyanyuka kiuchumi wakaishi kwa heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona Mheshimiwa Waziri Mkuu aliongelea vitu vikuu vitatu kuhusu bajeti yake ya 2026/2027. Cha kwanza, aliongelea kuimarisha sekta binafsi ili iwe *engine* ya ajira kwa vijana; pili, ni kuwekeza zaidi katika ujuzi na mafunzo; na tatu, aliongelea kuhusu kuboresha mazingira ya biashara na upatikanaji wa mahitaji kwa vijana. Namuunga mkono kwa asilimia mia moja kwa haya ambayo aliyoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuongea kuhusu hii mikopo ambayo inaongelewa ya 10%. Mikopo hii ambayo imewekwa ni mizuri, lakini bado imekuwa ni changamoto kwa vijana wetu kupata stahiki hii moja kwa moja. Hii ni kutokana na urasimu uliowekwa katika upatakanaji wa mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba kutoa mapendekezo machache kwa Serikali. Kwanza kabisa, Serikali iboreshe mfumo wa utoaji mikopo kwa vijana kwa kuondoa urasimu usio wa lazima, kuweka mifumo ya kidijiti ili kurahisisha uwazi, na hii iende moja kwa moja kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali ianzishe *Skills Development Sector* ambazo zitawasaidia vijana kupata zile *skills* ambazo wanahitaji ili waweze kuajiriwa au kujiajiri wenyewe. Hii itasaidia sana katika upatikanaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba Serikali itoe kipaumbele mahususi kwa vijana katika zabuni za miradi ya kimaendeleo. Hii itawasaidia vijana kuweza kujiwekeza wao wenyewe na kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Vijana, nayo pia naipongeza. Ni jambo zuri ambalo wanalifanya na litawasaidia na litaweka uwazi jinsi gani vijana hawa wanaweza kupata hii mikopo na wakajiwezesha wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuongelea kuhusu hii kodi ambayo iliwekwa *tax code* kwa vijana ambayo inaonekana kwa sasa ni jambo ambalo haliwasaidii kutokana na urasimu uliokuwepo kule. Wanatakiwa watoe angalau fedha mwanzoni, ndiyo wapate. Sasa ndiyo kwanza wanaanza, hii fedha hawana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ASMA ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele imelia. Katika kuhitimisha kwangu nimeona Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa shilingi bilioni 200 kwa vijana. Ningependa hii pia ingeletwa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili vijana wa Welezo na pia wengine wote nao wapate kunufaika. Nasi tunakuahidi tutakuwa mfano wa kwanza Jimbo la Welezo kuonesha jinsi gani tutaweza kutumia na kurejesha hii mifuko, na kufuata masharti kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kusema kwamba ajira kwa vijana siyo chaguo, ni lazima kwao. Kwa hiyo, tunaomba kwamba sisi tuko tayari, na ninaahidi vijana wa Jimbo la Welezo kwamba niko nao bega kwa bega kuhakikisha kwamba ajira ipo katika ajenda yangu, ili angalau nao wapate, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi na huyo ndiyo mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, nawapongeza sana, tunakwenda vizuri. Msichoke kujikumbusha Kanuni na kuzifuata. Ninaamini baada ya muda tutakuwa hodari sana, tutakwenda *direct to the*

*point* na hata kwenye maswali, basi tutakuwa hivyo hivyo. Kwa hiyo, tusikate tamaa, tuendelee na mambo yatakuwa mazuri.

Nitawataja wachagiaji ambao wataanza jioni, tutaanza na Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi, Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar, Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mheshimiwa Said Salim Hamad, Mheshimiwa Dkt. Regina Malima, na Mheshimiwa Jesca John Magufuli. Baada ya hao tutaendelea na wengine.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo. Mnakumbushwa kwamba kesho siku ya Jumanne tarehe 21 Aprili, 2026, kutakuwa na zoezi la uchaguzi wa manahodha kwa michezo yote ya klabu ya Bunge kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 1.30 asubuhi wakati wa mazoezi. Aidha, uchaguzi utafanyika katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma kwa michezo yote, na siyo kama ilivyotangazwa awali. Hivyo wana michezo wote mnaombwa kufika bila kukosa.

Pia kuna tangazo lile nilitangaza mwanzo baada tu ya kusitisha shughuli za Bunge, kwamba Waheshimiwa Wabunge wote tunaombwa Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya semina kutoka Wizara ya Nishati.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.15 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Wachangiaji wetu wa jioni tutaanza na Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi atafuatiwa na Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar, na Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MUHSIN HAJI USSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ametupa afya njema, na leo tupo katika Bunge hili Tukufu kujadili mambo mtambuka yenye maslahi mapana kwa vijana wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwa dhati ya moyo wangu kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Vilevile, kumpongeza pia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa dhamira zao za dhati za kuanzisha Wizara ya Maendeleo ya Vijana ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema kwamba nimefanya tafiti na nimejiridhisha kwa Afrika, sisi Tanzania ni nchi ya kwanza kuwa Wizara pekee ambayo ina mamlaka ya wazi na ya moja kwa moja juu ya uratibu madhubuti wa sera na programu zote za vijana. Nchi nyingine zote zinatumia Mfumo wa *Integrated Ministry,* yaani Wizara ya Vijana imeunganishwa na michezo ama sanaa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuletea jembe Mheshimiwa Waziri Joel Nanauka, kijana mzalendo, mchapakazi ambaye mimi binafsi nimemfahamu kabla hajawa Mbunge wala Waziri. Amekuwa akishajihisha na kutoa elimu kwa vijana juu ya namna bora ya matumizi sahihi ya

fedha *(financial literacy)* na namna ya kubadilisha maisha yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninataka kuchangia niungane na Wabunge wengi ambao wameshangaa kwamba, Mheshimiwa huyu ana Wizara inayohusiana na vijana na maendeleo yake, lakini hana fedha; na kwa namna anavyofanya kazi mara nyingi yupo *site*, anakutana na makundi ya vijana na amekuwa maarufu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unampa kazi ya kumchonganisha na vijana wa Kitanzania, watamkimbia huko *site* wataona Waziri amekuja kupiga soga na sisi, lakini hana fedha. Kwa hiyo, ninaomba zile fedha mahsusi ambazo zimetengwa ikiwemo shilingi bilioni 200 kwa ajili ya vijana zipelekwe moja kwa moja kwenye Wizara hiyo ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwa umakini sana hotuba yake, ukurasa wa 10, Mheshimiwa Waziri anakiri ukosefu wa ajira Tanzania na hasa kwa vijana. Ukosefu wa ajira siyo Tanzania tu, tukubaliane; duniani kote kuna changamoto hii ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, pamoja na utafiti wa nguvu kazi wa mwaka 2023/2024 *(Integrated Labor Force Survey)* inaonesha zaidi ya 60% ya Watanzania ni vijana ambao wana *range* kwenye umri wa miaka 15 na 35. Kila mwaka, zaidi wa vijana 1,000,000 huwa wanaingia kwenye soko la kutafuta ajira, wanaofanikiwa ni vijana wasiozidi 300,000, wasiofanikiwa ni vijana wanaozidi zaidi ya 700,000 kwa mwaka. Ni kusema kwamba zaidi ya 12.12% ni vijana ambao wana ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limezidi hata lengo la Taifa ambalo tulijiwekea walau kwa asilimia nane ya ukosefu wa ajira. Hata hivyo, inaonesha vijijini kuna unafuu zaidi kuliko mijini, vijana wengi wa mijini wanahangaika na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata maandiko Matakifu ya Biblia yanasema, "Mtu yeyote asiyefanya kazi basi na asile." Hata

Katiba ya Chama Cha Mapinduzi, miongoni mwa masharti ya uanachama, sharti nambari tatu inasema, "Ukiwa mwanachama uwe ni mtu mwenye kuamini ya kwamba kazi ni kipimo cha utu na kuitekeleza imani hiyo kwa vitendo." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za mwaka 2024 zimeonesha, Tanzania ina watumiaji zaidi milioni 30 wa *internet*. Sasa ninataka kuja hapa kumsadia Mheshimiwa Waziri, anawezaje kutatua changamoto ya vijana wa mijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumiaji wa laini za simu zilizosajiliwa ni milioni 60. Katika hizo, laini milioni 35 zinatumia mfumo wa *mobile money,* yaani mfumo wa kutumia simu kwa ajili ya kufanya miamala ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe ushauri kwa Wizara, ili kuondoa changamoto hii Mijini, kwanza kwa upande wa sera, kuanzishwe vituo vya TEHAMA vya Kitaifa katika miji mikubwa. Kwa mfano, tunaweza tukawa na kituo pale Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule India mwaka 2015 walianzisha kituo kinaitwa *Digital* India ambacho kilikuwa kinafundisha vijana mambo mbalimbali ikiwemo *artificial intelligence, freelancing*, *digital economy* na kadhalika. Vijana wetu wengi sasa hivi wanatumia mitandao, wanatumia *internet,* hii itasaidia kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Zanzibar, ukienda Jimboni kwangu Malindi kuna eneo linaitwa Forodhani, kuna vijana wa Makachu wanatumia *internet,* na mitandao ya kijamii kuonesha namna gani Zanzibar na Tanzania ilivyo nzuri na kuvutia uwekezaji na watalii wengi. Vilevile, Serikali itoe motisha za kikodi kwa kampuni ambazo zinaajiri vijana na hasa katika eneo hili la teknolojia na mitandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe mchango wangu wa mwisho. Ukurasa wa 10 huo huo, Mheshimiwa Waziri amekiri ya kwamba vijana wanakosa ujuzi na utaalamu ambao unaendana

na mahitaji ya soko. Nimezungumzia vijana wa mjini, sasa wataniuliza wa kule vijijini inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna kitu cha kujivunia Tanzania, tuna ardhi nzuri yenye rutuba kwa ajili ya kilimo. Inaonesha zaidi ya 60% ya Watanzania wamejiwekeza kwenye kilimo. Niliwahi kusema hapa kwamba vijana tunakimbia kilimo, na sababu ziko wazi. Moja, kilimo hakina teknolojia ya kisasa; pili, hakina faida ya haraka; tatu, hakina mfumo mzuri wa soko. Kijana yuko tayari awe na bodaboda apate shilingi 10,000 kwa siku kuliko kuwekeza kwenye kilimo kitakachomtajirisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema hivi, "Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi." Uti huu wa mgongo unahitaji kuimarishwa ili kuendana na mahitaji ya sasa ya kiulimwengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kuishauri Serikali, kwanza, kuanzisha *agri-business parts* (kilimo biashara). Nitatoa mfano, kule Brazil wamefanikiwa sana kwa sababu, kilimo kimeunganishwa moja kwa moja na usindikaji na masoko. Kwa hiyo, vijana wanalima, wanapata fedha, na Serikali inakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuwe na mfumo wa mkataba unaitwa *contract farming*. Kule China wakulima wadogo wadogo wameunganishwa na kampuni kubwa za kilimo. Tunaacha udalali hapa katikati, vijana wanapata fedha, Serikali inapata uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, kuna kitu kinaitwa *agritech*. Kuna siku nilikuwa ninamtembelea, rafiki yangu kule Songea akaniambia siwezi kupata mazao kwa sababu ya mvua. Ninaishauri Serikali, tuwekeze katika *irrigation,* tuangalie namna bora ya kuwa na *drones* ambazo zitaweza kusaidia hususan kwenye umwagialiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. nilimwita Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar, Tinnar Andrew Chenge atafuatiwa na Mheshimiwa Saidi Salim Hamad.

Waheshimiwa Wabunge, tunachangia dakika nane. Kengele ya kwanza ikilia, kengele ya pili unaunga mkono hoja. Kwa hiyo, jipange vizuri unapomalizia ya kwamba utakuwa na dakika moja ya kumalizia. Tunaendelea Mheshimiwa Omar.

**MHE. ZULFA MMAKA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia leo hii katika Wizara hii. Kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha uhai na uzima ili kuweza kuungana na wananchi katika majukumu yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kufanya mambo mazuri, makubwa na yenye mwonekano kwa kipindi kifupi tu ambacho kaingia madarakani. Katika mambo hayo ambayo leo hii tunayoiona, Mheshimiwa Rais wetu wa Tanzania wakati analihutubia Bunge hili alitoa ahadi nyingi ikiwemo uanzishwaji wa Wizara hii. Wizara hii imeanzishwa, inafanya kazi na pia ameruzuku fedha nyingi kwa ajili ya kuwasaidia vijana katika kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite katika sera na mipango ya Wizara hii. Lazima tubadilike kutoka kuwa ya kiutawala na kwenda kuwa ya matokeo yanayoonekana. Ninaomba nichangie kuhusu mitaji. Tatizo la vijana siyo ukosefu wa ubunifu, bali ni ukosefu wa upatikanaji wa sera, mitaji nafuu na upatikanaji wa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko ya uwezeshaji ambayo tukonayo sasa hivi vijana, ni mifuko ambayo ina masharti magumu, na utaratibu mrefu wa kuipata. Suala hilo linachangia vijana kutokupata mikopo hii kwa ajili ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara basi ije na mfumo wa mikopo midogo *(micro finance)* ili tuweze kupata mikopo hiyo yenye riba nafuu, dhamana mbadala na ufuatiliaji wa karibu.

Aidha, kuwe kuna *blended finance model* ambayo Serikali itachukua sehemu hatarishi ili kuvutia taasisi binafsi kuweza kuwavutia vijana kuliko kuachia vijana kujiingiza katika mikopo chechefu kama vile kausha damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujuzi na vitendo ni muhimu kwa vijana wetu. Ni lazima tubadili mtazamo, siyo kila kijana anaweza kuajiriwa Serikalini. Basi, tunahitaji mapinduzi ya kweli katika mafunzo ya ufundi, ujenzi, kilimo cha kisasa, uchakataji wa mazao, TEHAMA na huduma za kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapendekeza kuanzishwa kwa vituo vya ubunifu katika kila mkoa vitakavyoweza kuunganisha mafunzo ya teknolojia na masoko ya bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibikaji wa Wizara bila viashiria mahsusi vya kupima mafanikio tutabakia tu na kauli nzuri bila mafanikio ambayo yanaonekana. Ninaiomba Wizara, basi iweke wazi takwimu za kila mwaka kuhusu idadi ya ajira mpya za vijana zilizotolewa, biashara mpya zilizoanzishwa, ongezeko la kipato kwa walengwa hizi, ziwe ni *KPI* rasmi zinazokaguliwa na Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusisitiza kwamba mapambano dhidi ya umaskini wa vijana siyo suala la sera pekee, ni suala la dharura la Kitaifa. Kushindwa kuwawezesha vijana leo hii tunajenga mzigo wa kesho. Hivyo basi, ninaiomba Wizara hii ije na mkakati mahsusi utakaotekelezeka na unaopimika kimikakati utakaowatoa vijana kutoka kwenye umaskini na kujiingiza kwenye uzalishaji wenye tija na unaonekana katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutambue kwamba vijana siyo viongozi wa kesho peke yake, bali ni nguvu kazi ya sasa. Unapomkosesha kijana ajira, siyo kwamba unamkosesha kipato peke yake, bali unamkosesha matumaini ya maisha yake ya baadaye na ya sasa, hadhi yake katika jamii, na imani yake katika mfumo mzima wa maisha. Jambo hili ni hatari sana katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa ajira unaweza kusababisha na kuchochea ongezeko la vitendo vibaya vya rushwa, uhalifu, matumizi ya dawa za kulevya pamoja na mmomonyoko wa maadili katika jamii zetu. Pia, ninaiomba sana Serikali hii inapokuja katika suala la mikopo, tuangalie mikopo hii wanaonufaika ni kweli wale wahusika? Au wanaonufaika ni wale ambao wana ukarimu wa karibu na wale watoaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wana imani sana na Serikali yetu hii ya Mama Samia. Tunafahamu kwamba Mama Samia ana imani kubwa sana juu ya sisi vijana na tunaona kwamba hata katika Bunge hili, kuna mifano ya kutosha. Wabunge wengi ambao walipitishwa na Chama chetu cha Mapinduzi ni vijana na pia katika uteuzi wa nafasi zake tunaona nafasi nyingi vijana wameteuliwa na wameaminiwa katika nafasi kubwa kubwa ili sasa kuleta maendeleo makubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwombe sana Mama Samia, sisi vijana tunampenda, tunamjali na tunamwomba Mwenyezi Mungu azidi kumzidishia nguvu, hekima na busara katika kuiongoza nchi hii. Sisi Vijana wa Tanzania tuko bega kwa bega na Mheshimiwa Rais, kuna msemo unasema, "Hakuna kama Mama." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunadhihirisha moja kwa moja kwa matendo anayoyafanya Mheshimiwa Mama Samia. Anayafanya kama Rais, lakini ni kama mama kwa watoto wake, katika nchi yake. Rais wetu wa Tanzania ameamua kuja na mageuzi makubwa kwa vijana, na sisi tunayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana vijana wenzangu walioko mitaani, wamwamini Mheshimiwa Rais kwamba anaweza na ana imani kubwa juu yetu, tusishawishike, na tusiingikie katika makundi mabaya ya kuaminishwa kwamba nchi yetu haitutambui ama haitupendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotoshaji unaofanyika huko katika mitandao; niwaombe sana vijana wenzangu tujikite katika kufanya kazi, tujikite katika masuala mazima ya kiupendo na imani na nchi yetu kumuunga mkono Mheshimiwa Mama Samia

Suluhu Hassan ambaye anatuonesha imani kubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita sasa Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, na Mheshimiwa Saidi Hamad ajiandae.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Wizara ya Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumrudishia sifa na utukufu kwa kunipa uhai wa kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia kwa kuanzisha rasmi Wizara ya Maendeleo ya Vijana na kumteua kijana msikivu Mheshimiwa Joel Arthur Nanauka kuongaza Wizara hii ambayo imebeba changamoto, maono na matarajio ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, na kama ilivyowasilishwa kwenye taarifa yetu, tulipata bahati ya kutembelea kikundi cha vijana ambacho kipo pale Muheza Tanga. Kikundi hiki ni moja ya vikundi vya vijana ambavyo vinafanya vizuri sana. Ninaiomba kabisa Wizara iendelee kukilea kikundi hiki lakini pia kutumia kikundi hiki kama balozi wa mafanikio kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikundi hiki kinafanya shughuli zake pembezoni mwa barabara. Ninaomba sana uongozi wa Mkoa wa Tanga uone namna ya kuwatafutia eneo la kudumu vijana hawa ili waweze kufanya kazi zao kwa tija. Kikundi hiki pia kinazalisha bidhaa za ujenzi. Ninaomba sana uongozi wa Mkoa wa Tanga uone namna ya kuwasapoti vijana hawa kwa kutumia bidhaa zao kwenye miradi ya ujenzi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, vijana hawa waliomba mkopo kwa ajili ya kutafuta usafiri, kuweza kusafirisha bidhaa zao kuzipeleka kwa wateja. Ninaiomba sana Wizara ione namna ya kuwapatia mkopo huu ili waweze kufanya kazi zao na kuwapunguzia gharama za kusafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Wizara hii imetenga bajeti ya shilingi 35,957,298,000. Kati ya hizo, zilizotengwa kwa miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni tano *plus*. Kwangu mimi ninaona fedha hizi bado ni kidogo ukilinganisha na mahitaji makubwa ya kundi hili maalumu la vijana ambalo ndiyo nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Serikali ione namna ya kuongeza bajeti kwenye eneo hili. Ninaungana na Wabunge wenzangu kusisitiza kwamba zile shilingi bilioni 200 za vijana zirudi kwenye Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba niendelee kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inaendelea kuwainua kiuchumi siyo vijana tu, bali wanawake na watu wenye ulemavu. Ninaomba sasa nichangie katika maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ni kuhusu mitaji kwa vijana. Vijana wengi wana nia na ari ya kufanya kazi, lakini wanakosa mitaji au wakati mwingine wanakutana na masharti magumu ya mitaji au mikopo hii, kiasi ambacho wanashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba hapa Serikali iongeze juhudi katika kuhakikisha kwamba inapunguza urasimu wa upatikanaji wa mikopo hii. Hapa ninaomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli yake ya kusema kwamba, tutumie *NIDA* badala ya kuomba barua. Kwa hiyo, kama mtu ana *NIDA,* hakuna sababu ya kupewa barua ya utambulisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni changamoto ya ujuzi usioendana na soko halisi la ajira kwa sasa. Ni dhahiri kwamba, bado kuna pengo kati ya elimu ambayo tunaitoa kwa wahitimu wetu na soko la ajira. Ninaiomba Serikali iendelee

kuboresha mitaala, hasa kwenye eneo la mafunzo kwa vitendo, teknolojia na ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ajira zisizo na uhakika wa kipato kwa vijana wetu. Vijana wetu wengi wanafanya kazi katika sekta ambayo siyo rasmi, ambayo haina uhakika wa kipato cha kudumu, lakini pia, haina uhakika wa hifadhi ya jamii. Hapa ninaiomba Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi iongeze rasilimali zaidi kwenye sekta zenye kutoa ajira nyingi, kwa mfano, kwenye Sekta ya Viwanda pamoja na Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la afya ya akili. Kutokana na matatizo na changamoto, vijana wetu wengi wanakumbwa na tatizo la msongo wa mawazo. Kwa ajili hiyo, wengine wamefikia hatua wanakata tamaa, na wengine wanaingia kwenye vitendo ambavyo havina tija, kwa mfano kucheza kamari kupita kiasi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iwekeze zaidi kwenye eneo la afya ya jamii kwa kuongeza wataalamu wa kutoa ushauri nahasa kwa vijana wetu, ili kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni matumizi yasiyo na tija ya mitandao ya jamii. Ni ukweli usiopingika kwamba, mitandao ya jamii ni fursa na ni uchumi kama ikitumika vizuri, lakini bado vijana wetu wengi wanatumia mitandao hii vibaya. Ninaiomba Wizara, ikishirikiana na wadau wa vijana, ione namna ya kuwaelimisha vijana wetu juu ya matumizi sahihi ya mitandao ya jamii, ili waweze kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano mingi ya ambao wanatumia mitandao ya jamii na wanaishi maisha yao vizuri kama akina Shilole, Niffa, na Kelvin. Ninaomba tujifunze kutoka kwa vijana hao. Ninaiomba Wizara iendelee kuwafikia vijana, hasa wale walioko katika maeneo ya vijijini, ili na wenyewe waweze kupata fursa kama vijana wa mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ukosefu wa mwongozo au *mentorship* kwa vijana wetu. Vijana wetu hawajapata watu wa kuweza kuwasaida katika safari zao za

kiuchumi au kitaaluma. Ninaomba tuwekeze sana kwenye eneo hili, ili tupate washauri watakaoweza kuwasaidia katika kuwapa mwongozo wa namna gani hasa kwenye eneo la uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, japo siyo kwa umuhimu, ni kitu ambacho mimi ninakiita *after care,* hata sisi wazazi tukishajifungua kuna kitu kinaitwa *postnatal*. Sasa, ni kweli tunawapa vijana mikopo, lakini mara nyingi hatuwafuatilii kwamba wanaendeleaje? Ninaomba tuweke mkazo kwenye ufuatiliaji, ili kuweza kubaini changamoto za vijana hao. Siyo changamoto tu, na maendeleo yao pia, ili tuweze kuwapa ushauri wa namna gani ya kutunza fedha, kwa sababu, hapa ndiyo kwenye tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Saidi Salim Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Regina Malima, na Mheshimiwa Jesca John Magufuli ajiandae.

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru nami kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi. Pia ninaishukuru Kamati za Siasa kwa ngazi zote zilizonipitisha kuanzia mkoa na wilaya. Kipekee kabisa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Ole, hususan Wajumbe, wamekuwa wema kwangu, ni watu wazuri. Wajumbe hawa watakapokufa wote wataingia Peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa Wizara hii ya Vijana, ninatanguliza pongezi. Pongezi hizi ninazielekeza moja kwa moja kwa Wizara inayoongozwa na kaka yangu, Mheshimiwa Nanauka. Tarehe 4 Aprili, 2026 nilisimama ndani ya Bunge hili

Tukufu kuchangia, nikauliza, kwa nini tusianzishe Benki ya Maendeleo ya Vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hilo leo katika wasilisho la Wizara hii, Mheshimiwa Waziri amesema sasa ni muda sahihi wa Serikali, kupitia Wizara ya Vijana, kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Vijana ili Vijana wa Kitanzania waende wakafungue akaunti zao, na wakafanye *cash deposit* hapo. Wakiwa wanahitaji kukopa, waende wakakope katika Benki yao ya Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipa pongezi Serikali kupitia Wizara hiyo. Nasi mnatupa imani ya kutafuta fikra mbalimbali kuja kuishauri Wizara, kwani tumeona mawazo ambayo tunayaleta, yanachukuliwa, yanachakatwa na wakiona yanafaa, basi wanakuja nayo kwenye mikakati yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipongeza Wizara ninaomba nichangie, kwa ruhusa yako, kuhusu fursa za vijana ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amezitengeneza kupitia Wizara mbalimbali. Tunajua tuna Wizara ya Vijana ambayo ni mpya, lakini kuna fursa za vijana za kiuchumi na za kiajira kupitia Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, Wizara ya Uchukuzi kwenye Taasisi yetu ya *DMI* pale, Wizara hii imefanya taasisi zake ziwe za kushikana na kusaidiana. *DMI* imewezeshwa na *TPA* chini ya mwekezaji wetu *DP World* kununua *simulator* ya kisasa, ambayo inaitwa *Full Mission Desk and Engine Simulator*. Unaposoma *DMI* sasa hivi, ndani ya miaka hii miwili iliyopita, unasoma kupitia *simulator* hii na unapotoka pale unakuwa umebobea. Mtambo huu ambao uko pale ni nchi siyo zaidi ya tatu Afrika nzima ambazo tunaumiliki, tukiwemo na sisi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya mtambo huu ambao umenunuliwa chini ya Profesa Tumaini pale, una thamani ya Dola za Kimarekani *2.8 million*. Huu umesababisha vijana wetu wa Kitanzania kwenda *DMI,* wanapata fursa za kielimu za kisasa na

wanapotoka pale wanapata fursa za kiajira, dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Taasisi ile ya *DMI* tulipokwenda kutembelea, Kamati ya Miundombinu, tumepata fursa za vijana zilizotengenezwa kupitia mtambo huu. Kuna meli za Kimataifa zimejikita sasa hivi kutaka kufunga mkataba na *DMI* kwamba, *cabin crew* yote na mabaharia wote wa meli hizo wawe ni vijana wa Kitanzania ambao wametoka pale *DMI* kupitia mtambo ule. Kwa hiyo, haya mambo hayatokei tu *by nature,* ni jitihada za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya Serikali yake, ambayo imewezesha kupata fursa kama hizi za ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna fursa za vijana zilizoko katika Wizara ya Mawasiliano chini ya mama yetu Mheshimiwa Kairuki. Kuna huu Mfuko wa *UCSAF*, ambao unajenga minara, kama alivyozindua juzi pale Mheshimiwa Mama Samia. Mpaka sasa tumejenga takribani minara 2,151. Sisi tumebahatika kutembelea mnara mmoja tu, Kigamboni. Mnara huo umetengeneza fursa za vijana za ajira na kiuchumi, kama zifuatazo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnara ule wa pale Kigamboni ambao tumeenda kuutembelea umewezesha kuajiri au kujiajiri vijana 157 kama mawakala. Wamepata *job opportunity* kupitia mnara ule ambao umejengwa. Vilevile kuna vijana wa *Bolt* na *Uber* walikuwa pale hakuna *network*. Kwa hiyo, wanasema mtandao kulikuwa hakuna, walikuwa hawawezi kwenda kutoa *service* katika maeneo yale. Baada ya kujengwa mnara huu, vijana wetu wa *Uber* na *Bolt* wamejikuta wanaenda pale kupata riziki zao za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tukakutana na vijana ambao wamejiajiri kupitia *online shopping* pamoja na *delivery services* za *online* pia, nao wamejiajiri baada ya mnara ule kufika pale. Vilevile, tukakutana na wanafunzi ambao wanasoma chuo kikuu. Vijana wetu hawa ambao ni wasomi walikuwa wanapata shida ya mawasiliano wakiwa wako pale Kigamboni, walikuwa hawana *network,* wakati wa usiku wanasumbuka. Baada ya

Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, kupeleka mnara huu, vijana hawa wamepata ajira, mawakala 157, *Bolt* wanaenda pale kujiajiri, *online shopping* wanafanya kazi zao na vijana wetu ambao wanasoma, wamejipatia fursa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kutembelea *TCAA*, kuna fursa iko pale Chuo chetu cha Mamlaka ya Anga Tanzania, fursa ya kipekee kabisa. Kuna kozi inatolewa pale inaitwa ni *Aircraft Controller*. Hii *Aircraft Controller* ambayo inatolewa pale, vijana wanatoka Somalia, tumekuta zaidi ya wanafunzi 70 na wengine 34 kutoka Uganda wanasoma kozi ile kwa thamani ya shilingi milioni 70. Ni kozi ya wiki saba, lakini Mheshimiwa Mama Samia katoa maelekezo kwa Mheshimiwa Prof. Mbarawa, Kijana wa Kitanzania anayekwenda kusoma *Aircraft Controller* ndani ya chuo hiki alipie shilingi milioni 10 tu. Hizi ni fursa ambazo ziko katika Wizara nyingine, lakini zinatufaa sisi vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuchangia mchango wangu. Sisi vijana tulikuwa tunasikitika hapo zamani, zikitokea nafasi za jeshi tunatafutwa vijana; zikitokea nafasi za Polisi tunatafutwa vijana; zikitokea kazi ngumu za zege, tunawekwa vijana; lakini kazi za uongozi hatushirikishwi vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Bunge hili ambalo tupo, tuna Wabunge wa Vijana ambao ni Viti Maalumu na tuna Wabunge wa Majimbo ambao ni vijana. Leo ndani ya Bunge hili tuna Mawaziri ambao ni vijana. Leo ndani ya Bunge hili kuna Makatibu Wakuu, kuna Maafisa Mezani pale wote ni vijana. Haya ni maono ya Mheshimiwa Mama Samia kupitia kuwajali vijana wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kwa kusoma maneno matukufu kutoka katika Biblia. Methali 3:5-6 kuna maneno ya kumtia moyo Mheshimiwa Mama Samia, yanasema, *"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atanyoosha mapito yako."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Kitabu Kitukufu cha Quran kuna aya inayosema, *"Isubiru wa Swabiur"*. Ee Mama

Samia Quran inakwambia; subiria na uvute kwenye subira. Pia kuna aya inasema, *"Wa Bashir As-Sabireen."* Nimpe ishara njema Mheshimiwa Mama Samia, kwa anayoyasubiria ndani ya nchi hii. Mama fanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda wako umeisha. Ninamwita sasa Mheshimiwa Jesca John Magufuli, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Daniel Surati, na Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MAGUFULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenijaalia uhai na kuniwezesha kusimama hapa siku ya leo kwa niaba ya vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninaanza kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo ameweza kutekeleza dhima ya kuweza kuwainua vijana, hususan katika sekta ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo imeweza kudhihirishwa kutokana na mikopo na jitihada ambazo Mheshimiwa Rais amekuwa akizifanya kwa kusaidia kutoa mikopo kwa vijana. Kwa kweli, hili lazima tusimame kama vijana kumpongeza kwa jinsi ambavyo ameweza kuonesha na ameweza kusimama thabiti na vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza pia Waziri wa Maendeleo ya Vijana, kaka yangu Mheshimiwa Joel Nanauka. Kwa kweli, amewasilisha hotuba yake leo asubuhi na tumeweza kuipitia, lakini kwa kuipitia huko tumeweza kutambua ni jinsi gani ambavyo amejikita zaidi katika kuwasaidia vijana, kuwainua, na kuleta mapinduzi makubwa, ambayo yanawalenga moja kwa moja vijana wa Kitanzania. Kwa hiyo, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yameongelewa na vijana wenzangu, lakini kwa siku hii ya leo ninaomba nijikite kwenye mambo makuu mawili, nikianza na suala la mikopo. Kweli Serikali imejizatiti na imekuwa ikiendelea kutoa mikopo kwa vijana, lakini bado hatuwezi kutegemea mikopo tu. Ninajua ni ukweli mchungu, lakini lazima tuongee, kwamba hatuwezi kutegemea mikopo tu katika kuwezesha vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo hii, ili kijana aweze kunufaika kibiashara, ili kijana aweze kuwa na *consistency* katika biashara, ili kijana aweze kutanuka zaidi katika biashara, ni lazima tuwe na mfumo jumuishi wa ujasiriamali wa vijana wetu wa Taifa hili la Tanzania. Tunapozungumzia mfumo huo wa ujasiriamali kwanza kabisa ni lazima tuwajengee uwezo *(capacity building)* vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajikita zaidi katika kutoa mikopo ambayo kweli imekuwa ikitusaidia, lakini lazima tuwajengee uwezo vijana hawa ili waweze kupata elimu au mwanzo mzuri wa kuweza kuitumia mikopo hiyo. Ninaposemea hapa katika *capacity building,* nitajikita zaidi katika suala la elimu ndogo ndogo tu kama ya utunzaji wa fedha na pia elimu ya kuweza kutambua kodi za Serikali na jinsi ya kuanza mwanzo wa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itamwezesha kijana huyu hata anapoingia katika biashara kupitia mikopo ambayo imetolewa kuweza kutambua ni namna gani ataweza kutunza kumbukumbu zake za fedha na ni namna gani ataweza kukabiliana na kodi ambazo zitakuwa zinakuja. Anakuwa na uelewa wa kodi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nizungumzie kuhusu mafunzo ya kisekta *(specific training)*. Kweli mikopo imekuwa inatolewa na vijana wamejikita waziwazi katika kuwekeza katika nyanja tofauti. Wengine wamejikita katika kuwekeza katika teknolojia, lakini wapo ambao wamejikita kuwekeza katika kilimo, na wapo ambao wamejikita kuwekeza katika viwanda vidogo vidogo. Kusema kuwachukua hao wote na kuwapa *training* siku

moja kwa ujumla ni uongo. Ni sawasawa na kutwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwatafute ma-*professional*. Uzuri, Wizara ya Vijana inaweza kushirikiana na Wizara nyingine kama ya teknolojia, Wizara ya Kilimo pamoja na Mifugo, ili kuwasaidia vijana hawa pale ambapo wamepewa mkopo huo na inapoambatana na mafunzo hayo, ambayo ni ya kimkakati yatakayotolewa, kuwekeza zaidi na kwa ufasaha na kwa ukubwa ambao Serikali inataka iwekeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusu suala la *addition of value,* kuwajengea thamani vijana hawa. Mikopo inatolewa, lakini pia, lazima tuhakikishe kwamba tunawajengea thamani ya bidhaa zao ambazo vijana wamejikita zaidi katika kuziwekeza. Bidhaa hizi ni lazima ziambatane na soko la ushindani ambalo lipo Kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuwapatia *training,* na pia, kuwasukuma kuwezesha kuzalisha bidhaa ambazo zinaendana na soko la kila siku. Tusije tukawa tunatoa mikopo, lakini mwisho wa siku mikopo hiyo ikawa vijana wana-*produce products* ambazo ni za hapa hapa tu, yaani haziendi sehemu yoyote, na hazina ukuaji. Kwa hiyo, ni lazima tufuatilie, na ni lazima tu-*intensify* hili kwa ajili ya kusaidia kumpatia kipato kijana huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu upatikanaji wa masoko. Ni kweli Serikali imejikita katika kuendelea kutoa mikopo hiyo, lakini je imewatafutia soko vijana au ndiyo tunatoa mikopo na tunawaacha tu waendelee ku-*hang hang* tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuwatafutie masoko ya Kimataifa na ya Kitaifa pia. Kwanza utamjengea uwezo kijana huyo, na jambo la pili utamsaidia yeye mwenyewe kuongeza kipato, *comfort* ambayo anaipata pale ambapo anapata mkopo. Pia Serikali iwatafutie masoko kuweza kuuza bidhaa hizo ambazo wataweza kuzalisha kupitia mkopo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba Waziri niendelee kumshauri jambo la mwisho kuhusu kuanzisha maonesho ya vijana *(youth expo)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imekuwa ikisifika kwa kuanzisha maonesho ya biashara kama Saba Saba ambayo kiuhalisia yamekuwepo kwa miaka mingi, lakini pia kuna maonesho ya wakulima Nane Nane. Kwa nini sasa isifike wakati nasi tuwe na maonesho yetu, kwa kuwa tumetoa mikopo na tumewawezesha vijana hawa, *database* tunayo, kwa nini tusiwajengee kuwepo na maonesho hayo ya vijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca muda wako umeisha.

**MHE. JESCA J. MAGUFULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Malizia kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MAGUFULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa atafuatia, Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar, ajiandae.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuchangia bajeti ya Maendeleo ya Vijana. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuendelea kusimama hapa nikiwa buheri wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, pia ninaendelea kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Serengeti kwa kuendelea kuniamini kijana kama mimi kuendelea kuwawakilisha Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa ni mchoyo wa fadhila kama kijana ambaye ninatokana na asasi za kiraia ambapo ninafahamu ni kwa jinsi gani kipindi hicho, hata sijajua Mungu atanibariki kuwa Mbunge, tulikuwa tunakuja mara ngapi hapa Bungeni kushawishi Wabunge kwamba sisi vijana tuweze kupewa Wizara yetu ya Vijana. Ndoto hii amekwenda kuitimiza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kwa dhati ya moyo wangu ninasema ahsante kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakukomea hapo tu, ameenda mbali, amerekebisha Sheria ya Manunuzi ya Umma, ambapo amezitaka taasisi zote kutenga 30% ya manunuzi yao kuhakikisha kwamba makundi maalum yanaweza kunufaika. Katika makundi hayo ni sambamba na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kumekuwa na programu mbalimbali za kunufaisha vijana, kama programu ya *Building a Better Tomorrow*. Pia kuna mafunzo ambayo yamekuwa yanatolewa kupitia *VETA* na takribani vijana 8,000 wamenufaika na mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo kuna ajira ambazo zimekuwa zinatolewa na sekta mbalimbali ambapo jumla ni sekta milioni nane. Ninazidi kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia ninampongeza kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Joel Arthur Nanauka, nikitambua kwamba ni Mbunge kwa mara ya kwanza, ni Waziri mara ya kwanza na Wizara pia ni mpya kwa mara ya kwanza, lakini ameonesha weledi yeye pamoja na watendaji wote anaofanya nao kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwa kuwa ni wapya, bado wapo katika kutengeneza na kuboresha *system* za kuweza kuwatumikia vijana. Ila amekuwa mchapakazi kweli kweli, na hata sisi vijana wenzie tunajivunia uwepo wake, na tunaona imani ambayo Rais amempatia, hajakosea. Tunashukuru sana kwa jinsi anavyotuwakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo nimeguswa nalo sana katika bajeti ambayo kaka yangu Joel, amei-*present* leo ni kwamba, katika bajeti ya 2024/2025 vijana tukiwa tu kama Idara, fedha ambazo tulitengewa kwa ajili ya maendeleo ya vijana ilikuwa ni shilingi bilioni moja pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ndugu yangu Waziri Joel Arthur Nanauka, ametusomea hapa inaonesha tunaenda kupewa takribani shilingi bilioni tano, ambayo ni sawa na ongezeko la 80%. Hii ni dhati Dkt. Samia Suluhu Hassan nia yake ya ukweli ya kuwezesha vijana inazidi kuthibitika siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, ukiangalia pamoja na ku-*present* jambo hili, pia kulikuwa na suala la kanzidata. Ni moja kati ya mambo ambayo yamekuwa yanaongelewa mara nyingi sana. Tunawezaje kupanga kusaidia vijana ikiwa hatuwatambui? Leo Waziri wa Maendeleo ya Vijana amekuja hapa na ametuhakikishia tutakuwa na kanzidata ambayo itatambua vijana wetu na itaweza kuhakikisha inawaunganisha na fursa ambazo zinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye ushauri. Kulingana na hayo yote ambayo yamezungumzwa na mazuri mengi, sema tu ni muda umeisha, lakini yapo mengi ambayo natamani niendelee kuyaongelea. Kwa kuwa, nina imani na Wizara husika ninaomba sasa nishauri kwa wepesi sana na haraka mambo machache tu ambayo ninaamini yatazidi kuboresha mambo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kwamba tunayo Sheria ya Manunuzi ya Umma; pamoja na kwamba imetengwa hii 30% lakini ni ukweli usiopingika bado kuna taasisi za umma hazifikii hiyo 30%. Nimwombe Waziri wa Maendeleo ya Vijana, kwa namna ambavyo amekuwa mchakarikaji, tafadhali tushirikiane na Ndugu zetu wa *VETA* ili tuongeze vikundi vingi ambavyo vitakwenda kuomba fursa hiyo na kuweza kusaidia vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nimeona Ndugu yangu ameweza kuongea hoja ambayo ni agenda ya

muda mrefu sana ya kuanzishwa kwa benki ya vijana, nimwombe Waziri wetu wa Maendeleo ya Vijana, hizi fedha ambazo zitakuwepo ambazo tutapatiwa shilingi bilioni tano, sambamba na hizi shilingi bilioni 200 ambazo Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeomba zirudishwe katika Wizara husika. Ninaomba zitumike pamoja na kuanzisha benki yetu ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hekima yangu inanituma kwamba watendaji wetu wa Wizara ya Vijana siyo *bankers*, siyo *loan officers* wao wapo pale kutengeneza mazingira rafiki ya kuwawezesha vijana kuweza kufikia malengo yao. Tunapokuwa tunajikita wao ndio wawe wakopeshaji, ndio wawe wafuatiliaji, ndio tena wabadilike wawe chombo cha fedha, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kushauri kwamba Wizara ya Vijana ibaki Wizara ya Vijana na isigeuzwe kuwa taasisi ya fedha. Hivyo, tutengeneze benki yetu ambayo itakuwa ni taasisi ya fedha, ishughulike na changamoto za vijana kama kutoa elimu ya mikopo, kuwafundisha vijana namna ya kuweka maandiko kwa ajili ya kutengeneza miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyong'ang'ana kuendelea kuwaachia na kuwatwika mzigo huu watendaji wetu, ndiyo maana tunatengeneza *loan defaulters* wengi. Tunaweza kuzungumza hapa fedha zitoke, zitoke, je, zinarudije? Fedha zetu zile hazitoki ili mtu aende atumie na ziwe za kwake. Ni fedha ambazo ni *revolving fund*, mtu anatakiwa apewe, atumie, arejeshe ili na wengine waendelee kupewa. Kwa hiyo, ninaendelea kuhimiza Waziri wetu wa Maendeleo ya Vijana, ajikite katika hii ndoto ili itimilizike, vijana tuweze kuwa na benki yetu ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuongezea jambo lingine katika mitandao ya kijamii. Waziri wa Maendeleo ya Vijana, amempongeza kijana mmoja ambaye anafahamika zaidi kwa jina la Leon Mendez, jina lake halisi ni Leodiga Kachebona. Kama tuna vijana ambao wanakuwa na mawazo makubwa na ya msingi kama haya wanaweza kutambulika *East African Youth Award*, wanaweza kutambulika Ghana Accra, kuna dhambi gani

wakatambulika na sisi hapa kwetu nchini, na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akaalikwa kama mgeni rasmi ili aone juhudi zake, upendo wake na yale yote anayoyafanya kwa ajili ya vijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana kweli tupo tayari na tunahakikisha kweli tunayafanyia kazi. Kwa hiyo, ninakuomba Waziri wa Maendeleo ya Vijana, Tanzania tuanze kutoa tuzo maalumu ya kutambua mawazo bora na ya msingi ambayo vijana wetu wanayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kumalizia japo siyo kwa umuhimu, nilikuwa ninaomba, pamoja na kwamba Serikali yetu inashughulika usiku na mchana kwa kushirikiana na sekta nyingine zote kutatua changamoto ya vijana. Ni changamoto mtambuka na Wizara ya Vijana pekee haiwezi kumaliza hilo tatizo. Tunaamini na sekta nyingine pia zinaendelea kutoa ushiriki wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri wa Maendeleo ya Vijana, tuangalie namna taasisi zinazoongozwa na vijana, ambazo ni *Non-Governmental Organisation* wanajitolea kuweza kutoa elimu za fedha, kuweza kuunganisha vijana, kuwaelimisha katika uongozi, lakini bado hawana uwezo wa kifedha, bado hawana mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa Wizara hii iwe na mkakati maalumu wa kuangalia ni jinsi gani hizi *non-governmental organisation* zinazoongozwa na vijana, zinaweza walau kusaidiwa ruzuku, ama mafunzo ili ziendelee kusaidia nguvu kubwa hii ambayo tunaona Wizara ya Maendeleo ya Vijana kwa kuongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joel Arthur Nanauka, inakuwa inafanya mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ninaona kwamba ni jambo la heri sana tukiendelea kushirikiana kwa dhati ya mioyo yetu ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya mioyo yetu kuendelea kulitengeneza Taifa letu, maana sisi ni leo, na ni kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ninamwita sasa Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa, Mheshimiwa Yumna Omar, atafuatia Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka.

**MHE. BENG'I M. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nami ninapenda nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama wengine walivyosema, kwa kuanzisha Wizara hii, limekuwa ni jambo la kimkakati, na kwa kweli litatusaidia sana kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninapenda niwapongeze kwa dhati kabisa Wizara ya Maendeleo ya Vijana kwa hotuba nzuri na mikakati ambayo wameipanga ya kuendeleza masuala ya vijana hapa nchini. Ninampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Nanauka, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya tangu alipoteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sasa nichangie hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2026/2027. Ninapenda nijikite kwenye muundo wa utekelezaji. Unapokuwa na Wizara mpya kama hii ambayo imeanzishwa sasa hivi, na wakati tayari kulikuwa na Wizara nyingi zinafanya mambo ya vijana, mambo mengi yanakuwa ni magumu mara nyingine kuyatekeleza kwa sababu ni ngumu kumnyang'anya mtu mara moja kitu anachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa sababu ni Wizara ambayo inalenga Kundi la wananchi fulani, ni ngumu pia kusema kwamba kazi zote zitafanywa na Wizara hii, kwa sababu tayari kuna Wizara zinafanya kazi na vijana na ni vizuri wao wakaangalia

jinsi ambavyo wataji-*network* au watajipanga kufanya kazi na Wizara mbalimbali kwa kuzipa miongozo na kuhakikisha kwamba wao wanapata taarifa zote za utekelezaji na kuongoza vizuri masuala ya vijana ambayo yanafanywa na Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ambalo tumeliona muda mrefu katika masuala ya vijana, tumezungumza mambo mengi kwa kweli, masuala ya ajira ambazo hazina uhakika, ajira za *informal sector*, suala la uzoefu imekuwa ni tatizo kubwa. Mara nyingi vijana hawapati kazi kwa sababu hawana uzoefu, vilevile ujuzi na maarifa ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wa Kitanzania wanaweza kuwa na ujuzi, tunasema *technical skill,* lakini wakakosa *soft skills*. Hiki ni kitu ambacho ni muhimu sana Wizara ikakiangalia, kwa sababu unapokwenda kufanya kazi, unaweza kuwa unajua kazi, lakini usijue kujiongeza, usijue labda *customer care* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo kwa sababu hawa ni vijana, na vijana ni wachanga, wanakuwa bado hawajawa *exposed* kwenye vitu vingi, na kuna vitu vingine hawavifahamu kabisa. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na *programs* ambazo zitasaidia kujenga tabia zao vizuri na kuongeza ujuzi ambao unahitajika ili wawe vizuri katika vitu ambavyo wanavifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jambo la upatikanaji wa taarifa ni tatizo kubwa. Hii siyo kwa vijana tu, ni kwa wananchi wengi tu ambao wanahitaji fursa zinazoletwa na Serikali. Kwa hiyo, nimefurahi kusikia kwamba kutakuwa na kanzidata vilevile kuwepo na utaratibu ambao utawafanya vijana wapate taarifa kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mikopo ambayo imetangazwa hivi sasa, na hata zabuni ambazo zinatolewa kwa vijana, sasa hivi bado hawajui wanazipata namna gani? Kwa hiyo, utaratibu wa upatikanaji wa taarifa, lazima utengenezwe na uwe rafiki kuwafikia vijana kwa utaratibu ambao unatakiwa,

ambao utasaidia kuwaleta kwa wingi zaidi katika fursa ambazo zinatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa vijana ndiyo ambao ni wabunifu kwa kiasi kikubwa. Tunao vijana wabunifu wengi sana hapa nchini, lakini kumekuwa hakuna utaratibu wa kuwatoa kwenye ubunifu kuwapeleka kwenye kufanya biashara. Mtu anaweza akabuni jambo lake zuri, lakini anakosa ujuzi kwa kutoa ule ubunifu kufanya ile *product* ikawa *product* na ikauzika kibiashara. Haya ni mambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tulikuwa na tatizo kubwa la biashara zinazoanza *(startups)*. *Startups* nyingi zilikuwa hazipati mitaji, kwa sababu kila anayetoa mtaji alikuwa anataka uzoefu na vijana wetu walikuwa hawana uzoefu, lakini kuanzishwa kwa Wizara hii kumeleta chachu ya kuangalia hili suala kwa upekee na tunafikiri kwamba kwenye *startups* tutaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo tu ni kwamba, katika utoaji mikopo na kum-*finance* mtu ambaye anaanza biashara kuna *risk* kubwa, kwamba unaweza ukatoa fedha na isirudi. Kwa hiyo, ni vizuri sana hawa vijana wakawa na programu za kuwasaidia kujenga tabia zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia tabia hapa, nina maana kwamba tuwe na programu za malezi kwa wale ambao wanafanya biashara ambao ni wazoefu, wawekwe na wafanyabiashara vijana ili kuwafundisha tabia nzuri za kufanya biashara ambayo kwa Kiingereza tunaita *mentors*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na *mentorship program* kwa kushirikiana na taasisi kama hizi za biashara *TWCC* au *TCCIA* tutawapa vijana. Kila kijana atakuwa anapata mtu mzima ambaye anaweza kumlea katika shughuli ambazo anafanya za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni masuala ya uvumilivu. Vijana mara nyingi sio wavumilivu, na hili jambo ni lazima wafundishwe kwamba mafanikio hayaji kwa urahisi. Mafanikio yoyote yanahitaji *struggle*, upitie ugumu ili uweze

kufanikiwa. Kama hawaambiwi, hawawezi kujua kwamba lazima upitie mambo magumu, uvumilie, mara nyingine ukae muda mrefu bila kukipata hicho ambacho unakitaka, lakini mwisho wake utakipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni nidhamu ya fedha. Nidhamu ya fedha ni tatizo kubwa sana. Watu wengi tunapenda fedha, tunataka mikopo, lakini hatuna nidhamu ya hizo fedha. Kwa hiyo, tufundishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna programu nyingi, ninakumbuka Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ina programu kabisa ya elimu ya fedha. Kwa hiyo, ni vizuri sana vijana wetu wafundishwe nidhamu ya fedha, kuweka akiba, kuwekeza na fedha izae ilete matokeo chanya katika shughuli ambazo anazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni vitu muhimu sana tukiweza kufanya, hata Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao sasa umehuishwa vizuri na unatoa mikopo, utaendelea kushamiri kama vijana wetu watakuwa na nidhamu ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar, Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka atafuatia, Mheshimiwa Ali Hassan King, ajiandae.

**MHE. YUMNA MMANGA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na uzima na kutujaalia sote tukiwa hapa leo tukiendelea na majukumu yetu ya kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na vijana wenzangu kwa kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan sambamba na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuanzisha Wizara hizi ambazo zinagusa mahsusi maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, na mimi niende moja kwa moja katika hoja iliyopo Mezani. Wakati ninasoma hotuba hii ya Waziri, nimeona kwamba ameomba shilingi milioni 35 kwa ajili ya utekelezaji wake wa mwaka 2026/2027, lakini 83% ya fedha hizi zinakwenda kwenye uendeshaji ikiwemo mishahara na *OC* na 17% zinakwenda kwenye uwezeshaji wa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu ni kwamba, kama Wabunge wenzangu waliotangulia kusema, fedha hizi shilingi bilioni 200 ambazo zimetolewa kwa maendeleo ya vijana zingeletwa kwenye Wizara hii zikaweza kuratibiwa vizuri. Kuzipeleka kwenye Wizara nyingine, inasababisha *fragmentation* ya *activities*, ujasiriamali na kupelekea kutokupimwa, ufanisi wa upimaji wa matokeo wa hizi fedha kuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *inclusivity* ya uwezeshaji inaweza kupungua kwa sababu tunatambua Wizara hizi za sekta ziko zaidi katika uzalishaji, siyo uwezeshaji wa vijana, na sisi vijana wa Kitanzania tunataka kuwezeshwa na siyo kuendeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, niseme tu kwamba, moja ya malengo la Wizara hii ni kuongeza kuhamasisha vijana kushiriki kwenye nafasi za uongozi kuanzia ngazi za Taifa hadi kata. Hii ameanza kumdhihirisha Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuanzia Baraza lake la Mawaziri, humu ndani ya Bunge, pamoja na maeneo mengine ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu hii imezindua kamati ya utekelezaji wa kusimamia programu za uwezeshaji wa vijana ikiwemo *Hub Challenge* na *Idea* Kitaa. Kamati ile haina uwakilishi wa vijana wenye ulemavu. Hatulilii uwakilishi, tunalilia *meaningful participation,* kwa sababu ni sisi ndio tunatambua pilipili inatuwasha kwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sisi ndio tunatambua kiatu kinatubana kwa namna gani? Ni sisi tunatambua changamoto zetu na namna gani ya kwenda kuzitatua. Kwa maana hiyo, basi

hata ile fomu ya maombi ya kwenye programu hii, inapokosa kipengele cha ulemavu, ni kipengele kidogo, lakini *impact* yake ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kukosekana kwa kipengele hiki, tunaweza kukosa takwimu sahihi ni vijana wangapi wenye ulemavu wamefikiwa na taarifa ya fursa hii? Ni vijana wangapi wenye ulemavu ambao wameomba fursa hii? Ni vijana wangapi wenye ulemavu wamepatiwa fursa hii? ni vijana wenye ulemavu wa aina gani wamepata fursa hii? Vivyo hivyo, kutokana na ukosefu wa takwimu hizi tunashindwa kupima matokeo halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ulimwengu wa sasa ambao ni *data driven decision making,* ukitutoa kwenye nafasi ya maamuzi, maana yake umekusudia kwa madhumuni mazima kutoa kwenye matokeo. Hivyo basi, ninaiomba Wizara ikaangalie namna inavyokwenda kutushirikisha sisi vijana wenye ulemavu kwenye nafasi hizi, na pia nafasi ya kurekebisha ile fomu kwa matokeo mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara imeanzisha makongamano mbalimbali ambayo yanakutanisha vijana sehemu mbalimbali kujadili fursa na changamoto. Makongamano haya ni kwa namna gani yanajumuisha vijana wenye ulemavu *in terms of* miundombinu na kufikiwa na taarifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya makongamano mijini na vijijini, ni lazima tuhakikishe tunaweka mazingira ya kwenye kivuli, yaani miundombinu rafiki ili vijana wenye ulemavu wa viungo waweze kufika, na pia wakalimani wa lugha ya alama ili ndugu zetu wenye ulemavu wa uziwi waweze kupata taarifa na kunufaika na fursa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mapendekezo yangu kwa Wizara kuona ni namna gani wanaweka jitihada za makusudi za kuweza kuhakikisha kuwa nasi vijana wenye ulemavu tunatufaika kwa 100% kwenye fursa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukaweka *specific intervention*. Kama ni mashindano, tunaweka mahususi kwa vijana wenye ulemavu; na yapo yanaendelea. Tarehe 7 Machi, nimehudhuria Programu ya Wazo Bora, *Pitch Programme,* ambayo vijana wenye ulemavu wameshindanishwa mawazo yao, *ideas* zao za ubunifu na washindi watatu walipewa zawadi. Shindano hili lilianzishwa na *Standard Chartered Bank* wakishirikiana na *Side Saver Organization.* Taasisi hizi zipo, na sisi kama Serikali tuna nafasi kubwa ya kutekeleza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawasilisha hoja na ninakubaliana nayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba, ajiandae.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema kubwa ya kuendelea kuwepo hapa tukiendelea kulijenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia kwa heshima kubwa na unyenyekevu, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, kaka yangu Mheshimiwa Joel Nanauka. Mosi, kwa kazi nzuri aliyoanza nayo ya kuitumia Wizara hii ambayo ni mpya; na la pili, kwa uwasilishaji mzuri ambao umebeba mapana na maono makubwa kwa ajili ya vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mpya, na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliamua kuianzisha makusudi ili kuweza kulipa nguvu Taifa la vijana walio wengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivi ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, anaweza asituone kwenye gari lake analopanda, anaweza asituone kwenye meza yake pale ofisini, anaweza asituone kwenye majukwaa mbalimbali ndani na nje ya nchi, lakini tunafikiri pamoja na yeye, tunawaza pamoja na

yeye, tunaamua pamoja na yeye na tuongoza pamoja na yeye. Kwa lugha nyepesi, vijana wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuko pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa ya vijana kuweza kulitumikia Taifa hili iliasisiwa tangu kuanzishwa kwa Taifa hili, lakini tumekuwa na vipindi kadhaa ambavyo tumekuwa tukiitazama fursa rasmi ya vijana kuweza kushiriki moja kwa moja kwenye kuleta matokeo chanya. Hii ni kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na dunia inavyokwenda sasa, na pia vijana wameongezeka, uhitaji umeongezeka, na tumekuwa na mahitaji makuwa ya kuingia kwenye maeneo mahususi ili kulijenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ni ukweli usiopingika kwamba hata kama tukiwa na nguvu ya kiasi gani, hatuwezi ku-*satisfy* mahitaji ya vijana kwenye soko la ajira tukawamaliza wote. Hiyo haiwezekani, lakini sisi kama nchi tunaweza kuwa na mipango mikakati na mwelekeo utakaowezesha vijana wetu kupata unafuu wa kuwa katika majukumu ya kila siku. Jambo hili ndilo dira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuanzisha Wizara ya Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina makundi mbalimbali ya vijana, na mimi nimekuwa muumini ninayeamini kwamba ni lazima tukatae dhana ya kuamini kwamba liko kundi la vijana linahesabika kama bomu. Makundi yote ya vijana nchi hii ni fursa, makundi yote ya vijana nchi hii ni ya uzalishaji, makundi yote ya nchi hii ni tegemeo la Taifa kwenye usalama wa nchi, uzalishaji na mwelekeo wa *free country. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi haya yote Serikali imedhamiria kuyaweka kwenye mwelekeo wa kuleta matokeo. Kundi la bodaboda tunalifikia, makundi ya machinga tunayafikia, makundi ya wachimbaji tunayafikia, makundi ya wakulima na wajasiriamali wote wenye ngazi ya ujana na kuelekea utu uzima kazi hii inafanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba sisi tuko tayari kabisa kumsaidia na kumshauri. Tunamwombea kwa Wizara zote zilizoko nchini zimfungulie milango aingie kwenye kila Wizara anayotaka. Wizara hii ni kama mtoto wa mwisho ambaye anaita kaka kushoto; anageuka, dada kulia, anageuka; mama mbele, anageuka. Atakwenda Wizara ya Madini kuna fursa za vijana afunguliwe milango ili vijana wapate manufaa. Tunayo Wizara ya Kilimo, kuna *irrigation schemes* nyingi nchi hii, afunguliwe milango ili vijana wapate fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua ziko Wizara nyingi. Wizara ya Michezo ina wasanii, ina wacheza mpira, na ina wanamitindo. Hawa wote wako chini ya uratibu na usimamizi wa Wizara hii ya Maendeleo ya Vijana. Kwa hiyo, tuko hapa kuunga mkono Wizara hii, na pia kuondoa hofu kwa vijana, kwamba sasa wamepata mwarobanini wa masuala yao kuweza kujadiliwa kwa kina na kupatiwa utatuzi unaoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nishauri maeneo machache. Eneo la kwanza ni eneo la viwanda. Utakubaliana na mimi kwamba nchi zote duniani ziliweza kufanya mapinduzi ya viwanda vidogo na vikubwa, walisaidia sana kupunguza ombwe la vijana waliokosa ajira. Kwa wale ambao wanasafiri kwa barabara ya kusini kuelekea Mkoa wa Lindi, wataona unapopita Mkuranga pale kuna viwanda. Ukipita usiku, ukipita mchana utaona idadi ya watu wanaokwenda kiwandani kupishana ili kufanya shughuli za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lile linawezekana, na Wizara hii ina nguvu ya kufanya hivyo. Sisi tunaamini, kwamba kwa uwezo wa Waziri aliyeteuliwa, maarifa yake, uweledi wake, *exposure* aliyonayo, hawezi kuchoka kutafuta namna ya vijana kuingia kwenye soko la ajira kupitia viwanda mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena eneo la pili katika ushauri, bado ninasisitiza eneo la kutazama juu ya kodi na mlolongo wa tozo nyingi katika shughuli za vijana. Vijana wanaoanza kutengeneza ujenzi wa Taifa hili wanaanza na mitaji midogo sana. Wanachohitaji wao ni fursa ya kufanya shughuli zao ili kufikia miradi mitaji mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema kwenye Bunge hili, tupunguze baadhi ya tozo na baadhi ya kodi kwenye fursa za vijana kwenye ajira zao ikiwemo waendesha bodaboda. Tulishaomba na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, alifanya kongamano kubwa ambalo lilikuwa na mgeni rasmi Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vijana walileta hoja zao. Moja ya hoja kubwa waliyoleta ni pamoja na tozo hizi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunao Wamachinga, bado ninaamini kwamba tunaweza kukusanya kidogo tukapata kingi na kila kijana akawa *motivated* kufanya kazi ya kiuchumi. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tufanye mapitio vizuri kabisa ili kwenda kuona kundi lile la machinga tunapotaka kukusanya kutoka kwao, tunakusanya kwa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hoja ya vitambulisho ilikuwa ni hoja nzuri na ilisaidia kupata kwa usahihi na kwa wingi, tuifikirie, lakini kama iko njia nyingine kupitia makundi na kupitia *platform* walizoziweka, basi ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tushirikiane kwenye hili ili kuona fursa zao kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelekea kumaliza mchango wangu. Sasa nchi hii imejengwa vizuri sana, na moja ya jambo kubwa ambalo watu wanalipigania ni siasa na maendeleo. Hata hivyo, na mtanisaidia, imekuwa tofauti kidogo. Wako wenzetu wengine wameichagua siasa kuyatia masikio ya vijana kauli zenye maumivu badala ya kauli zenye matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapa kuwaomba vijana wa nchi hii, kwanza wawe na imani na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia. Pili, wajue kile tunachokifanya ni kwa ajili yao. Kwa bahati nzuri, niruhusu niseme kwa heshima kubwa sana, kwamba kaka yangu Mheshimiwa Ado Shaibu, yuko hapa ndani mtu ninayemheshimu sana, kwa sababu yupo kwenye chama kikubwa cha kisiasa chenye kusika ndani na nje, basi mimi na yeye na Wabunge wengine tusaidiane, tunapotoka nje kwenye *platform* zetu tuwaambie vijana juu ya kauli zinazoleta matumaini na siyo kuwalazimishia maumivu ambayo nchi haijachagua kuyafanya. Moja kati ya hayo, ni kutokuwatenga na mipango, sera na mwelekeo wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninakushukuru. Nimwite sana Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba, Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninakushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi. Nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimesoma randama vizuri, nimesoma sheria zinazoendana na jambo hili, na nimesoma matoleo tofauti tofauti na nimeona sasa niishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama ya Fungu 104 katika *page* ya nne ambayo wameelezea dira na dhima; dira inasema kuwa na vijana wenye ujuzi, halafu yanaendelea mengine. Dhima inasema, kuweka mfumo wa ufanisi wa kitaasisi, lakini mwisho wakataja kwamba, kuwapa vijana ujuzi husika. Sasa lengo langu mimi nililokusudia kuzungumza, ninataka kuzungumzia kukuza ujuzi wa vijana kwa ajili ya kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma vitu vyote, pamoja na ile ya Waziri Mkuu ambayo inashughulikia kazi, ajira na mahusiano, nimeona kwamba kuna upungufu katika Wizara hii. Upungufu wenyewe Mheshimiwa Waziri mwenyewe ameutambua na ameutaja *page* ambayo ameeleza katika hotuba yake. Tukiacha idara au kitengo cha kukuza ujuzi kwa ajili ya kupata ajira, hapo ndipo tumewaacha vijana, maana hakimo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama, utakuja kukuta katika *core functions* zake ni uratibu na uhamasishaji wa vijana, elimu ya uraia na uzalendo na uratibu wa mwenge, ukuzaji biashara na uwezeshaji vijana kiuchumi; na nyingine ustawi wa makuzi ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lalamiko letu kubwa lilikuwa ni ajira kwa vijana, na ajira huwezi kupata bila ujuzi. Kama huna ujuzi, ajira huna, na hiyo amesema mwenyewe Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 10 *paragraph* ya 13 alipotoa takwimu za kwamba vijana ni milioni 20.6 kati ya waajiriwa walioajriwa milioni 26. Vijana wa kutoka miaka 15 mpaka 35 wako milioni 20.6, ukitazama, wengine ni milioni sita. Maana yake ni kwamba vijana wanahitaji wawezeshwe zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba kuna ukosefu mkubwa wa ujuzi kwa vijana, kwamba hii ni changamoto. Pia akesema kwamba ujuzi wenyewe ni ambao unaendana na soko. Kwa maana hiyo, kazi ya Wizara hii sasa watuletee ujuzi unaoendana na soko, hatutaki waratibu wafanye wao. Kwa nini wasifanye wao? Farasi huyu ni wake mwenyewe Mheshimiwa Waziri, anakaaje mkiani? Vijana na ajira ni wake. Hilo ndilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama changu kimeahidi katika Ilani kuwapatia ajira watu 8,500,000. Kutoa ajira hizo anafanya kama anamnyooshea kidole mtu yuko Uingereza, yeye yuko Tanzania. Anampandisha mtu shetani wa Uingereza kwa kunyoosha kidole, anampataje? Achukue hiki kitengo kiwepo kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo hiki ni muhimu, kwa sababu ukitazama hivi vitengo vyote nilivyovitaja, *investment* yake ni shilingi 5,383,000,000, kitu kama hicho; lakini akichukua hiki cha kukuza ujuzi kwa vijana *investment* yake ni shilingi bilioni 9.7, takriban mara mbili zaidi; ni zaidi ya 200%. Kitengo hiki akikiacha ina maana kwamba tutakwenda tofauti na dira. Dira yetu inatutaka kuwafanya vijana wawe na ujuzi ili uchumi tuliou-*target* tuweze kuufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nizungumzie kitu kimoja. Ni kwa nini kukawekwa programu ya kukuza ujuzi? *ATE (Association of Tanzania Employers)* walikaa wakakubaliana na Serikali, kwamba iwepo *Skills Development Levy,* ichajiwe kwa ajili ya kukuza ujuzi, na hii *one third* itakwenda kwenye kukuza ujuzi na vingine vitakwenda katika elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa makubaliano hayo *ATE* wao watapewa *gap* ya *skills* ambayo ipo na Serikali i-*finance* kupitia *Skills Development Levy* kuwasomesha watu ili tupate ujuzi unaotakiwa, maana kama kiwanda kimekosa ujuzi, ina maana tuna-*import labour.* Sasa ili tusi-*import labou,r* tuwape ujuzi vijana wetu. Tutakapowapa ujuzi, hapo ndipo tutakapozifanya hizi kazi wenyewe. Vinginevyo hatutaweza kupata ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, *page number* 15 ametaja hapa programu ya kukuza ujuzi ambayo inafanyika kule katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, kwamba, ukijumlisha namba zote tatu unapata; kwa mwaka 2025 waliofanyiwa huo ujuzi ni watu 16,000. Hii ni namba ndogo sana. Kwa nini, hili jambo asiwe nalo yeye? Akiwa nalo yeye anaweza akalifanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai, kwa kuwa tozo hii imewekwa, tuipeleke. Kama hatujaipeleka, ina maana kwamba tutakosa kuwapatia vijana wetu ujuzi na tutakosa kuwapa vijana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza kitu kimoja, nini maana ya kukuza ujuzi? Kukuza ujuzi maana yake ni kwamba vile *gap* zilizokuwa zimepatikana viwandani wapatikane wataalamu wasomeshwe. Wakishasomeshwa, zile kazi tunakaa sisi wenyewe. Kama kazi hizi hatujakaa sisi wenyewe, ina maana moja kwa moja tunapoteza, na ajira hizo tunazipeleka kwa watu wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya vijana. Watu wengi wanazungumza falsafa za kuhusiana na vijana. Kuhusiana na vijana, mimi nina falsafa moja. Nabii Musa, watu wote wanamjua; katika Biblia, ni Musa. Katika Quran, Mungu anasema, "*Famaaa aamana li-Moosaaa illaa zurriyyatum*", hawajamwamini watu wote Musa isipokuwa vijana ndio walimwamini. Musa alishinda na vijana, na nchi hii tutashinda tukiwakamata vijana, maana kila mwenye lake analitupa kwa vijana, lakini sisi tunaweza tukawatumia vijana wetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kitu kimoja kwa kumalizia ili niweze kuunga mkono hoja. Mimi ninasema, "*Tanzania*

*ndipo kwetu, hatuna kwingine katu, Asitudanganye mtu, kujenga wajibu wetu, kwa nguvu na jasho letu, tuishi kama wenzetu." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kitengo cha kukuza ujuzi kiwepo kwa Mheshimiwa Waziri wa Vijana, hapo ndiyo atakuwa ana Wizara kamili. Kama anaratibu, akiratibu kwa mbali hawezi kuratibu hivyo. Wengine wanaweza wakaratibu, na wana sekta. Kilimo wana sekta, uvuvi wana sekta, sasa wanaenda kumratibu Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tutizame, unaenda kumratibu Waziri Mkuu? Sasa hili ninaona halijakaa vizuri. Hiki kitengo kichukuliwe, kwa sababu Wizara zote hata kama TAMISEMI, *whether* itawekwa Ofisi ya Rais au itawekwa kwa Waziri Mkuu. Sasa hii ipo kwa Waziri Mkuu, unaenda kuiratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi juu ya hili. Ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa, nimwite sasa Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas.

**MHE. SAID IBRAHIM MZIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ni mara yangu ya kwanza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kunifikisha hapa kwa sababu hakuna jambo lolote chini ya jua linalowezekana bila idhini ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nikishukuru chama changu cha *ACT*-Wazalendo kwa kuniamini na kunipa heshima ya kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Said Ibrahim Mzimba kwa mujibu wa kanuni zetu, hutakiwi kusoma, unatakiwa kufanya rejea tu kwenye hiyo *document,* lakini siyo unasoma, endelea.

**MHE. SAID IBRAHIM MZIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtambile kwa imani walionionesha kwa kunichagua kwa kura nyingi. Ninaahidi mbele ya Bunge hili na mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachangia kuhusu Baraza la Vijana Tanzania. Kuna umuhimu mkubwa wa kuanzishwa kwa Baraza la Vijana Tanzania. Ninafurahi kwa kuwa nilimsikia Waziri akizungumzia jambo hili, lakini ninataka nimwambie, hakuna wakati ambao Tanzania inapenda kuwa na Baraza la Vijana kama wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna wakati ambao vijana wa Tanzania wanapenda kuwa na Baraza la Vijana kama wakati huu. Kwa hiyo, ninaomba, kuweka msisitizo, na katika baraza hilo ninaomba katika uundwaji wake kusiwe na pingamizi ya siasa, kidini, wapi unatoka, au jinsia. Baraza hili liwe chombo cha kuwaunganisha Watanzania na vijana wetu wote kwa sababu sisi ndio tuliowazaa, na tuliowalea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wanahitaji umoja wetu na mshikamano wetu ili kuliendeleza Taifa kwa hivi sasa, maana yake tumezoea kuwaita vijana ni Taifa la kesho, lakini kwa hivi sasa, kwa wakati huu vijana ni Taifa la hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nichangie kuhusu shilingi bilioni 200 zilizowekwa na Rais wa Tanzania. Ninaunga mkono hii hoja ya Rais wetu kuweka fedha hizi, lakini sasa utekelezaji wake una changamoto kubwa kwa sababu hizi fedha zimetawanywa kwenye Wizara mbalimbali: Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Uvuvi na Wizara ya Viwanda na Biashara. Sasa usimamizi wa hizi fedha sijui utakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, hizi fedha zikusanywe, zirudi kwenye Wizara ya Vijana kwa sababu Waziri wa Vijana ndiye aliyekabidhiwa bango la lile hundi. Kwa hiyo, vijana wote wa Tanzania fedha hizi wanajua kuwa anazo Waziri wa Vijana. Kwa hiyo, zirudi hapa ili ziweze kudhibitiwa, kwa sababu

zikiwekwa kwenye Wizara ya Mifugo, au Wizara ya Biashara, nani atakayekuwa mdhibiti wa fedha hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba, Waziri wa Vijana ndio awe msimamizi wa fedha hizi, zikigaiwa kwenye sehemu mbalimbali, uwezekano mkubwa wa matumizi yasiyo na tija yatapatikana, pia ugumu wa ufuatiliaji wa matokeo utapatikana. Ninapendekeza fedha hizi zirudi kwenye Wizara ya Vijana na masharti ya mikopo siku zote jamani, anayetaka kusaidiwa ni yule aliyekuwa hana kitu. Utamsaidiaje mtu ambaye ana chanzo, umwache mtu ambaye hana kitu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba haya masharti ya kuwa lazima uwe na mtaji ndiyo uweze kupata mkopo huu, yaondolewe kwa sababu tutawafungia milango wale wahusika ambao walitakiwa kupata fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli tuseme, vijana wetu wa Tanzania wengi hawana ajira, na wengi hawajapata mwendelezo wa kibiashara. Kwa hiyo, unapozuia ukasema lazima wenye mitaji ndio wapewe fedha hizi, tutakuwa hatuwatendei haki wale ambao ndio wanajikusanya hivi sasa waanze kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wengi wa Tanzania ni wale ambao wanajitafutia riziki ya kula leo, kesho atoke. Kwa hiyo, ninaomba hili tulizingatie kwa mapana makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa sababu ya ufinyu wa muda, ninaomba, sisi *ACT* – Wazalendo, tumefanya uchambuzi mkubwa sana wa hoja hii ya vijana. Kwa hiyo, tutawasilisha kwa maandishi kwenye Ofisi ya Waziri ya Vijana na Maendeleo ya Vijana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaenda kwa mchangiaji wa mwisho, kabla ya mtoa hoja, ndani ya Bunge letu tuna mgeni ambaye ni mgeni wangu. Huyu ni Ndugu Nicas Nicodemus, Mjasiriamali kutoka Njombe, karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo ya Vijana. Pia ninapenda kuanza kwa andiko moja kutoka Waraka wa Kwanza wa Yohana 02:14 ambao unasema, "*Nimewaandikia ninyi vijana kwa sababu mna nguvu.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu lina vijana wa kutosha 34% ya *population* ambao wana nguvu na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa na kizazi ambacho kina nguvu ndani ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana ambao Biblia inasema tunawaandikia, na kwa kuwa wana nguvu; Biblia inasema kwamba, pia wamejaa Neno la Mungu. Nami ninasema, wamejaa pia maarifa, ujuzi na uwezo wa kuchangia maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema kwamba hawa vijana wetu ni rasilimali na ni fursa kwa ajili ya nchi yetu na wao wenyewe. Kwa hiyo, ninapenda kuanza na andiko hilo na kusema kwamba tutambue rasilimali hii kubwa ambayo nchi yetu imejaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba pia hawa vijana wetu wanachangia asilimia kubwa sana ya nguvu kazi, zaidi ya 55%. Kwa hiyo, kama nchi kwa kweli ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutambua kundi hili la vijana ambao ni zaidi ya 34%, kwa kuliundia Wizara kabisa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana wetu wametawanyika, wapo vijijini na mijini. Vilevile, wana elimu tofauti, wengine wamemaliza darasa la saba, wengine hawajamaliza, wengine wapo *Form Four*, wengine vyuo, ngazi mbalimbali za elimu. Lazima tuwatambue na kuwapa fursa sawa za kuweza kuwaendeleza na kuweza kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutambua mchango huu, Rais amefanya kazi kubwa, ndiyo maana ametoa ajira 12,000, ajira 5,000 sekta ya afya na 7,000 sekta ya elimu. Bado tumesikia juzi katika mwaka unaokuja zaidi ya 45,000 watakwenda kuajiriwa katika mwaka unaokuja. Kwa kweli ni mchango mkubwa sana ambao Serikali inaendelea kutambua nguvu kazi hii ambayo inakwenda kutumikia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kuunga mkono Wizara hii na kazi ambayo inaifanya. Ninapendekeza mambo machache. Jambo la kwanza, katika kupitia tumeona kuna vitengo vingi sana, lakini ningependa kupendekeza kwamba mahitaji ya vijana yanabadilika muda hadi muda, hivyo kuwepo na kitengo cha utafiti na ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya vijana yanabadilika sana, na vilevile vijana wetu ni wabunifu na wana talanta mbalimbali. Kuwe na kitengo ambacho kitatengewa fedha ili tuweze kutambua mahitaji ya vijana kadiri muda unavyokwenda, na pia umri wao unavyobadilika na mahitaji yao kutoka eneo hadi eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo hiki pia kitatambua namna ya rasilimali fedha inayotengwa itakavyogawanywa. Mahitaji ya kijana wa Ilala ni tofauti na mahitaji ya kijana wa Nkasi na mahitaji ya kijana wa Nkasi ni tofauti na mahitaji ya kijana wa Mbulu. Kwa hiyo, tuweze kuona tusije tukaweka kwenye kapu moja, tuone namna ambavyo tutatambua mahitaji yao na kitakachotusaidia ni utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua umri unawatofautisha, lakini pia jiografia inaweka tofauti ya mahitaji, elimu walizonazo pia inaweka tofauti ya mahitaji yao, na pia hata na jinsia. Kwa hiyo, ningependekeza kuwe na kitengo hicho na kitengewe fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vijana kwa kuwa wana nguvu, wana uwezo na wana maarifa, lakini wana upungufu, tunahitaji kuwajengea uwezo; lakini je, tunahitaji kuwasikiliza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na ninampongeza Mheshimiwa Waziri, ameanzisha vijana *platforms*. Ninaomba zile vijana *platforms* ziende mpaka ngazi ya kata. Zikifanyika katika ngazi ya halmashauri, changamoto ni kwamba wapo vijana ambao hawawezi kufika, ama kwa sababu ya miundombinu, ama kwa sababu ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende mpaka ngazi ya kata, tuwasikilize vijana hawa, wana mawazo, wana maoni, wana ujuzi, wana vitu vyao, tuwasikilize ili tuweze kuwagawanyia fursa kulingana na mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, pamoja na hayo, tunajua kwamba ili kutengeneza fursa za ajira, tunahitaji kutazama mambo kadha wa kadha. Moja ni mafunzo ya ujuzi kwa vijana wetu. Hawa vijana wapo makundi mengi sana. Wapo wenye elimu ya darasa la saba, wasio nayo, wenye *Form Four*, wenye *Diploma*, wenye *Degree* na wana mahitaji ya ajira pamoja na fursa za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutazame kwa kuhakikisha kwamba tunatengeneza mwongozo wa mafunzo ambao utawakamata vijana wote hawa ambao utakwenda kuwasaidia kuwapa ujuzi na kuwapa maarifa kulingana na sekta zao na eneo ambalo wanafanyia kazi au eneo ambalo wanahitaji kujiendeleza. Kwa hiyo, tunaweza tukaandaa *short courses* au *short contents* ambazo zitawasaidia vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba suala la ujasiriamali na kuwajumuisha vijana katika maeneo yale ya upatikanaji wa fedha. Tunajua kuna elimu tofauti, tunajua kwamba wanahitaji mitaji, lakini ninaomba tuwe na mwongozo wa kuwasaidia vijana hawa katika eneo hili la ujasiriamali, na kuwajumuisha katika upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja, tunahitaji mazingira wezeshi kwa ajili ya kuwawezesha vijana wetu. Kwa mfano, bodaboda tumewapa vijana, na tumewakopesha katika zile 10% na wapo watakaokuja kukopa, lakini vilevile wengine watakwenda kwenye kilimo. Wanapopita barabarani, kuna

changamoto za kuadhibiwa kwa sera fulani fulani hasa za kukamatwa na kupigwa faini, na wanapopigwa faini tunawarudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria kwa mfano kijana ambaye anabeba gunia moja, anachajiwa labda shilingi 20,000 au 30,000 ya faini njiani. Tayari umeshamfilisi; iwe ni bodaboda, iwe anafanya shughuli za ujasiriamali katika kilimo. Kwa hiyo, tuone sera zetu na mazingira yetu yawe wezeshi kwa ajili ya kuwasaidia vijana wetu kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna taasisi ambazo zinaajiri, tuone namna ambavyo tunaweka *incentives;* iwe ni *tax incentives* kwa zile taasisi ambazo zitaajiri vijana, iwe pia ni kwa kupata *access to the capital incentives,* tuweze kuona namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie mambo mawili ya mwisho. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, tumepata shilingi bilioni 200 na tunashukuru kwamba vijana wengine wamependekeza kuwa na benki, Wizara itazame, lakini ninapendekeza namna ambavyo fedha hizi zitawafikia vijana, tuone *routs* ziwe tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona ile *cheque* wakati inakabidhiwa inakwenda *CRDB Bank*, lakini tuone benki ambazo zipo katika halmashauri zetu ziweze kutoa fursa ili vijana wetu waweze kupata hizi fedha katika maeneo wanapoishi bila kuingia gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuishauri Serikali katika eneo moja. Eneo lingine ni suala la kuweza kutengeneza mazingira ya vijana kutimiza masharti.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa hawana *NIDA*, wala hawana leseni ya biashara. Katika ngazi za halmashauri na ngazi ya kata tuone namna ya kuwa na ofisi moja ambayo itawahudumia vijana hawa kwa wakati, na pia kwa urahisi ili kuweza kutimiza masharti ya mikopo na kuweza ku-*access* hizi fursa ambazo tunazitengeneza kupitia Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nuwas.

Waheshimiwa, tumemaliza wachangiaji. Ni nafasi sasa ya Mtoa hoja kuja kuhitimisha hoja yake. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Joel Arthur Nanauka.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuhitimisha hoja baada ya michango mizuri sana ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeanza kwa kuwashukuru kwa namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa umakini mkubwa sana na kila mchango uliokuwa unatolewa ulikuwa unaona kabisa inatoka moyoni, nikimaanisha kwamba Bunge hili lina dhamira njema na limeweka vijana katikati ya ajenda za muhimu katika mijadala yetu. Kwa hiyo, niwapongeze sana na niwashukuru sana pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi ambayo yamezungumzwa, yamegusia ushauri, na ninapenda kukiri kwamba yale yote ambayo yametolewa kama sehemu ya ushauri, sisi kama Wizara pamoja na watendaji tunayachukua, tutayafanyia kazi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo masuala kadhaa ambayo ninaomba niyatolee ufafanuzi ili kuendelea kuwa pamoja katika namna ya uelewa, lakini pia kupata ufahamu mpana katika maeneo ambayo nilieleza katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kabisa, ninaamini kwamba sisi wote kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunakubaliana kwa pamoja na dhamira ya Mheshimiwa Rais kuhusiana na kuwawezesha vijana wa nchi hii. Dhamira hii ameionesha hata kabla ya kuiunda Wizara hii ya Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anatoa ahadi kipindi cha kampeni katika ahadi zake hasa zile ahadi za siku 100 hadi 13 Wizara ilikuwa haijaundwa bado, lakini ulikuwa unaona kwamba Mheshimiwa Rais alikuwa na lengo mahususi kuhusiana na uwezeshaji wa vijana. Katika ahadi zake 13, ahadi sita ziligusa moja kwa moja maisha ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuja akihutubia Bunge, wakati analifungua Bunge hili, tutakumbuka alizungumza mambo mengi sana yanayohusiana na vijana. Ukipitia katika kile kitabu chake cha hotuba utagundua kuna mambo kama 13 mahususi ambayo aliyagusia yanahusiana na uwezeshaji wa vijana kiuchumi, kijamii, kisiasa, na pia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hilo, ningependa kwa mara nyingine tena niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na vijana wa Tanzania kwa ujumla kwamba Mheshimiwa Rais anayo dhamira ya dhati ambayo hajaifanya tu kwa maneno, lakini ameendelea kuitekeleza kwa vitendo kwenye masuala ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kumekuwa na sera ambazo zinaongoza masuala ambayo yanahusiana na vijana. Tumekuwa na Sera yetu ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 ambayo kupitia Sera hiyo Serikali imekuwa na mkazo mkubwa sana katika masuala mbalimbali ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumesikia katika baadhi ya michango ambayo imetolewa hapa kwamba ipo sheria iliyopitishwa ya Manunuzi ya Umma *(PPRA)* inayotaka taasisi kutenga 30%, na katika hizo, 10% ni kwa ajili ya vijana. Sheria hii

ilitungwa kwa sababu ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba Serikali inapoweka sera, inakuwa na nia ya dhati kuingiza utekelezaji katika vitendo. Leo ninapozungumza, mwaka 2025 peke yake vijana walioingia katika Mfumo wa *NeST* wameweza kupata *tender* za thamani ya shilingi bilioni 13.2. Hii yote ni kumaanisha kwamba Serikali haizungumzi tu uwezeshaji wa vijana, lakini pia inatoa fursa katika maeneo hayo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, leo tunazungumza mikopo ya 10%, mikopo hii pia ni matokeo ya Sera ya Maendeleo ya Vijana. Ilipotengenezwa sheria ya kutoa mikopo hii katika Serikali za Mitaa, ni kwa sababu ya uboreshaji ambao umetokana na uundwaji wa sera ya maendeleo ya vijana. Ndiyo maana, Mheshimiwa Rais alitoa agizo alipoingia madarakani, turejee Sera ya Maendeleo ya Vijana ili kuiboreshsa zaidi. Sasa hivi tunayo sera ya mwaka 2007, na toleo jipya la mwaka 2024 ambalo limelenga maeneo mahsusi ya kuwezesha vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwamba, pamoja na mambo ya jumla tunayoyazungumza, lakini tunao utekelezaji mahususi ambao tunautekeleza kwa kutumia sera hii. Sera hii uzuri wake pia, imetengeneza mkakati wa utekelezaji kati ya mwaka 2024 mpaka 2034.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati huo wa utekelezaji, yapo masuala ambayo yanahusisha sekta binafsi, sawasawa na maono yetu na mpango wetu wa mwaka 2050 ambao unataka sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi ambao wanahusiana na masuala ya vijana pia wachangie maendeleo ya vijana katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, katika utekelezaji wa afua za vijana, pamoja na juhudi ambazo Serikali inazifanya, tunayo mahusiano mazuri na sekta binafsi kwa kupitia miongozo ambayo Serikali imeweka na tutahakikisha pale

ambapo bado kuna *gaps,* tutatumia mikakati hiyo ambayo tumeweka ili kutekeleza masuala yanayohusiana na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno la pili ambalo limezungumzwa kwa mapana sana, na nikiri kwamba limetolewa ushauri mwingi sana, na sisi tumeupokea, ni eneo la mikopo. Limezungumzwa kwa mapana na hoja nyingi zinazungumzia juu ya uboreshaji wa vigezo vya mikopo, juu ya urahisi wa vijana kupata mikopo na masuala yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe maelezo machache kwenye eneo hili. Kwanza, ningependa kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna mabadiliko na maboresho makubwa sana yamefanyika katika utoaji wa mikopo hasa inayotolewa katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Kupitia mwongozo mpya ambao ninao hapa, unaitwa *Youth Development Fund Operation Guidelines,* tumeboresha maeneo kadhaa ambayo ningependa niyataje kwa ufupi ili pia tuweze kuyafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo vijana walikuwa wakilalamikia lilikuwa eneo la riba, kwamba ilikuwa ni kubwa. Kupitia mwongozo huu kwa sasa, riba imeshuka sana, na hata hatuiti riba, tunaita *administrative costs,* kwa sababu, asilimia ambayo wanachajiwa kwa muda wote wa mkopo, hata kama amekopa miaka mitatu yote, ni asilimia tano, siyo kwa mwaka ni kwa miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia tatu ni kwa ajili ya taasisi ya kifedha ambayo inatusaidia kutoa mafunzo na usimamizi, asilimia moja ni kwa ajili ya bima, asilimia moja inayobakia ni kwa ajili ya kurudisha kwenye mfuko ili ule mfuko uwe ni *revolving.* Kwa maneno mengine ni sawa na kusema kwamba, masharti ya riba yamekuwa ni madogo sana kwa ajili ya mikopo ambayo inatolewa na Serikali kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo lilikuwa linazungumzwa sana ni eneo la ukopaji wa mtu mmoja mmoja badala ya kukopa kwa vikundi. Mwongozo wetu wa sasa hivi unaturuhusu kufanya hivyo. Hivi ninavyozungumza, katika ripoti

ambayo niliisoma hapa, vikundi ambavyo tumewapa na wapo watu binafsi ambao tayari pia tumewapatia mikopo hii ambayo inatokana na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ili pia kuthamini vijana ambao wana kampuni binafsi au wameanzisha juhudi zao wenyewe binafsi za kuweza kutekeleza malengo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo limeboreshwa ni eneo la *grace period*. Nilizungumza katika hotuba yangu pia kwamba, sasa hivi kijana akikopeshwa fedha hii ambayo inatoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, anapewa miezi mitatu kabla hajaanza kulipa deni lake. Anapewa miezi mitatu ya kuboresha biashara yake, hata kama biashara inaendelea, Serikali imesema tunakupa miezi mitatu kwanza, uongeze mtaji wako wa uzalishaji, baada ya miezi mitatu ndiyo utaanza kulipa deni lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara nyingine tumezipa miezi sita, na nyingine kama za uzalishaji kwa mfano, kama samaki, visima vya samaki au kwenye kilimo, wanalipa mpaka baada ya miezi minane, hawadaiwi chochote na hawatakiwi kulipa jambo lolote lile. Jambo hili pia tumelifanya kama sehemu ya kuboresha mikopo hii kwa ajili ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo lilikuwa linalalamikiwa ni dhamana, kwamba kijana akienda anahitaji kupewa dhamana. Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tumezungumza katika hii ripoti, katika muda mfupi tangu Wizara hii imeundwa, tumetoa zaidi ya shilingi milioni 400, na hakuna kijana yeyote aliyepata fedha hizo ambaye ameombwa dhamana ya aina yoyote katika mkopo ambao tumempatia. Dhamana tunayohitaji sisi kwa walio katika vikundi, kikundi chao ndiyo kilikuwa dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunampa *asset,* kama ni pikipiki, au guta, ama *truck* la kufanyia biashara, ile *asset* tunayompa ndiyo inafanyika kuwa dhamana, haiitaji nyumba, haiitaji kiwanja, shamba wala kitu chochote kile, kwa sababu, hayo ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba turahisishe upatikanaji wa mikopo kwa vijana wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie, huo ndio mwelekeo wa Wizara. Katika fedha ambazo tutaendelea kuzitoa za mikopo, hayo ndiyo masharti ambayo tumeyaweka, ambayo ni masharti nafuu ambayo tunaamini mtu yeyote na kijana yeyote yule mwenye nia ya dhati anaweza pia kuyakamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tumeboresha ni eneo la usimamizi. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza hapa kwamba, vijana wanapewa mikopo lakini baada ya hapo pia inakuwa ni changamoto wao kuweza kurejesha, kwa sababu ya ufahamu na ujuzi wa biashara na elimu ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeingia makubaliano na baadhi ya taasisi za kifedha tayari, ambazo zenyewe kazi yake mojawapo ni kutoa mafunzo kwa vijana kabla hawajapata mkopo, lakini pia kipindi chote wakati wanahudumia ule mkopo, taasisi hizi za kifedha huwa zinaendelea kutoa mafunzo kwa ajili ya hawa vijana ili kuhakikisha wanafanyiwa *mentorship* ili wawe na uwezo wa kukuza biashara zao pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia pia kuondoa *defaulters* wengi katika hii mikopo kwa kuzingatia kwamba mikopo hii dhamira yake ni kwamba, akirudisha waweze kukopeshwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo pia *cycle* ya mkopo tumeipunguza sana. Kwa sasa hivi, akisha-*apply* tuna siku 14 za uchambuzi, baada ya hapo tuna siku 10 nyingine za kufanya uhakiki, na baada ya hapo kuna siku 10 zinazofuata kwa ajili ya kufanya *disbursement*. Kwa hiyo, ndani ya mwezi mmoja, tunakuwa tuna uwezo wa kufanya uhakiki unaojitosheleza na kuweza kutoa hiyo mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mikopo tuliyoitoa Mwanza, walikuwa wameomba mwezi wa 12 na mwezi wa Kwanza tuliweza kuwapatia pale vikundi viwili. Kikundi kimoja shilingi milioni 100 kwa ajili ya ufugaji wa Samaki, na kikundi kingine cha Buswelu tuliwapatia shilingi milioni 100 ambao wanafanya shughuli za usafirishaji wakiwa na maguta pamoja na pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, maboresho makubwa sana yamefanyika katika suala zima la mikopo na ninaomba mwendelee kuiunga mkono Serikali na dhamira ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwezesha vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ambalo Waheshimiwa Wabunge wameliongea kwa dhamira ya dhati sana kwamba, bado fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni chache sana. Ninakubaliana na mawazo hayo kwa kuangalia wingi na mahitaji ambayo tunayo katika sekta mbalimbali za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kukumbusha kwamba, Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana kwa miaka mingi tangu kuanzishwa kwake, umekuwa ukitengewa shilingi bilioni moja. Kuna baadhi ya miaka fedha hiyo pia ilishindikana kutoka kwa sababu za kibajeti. Kwa mara ya kwanza mwaka huu, bajeti hii, tumeleta mezani shilingi bilioni tano, mara tano zaidi ya fedha ambayo ilikuwa inatengwa kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea kwenye ripoti yangu, katika mwaka wa fedha uliopita tulitengewa shilingi bilioni moja. Leo ninavyozungumza, Serikali haijaweka tu shilingi bilioni moja, tayari imeweka shilingi bilioni 2.5 zaidi ya ile ambayo mwanzoni ilikuwa imetajwa pale. Maana yangu ni nini? Pamoja na uchache na uhaba tunaouona katika fedha hizi ambazo zimetengwa sasa hivi, lakini ukweli ambao hatuwezi kuupinga ni kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa zaidi katika fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kwamba, kwa sababu tunaanza, baadaye zitaendelea kuongezeka kadiri mipango inavyokuwa inaendelea. Kwa hiyo, ningeomba Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono katika hili ambalo tumeliweka mezani, ili tuanzie hapa tukiwa tunaendelea kujenga zaidi na kuongeza wingi wa fedha hizi ambazo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zimetolewa kwenye Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana siyo fedha pekee za vijana

ambazo wanazi-*access* katika nchi hii. Ninashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wameongea, na wametoa mawazo mazuri sana ya namna bora ya ku-*manage* fedha hizi katika namna ambayo wameitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba vijana wa nchi hii, bado ukiacha shilingi bilioni tano ambazo tumeziomba hapa, yapo maeneo mengine mengi ambayo, kama ambavyo Wabunge wamechangia, vijana wanaendelea kuwezeshwa katika namna mbalimbali na nitatoa mifano michache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumekuwa tukizungumzia hata 10% ya uwezeshaji hapa, kwa mwaka jana pekee tuliona shilingi bilioni 130 zilienda kwa ajili ya hawa vijana. Hiyo ni kwa ajili ya vijana peke yao katika ile asilimia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya tatizo ambalo tumekuwanalo ambalo ndiyo tunajaribu kulitibu sasa ni kwamba, pamoja na utokaji wa fedha nyingi kwa makundi ya vijana, zile zinazorudi ni chache. Sasa mfuko usipokuwa ni *revolving fund,* zisiporudi maana yake zinatukosesha uwezo. Nitatoa mfano kidogo, katika shilingi bilioni 130 ambazo zimetolewa kwenye asilimia nne kwenye Serikali za Mitaa, zimerudi shilingi bilioni 49 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata leo sisi kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuna shilingi bilioni 3.9 ambazo zipo nje, ambazo vijana wameshindwa kuzirudisha bado. Ndiyo maana katika mkakati wetu, tumeona pamoja na kutoa fedha kama Mwalimu Nyerere alivyosema, kwamba fedha siyo *engine* ya maendeleo peke yake, tunahitaji uwekezaji katika ufahamu, tunahitaji uwekezaji katika tabia, tunahitaji uwekezaji katika nidhamu ya hawa vijana pia, ili waweze kuwa na uwezo wa kurudisha hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na uchache unaoonekana, lakini bado naweza nikasema kwamba, Serikali imeongeza nguvu na kasi kubwa zaidi katika uwezeshaji wa vijana katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningeomba nilizungumzie kwa sehemu, ni kuhusiana na kufikisha taarifa kwa vijana. Nakubaliana na michango mizuri sana ya Waheshimiwa Wabunge, ambayo wameitoa kwamba bado tunahitaji kuongeza nguvu na mbinu zaidi za kuwafikia vijana katika maeneo mbalimbali. Ninapenda kusema mbele ya Bunge lako hili Tukufu kwamba, tutaendelea sisi kama Wizara, tumetumia mbinu mbalimbali kama ambavyo tumeeleza katika ripoti yetu kuwafikia vijana *physically* kwa maana ya uso kwa uso, kutumia teknolojia na tunaamini bado lipo kundi lingine ambalo linakosa taarifa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge, Serikali ina mtandao mpana mpaka ngazi ya kata, na bado tunaendelea kujipanga vizuri hasa tunapoendelea kuimarisha Muundo wa Wizara yetu, ili kuhakikisha kwamba vijana walioko mpaka ngazi ya chini kabisa na wenyewe pia wanafaidika na kupata taarifa kwa wakati ili na wenyewe waweze kutumia fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kujifunza, kutokana na yale ambayo tumeanza kuyafanya sasa, na kutokana na masomo tunayoyapata na michango yenu, tutaendelea kuboresha namna bora ya kuwafikia vijana wa nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea ushauri mzuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Yunus, hasa ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu. Ninapenda kukiri sera yetu ya maendeleo ya vijana kipengele cha 3.13 kinazungumza katika ukurasa wa 33 kuhusiana na eneo mojawapo la msingi ni kushughulika na makundi maalum hasa ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea maoni aliyoyatoa, tutaenda kuyaboresha na kuaona namna bora ya kuwashirikisha kwa karibu sana katika kuhakikisha kwamba nao pia wanakuwa sehemu ya msingi na ya muhimu katika shughuli zinazohusiana na mambo ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni la kuhusiana na ukuzaji wa ujuzi kwa vijana. Ninashukuru kwa maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kwamba changamoto nyingi za vijana ziko katika ujuzi ambao unaendana katika ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoeleza katika hotuba yetu, tutashirikiana na kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo inashughulika na mambo ya ajira na maoni ambayo mmeyatoa, tunayapokea na sisi kama Serikali tutayafanyia kazi, tutayachakata na mwisho wa siku tutaona namna bora pia ya kuweza kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni mingi sana, nami niseme kwamba michango hii mingi mliyoitoa inaenda kutujenga na kutufanya tuwe bora zaidi katika utekelezaji wetu. Kama tulivyokuja hapa katika Bunge lililopita, maswali na maoni ya Waheshimiwa Wabunge waliyoyatoa tulikwenda kuyafanyia kazi na leo tumefika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba yale ambayo mmeyasema pia tutaenda kuyafanyia kazi kwa ufanisi ili kuhakikisha vijana na nchi hii, sawasawa na maneno ya Mheshimiwa Rais, wanaachiwa tabasamu kwa maendeleo ambayo watayapata na uwezeshaji ambao atawapatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa shukrani za mwisho, ningependa niseme jambo moja. Ni kweli kwamba changamoto za vijana ni nyingi, lakini ninaamini ni uamuzi wetu sisi kuamua, tunaziona kwa namna gani, na tunazitafsiri vipi? Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, vijana wa nchi hii ni *asset* kubwa sana katika kuhakikisha nchi hii inasogea hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, katika majimbo yetu, katika shughuli zetu, tuendelee kuwafanya vijana kama sehemu muhimu pia ya kuhakikisha wanashiriki katika mambo tunayoyafanya, lakini pia tunaruhusu ujuzi wao, nguvu yao na ubunifu wao uwe sehemu ya muhimu sana katika shughuli zetu za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni moja ilituma watu wawili kwenda kutafuta soko la viatu kwenye kisiwa. Walivyokwenda siku wamerudi kutoa ripoti, wa kwanza alivyorudi kutoa ripoti akawaambia *management* kwamba nimekuta katika kisiwa kile watu hawavai viatu kabisa, ina maana hakuna soko kabisa katika kisiwa kile, tuachane na habari za kwenda kupeleka viatu kuuza. Mtu wa pili alipoingia kutoa taarifa yake, akasema, naomba tujipigie makofi, kwa sababu nimeenda nimekuta hakuna watu wanavaa viatu, ina maana sisi ndiyo tutakuwa kampuni ya kwanza kuuza viatu katika kisiwa kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana na Tanzania tunapowaangalia na udhaifu walionao na changamoto walizonazo, tuwaangalie upande kama *asset* kwa ajili ya nchi yetu. Tutumie ujuzi wao, tutumie ubunifu wao na ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Nasi kama Wizara tunasema, changamoto zote zilizopo tutazigeuza, tutazifanya kuwa ni fursa ili kuhakikisha vijana wa Tanzania wanakuwa ni sehemu muhimu ya kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ambao wametoa mchango wao mzuri na ushauri wao wa mara kwa mara ambao umetusaidia pia kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kuboresha kazi zetu pia. Pia, kwa namna ya kipekee ninawashukuru Wabunge hasa wanaotokea katika kundi la vijana ambao wamekuwa mstari wa mbele kutoa ushauri wa mara kwa mara, wakichangia, na pia kutoa maelekezo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, ninaomba nichukue fursa hii kuwashukuru Mawaziri wenzangu ambao nao pia wamekuwa ni nguzo muhimu ya kunishauri na kunisaidia pale ambapo ninahitaji kuongozwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee sana, ninaomba nitoe shukrani zangu kwa Wabunge wote ambao tumejadili bajeti hii, wale waliozungumza, wale waliotuma michango yao kwa maandishi, wale waliotuma *message* na wale ambao hata wataongea na kunishauri baada ya hapa,

nimepokea michango yenu, nimeielewa michango yenu na nitaifanyia kazi kwa maslahi mapana ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 104 – Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management Division*…………………Sh.9,027,961,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*….….......Sh.1,300,225,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division*…………Sh.1,656,533,000
Kifungu 1004 - *Procurement and Supplies Management Unit*………………………………………Sh.1,252,675,000
Kifungu 1005 - *Information and Communication Technology Unit*………………….……Sh.1,158,654,000
Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit*……………………..Sh.1,107,200,000
Kifungu 1007 - *Monitoring and Evaluation Unit*.........Sh.1,195,491,000
Kifungu 1008 - *Government Communication Unit*…Sh.1,134,083,000
Kifungu 1009 - *Legal Services Unit*……………………Sh.1,177,706,000
Kifungu 2001 - *Youth Coordination and Mobilization Division*……………………………………..Sh.2,235,000,000

Kifungu 2002 - *Civic Education, Pariotism and Uhuru Torch Coordination Division*…………Sh.2,622,933,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2004 - *Youth Business Development and Economic Empowerment Division*…Sh.4,574,937,000

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. Bila shaka tupo Kifungu 2004.

**MWENYEKITI:** Bado hatujafika, uliomba kwenye Kitabu cha Maendeleo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 2005 – *Youth Welfare and Upbringing Division* …………………..Sh. 1,660,866,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 104 – Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana**

Kifungu 2001 – *Youth Coordination and Mobilization Division*........................... Sh. 394,153,000
Kifungu 2002 – *Civic Education, Patriotism and Uhuru Torch Coordination Division*.....Sh. 458,881,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2004 – *Youth Business Development and Economic Empowerment Division*………………Sh.5,000,000,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado Shaibu.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninasimama chini ya Kanuni ya 125(2). Kanuni ambayo inanipa nafasi kama Mbunge kuweza kutoa hoja ya kuondoa shilingi moja katika kifungu chochote kile. Kwa hiyo, ninaomba kutoa hoja kwamba ninaondoa shilingi moja katika Kifungu cha 2004 kinachohusu uwezeshaji wa vijana kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado, kabla hujaondoa shilingi, utoe maelezo, ueleze *issue* yako ni nini hapo?

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kutoa maelezo.

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi, dakika mbili.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa kwa ufupi kabisa. Kama ambavyo imeelezwa kwenye hotuba na kwenye randama...

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Huu siyo wakati wa Taarifa. Mheshimiwa Ado, endelea.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imeelezwa na kuoneshwa kwenye randama kiwango cha fedha ambacho kimetengwa ni shilingi 5,000,000,000. Imeelezwa vizuri sana, hizi ni fedha za kuwawezesha vijana kiuchumi na kati ya hizo shilingi 300,000,000 zitatumika kwa ajili ya elimu ya ujasiriamali na shilingi 4,700,000,000 zitatumika kwa ajili ya kuviwezesha vikundi 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama umesikiliza tangu asubuhi, ipo kiu ya kwamba hizi fedha hazitoshi. Nilitaka kupata maelezo ya ziada kuna vigugumizi gani? Kuna shida gani kwa Serikali kuzichukua fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha vijana kwenye maeneo mengine, kwenye Wizara nyingine ikiwemo hii *commitment* ya Serikali ya shilingi bilioni 200 ili kuipa nguvu zaidi Wizara ya Vijana? Ninaomba maelezo ya msingi katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Ado kuhusiana na swali alilouliza. Wizara ya Maendeleo ya Vijana katika hotuba yetu tumeeleza katika ukurasa wetu wa 18, moja ya kitu ambacho tunafanya ni kuandaa mwongozo wa namna ambavyo fedha za uwezeshaji wa vijana zinaweza zikawa na utaratibu mmoja wa kutolewa unaounganisha sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Ado, sawasawa na maelezo niliyoyatoa katika ule ukurasa wa 18, kinachofanyika sasa hivi na Serikali ni kuandaa utaratibu mzuri ambao utakuwa na ufanisi ambao pia utawasaidia vijana wenyewe kuhakikisha fedha hizo zinafika kwa wakati, na pia zinatekeleza majukumu yaliyomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, sisi kama Wizara tunaendelea kuandaa mfumo. Nimeeleza katika hotuba yangu kwamba tunaandaa mfumo ambao utakuwa ni kanzidata itakayoturahisishia kuwafikia vijana hao ili fedha zitakapotolewa kusiwe na changamoto nyingine za kuwafikia vijana kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Ado aweze kuondoa shilingi ili pia atuunge mkono na ninamhakikishia Serikali itaendelea kuboresha masilahi ya vijana wa nchi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, baada ya maelezo hayo ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninasema baada ya ufafanuzi huo, ninaiondoa hoja yangu kwa imani kwamba Serikali itakuwa imetusikia vijana wa Bunge hili na itatafakari hoja yetu na kuona namna ya kuipa nguvu zaidi Wizara ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi kujadili Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na limekamilisha kazi zake, na kwamba taarifa ya Kamati ya Matumizi sasa ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninaomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja kutolewa na kuungwa mkono, sasa nitawahoji, kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwenye Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2026/2027.

*(Hapa ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi kutangaza rasmi kwamba Bunge hili sasa limekubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwenye Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, kwa mwaka 2026/2027 kwa kauli moja. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, ninachukua nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri Joel Nanauka, kwa kazi nzuri ya kuelewesha Waheshimiwa Wabunge na kujibu hoja zao kwa ufasaha mzuri sana. Pia, ninawapongeza Makatibu Wakuu ambao unafanya nao kazi, Bi. Jenifa Omolo na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Mapana na watendaji wote ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Ni wazi kwamba hoja za Wabunge zilikuwa nyingi na mlizisikia, lakini Mheshimiwa Rais ana nia njema na makusudio na vijana wa Tanzania. Amewapa kazi hii ninyi mumwakilishe katika kuyafikia yale maono ya vijana. Sisi kama Bunge tunawatakia kazi njema, mafanikio mema na Bunge litaendelea kutoa kila linalowezekana kwa upande wa *support* kwenye kazi hii kubwa ambayo Wizara hii imekabidhiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Bunge hili sasa mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.08 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 21 Aprili, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*